# Nipashe

Jumanne Januari 7, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580121


www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710



Nipashe TESA
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Waliofuata shule kilomita 5 sasa kupumua kwa shule mpya kijijini
Hii ndio haki na gharama zake
Mhitimu uhandisi 'anayepiga kiwi' sasa ajutia safari ya shule
SHIDA YAANZIA UKUNGA...
Mtoto mwenye ulemavu alia kusoma na kuandika, juhudi zaishia hewani

UKURASA 13




## RC aamuru kung'olewa mabango yanayodai kutibu nguvu za kiume

UKURASA 21

# Mbunge CCM adaiwa kuibiwa mil. 440/-

**ANAYETUHUMIWA** 'kumwingiza mjini' aburuzwa kortini kwa... *Endelea ukurasa wa 2*



## UTATA MTUPU WIZI VIFAA NIDA

UKURASA 2

Mtumishi wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida), Wilaya ya Arusha, Neema Nkya, akionyesha kwa wanahabari makasha matupu baada ya wezi kuiba vitendea kazi vya mamlaka hiyo, zikiwamo kompyuta na kamera. PICHA NDOGO: Makasha matupu. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**MZAZI ASHTAKIWA KWA KUKEKETA WATOTO WATATU**

MKAZI wa Kivule jijini Dar es Salaam, Cosmas Chacha (45), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu...

UKURASA WA 3

**MAZUNGUMZO DPP, KIGOGO WA TAKUKURU YAVUNJIKA**

UPANDE wa utetezi katika kesi ya kutakatisha Sh. bilioni 1.477 inayomkabili Mkurugenzi wa zamani wa Mipango...

## MBARONI KUFUKUA KABURI LA MTOTO

UKURASA 12




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play | App Store


**MICHEZO** **SIMBA, YANGA SASA VITANI MAPINDUZI CUP** UK. 32

**MAONI, KATUNI UK.6**

HABARI KITAIFA

# Mbunge CCM adaiwa kuibiwa mil. 440/-

**Na Gideon Mwakanosya, SONGEA**

MFANYABIASHARA wa duka la pembejeo katika Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma, Cosmas Haule (42), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi mkoani humo akikabiliwa na shtaka la wizi wa kuaminiwa wa Sh. milioni 440.

Mamilioni hayo ya shilingi yanadaiwa kuwa mali ya Mbunge wa Viti Maalum, Jackline Ngonyani (CCM).

Wakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Kanda ya Songea, Shabani Mwigole, jana alidai mahakamani mbele ya Hakimu Mkazi Kussaga Majinge kuwa kati ya Novemba 27, 2015 na Desemba 31, 2019, katika Benki ya CRDB Tawi la Songea, mshtakiwa, aliiba Sh. milioni 440, mali ya Jackline Ngonyani kinyume cha sheria.

Mwigole alidai kuwa mshtakiwa aliiba fedha alizopatiwa na mbunge huyo kwa lengo la kuzihifadhi kwenye yake ya benki, akifafanua kuwa badala ya kuzihifadhi, mfanyabiashara huyo anadaiwa kuzitumia kwa mambo yake binafsi, kinyume cha makubaliano yao.

Hata hivyo, mshtakiwa alikana shtaka hilo na kesi hiyo itatajwa tena mahakamani hapo Januari 17, mwaka huu.

Hakimu Mkazi Majige alisema dhamana ya mshtakiwa iko wazi kwa masharti ya kuwa na wadhamini watatu, wenye mali zisizohamishika zikiwa na thamani ya Sh. milioni 133 kila mmoja.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein (wa pili kushoto), akimsikiliza Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), Mussa Ramadhani Haji akitoa maelezo ya kitaalamu ya ujenzi wa Tangi la Maji Saateni Zanzibar, baada ya kuzindua mradi huo, ikiwa ni sehemu ya shamrashamra ya miaka 56 ya Mapinduzi ya Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Utata waibuka wizi vifaa vya Nida

**Na Daniel Sabuni, ARUSHA**

ZIKIWA zimebaki siku 13 kabla ya kumalizika kwa siku 20 zilizoongezwa na Rais John Magufuli kukamilisha usajili wa laini za simu kwa mfumo wa vidole gumba, watu wasiojulikana wanadaiwa kuiba vifaa nyeti vya usajili katika Ofisi za Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) zilizoko Halmashauri ya Arusha.

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha, Jerry Muro, alithibitisha kupokea taarifa hiyo usiku wa kuamkia jana, huku kukiwa kumeibuka utata wa muda uliotumiwa na watu hao kutekeleza wizi huo na namna walivyoingi ndani.

Kwa mujibu wa taarifa ya awali ya Mkuu wa wilaya huyo, vifaa vilivyoibwa ni pamoja na kompyuta tatu, kamera mbili za kisasa na vifaa vingine ambavyo hadi sasa havijajulikana.

Alidai mazingira ya namna vifaa hivyo vilivyoibwa yanaacha maswali, kwa kuwa mlango wa chumba cha kuhifadhi vifaa hivyo haukuvunjwa na walinzi wa zamu wanadai hawajaona mtu yeyote aliyepita navyo kuanzia Ijumaa hadi jana, Jumatatu.

Muro, akiwa eneo la tukio akifuatana na Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Arumeru, alidai tukio hilo ambalo ni la pili tangu litokee la aina hiyo mwaka jana katika makao makuu ya Nida wilayani Arumeru, alifananisha na hujuma akidai hakuna palipovunjwa na walinzi wanajieleza kwa utatanishi.

"Ninachoweza kusema; vyombo vya ulinzi na usalama viko kazini na wataalamu wa alama za vidole kutoka makao makuu ya polisi mkoani Arusha, tutatoa taarifa zaidi kwa kuwa OCD na timu yake wanaendelea na uchunguzi," alisema.

Mkuu Wilaya huyo pia alitoa siku tatu kwa wahusika kurejesha kwa amani, vinginevyo atakayekutwa navyo, atachukukiwa hatua kali kwa mujibu wa sheria.

"Naomba nieleweke hapa atakayekutwa navyo, atachukuliwa kama mwizi wa nyara za serikali kama ngozi ya twiga, chui au meno ya tembo, hatuwezi kuvumilia hujuma hizi ambazo naweza kusema zinakwamisha maendeleo ya nchi kutokana na zoezi la kusajili simu ambalo limeongezewa siku 20 na Mheshimiwa Rais John Magufuli," alionya.

Muro pia alitoa wito kwa wenye vibanda vya kompyuta na vya kurikodi muziki, kutonunua vifaa vyovyote bila nyaraka halali, akifafanua kuwa kuna uwezekano wakanunua vifaa vilivyoibwa na kuingia kwenye matatizo makubwa.

Aliweka wazi kuwa kuna watumishi wanashikiliwa ili kuisaidia uchunguzi wa Jeshi la Polisi, miongoni mwao ni baadhi ya wafanyakazi wa Nida.

Mlinzi wa zamu, Lino Tiobiki, aliyekuwapo katika eneo la tukio, alidai inawekana uhalifu huo ulitokea mchana kwa kuwa wanahakiki milango kila jioni wanapoingia lindoni na kuongeza kuwa jana asubuhi, mhudumu aliyetambulika kwa jina la Wilson Laiser, alikuta mlango ukiwa wazi alipoingia kazini.

Tiobiki alidai kuwa mhudumu huyo aliendelea na usafi hadi pale ofisa wa Nida, Neema Nkya, alipofika na kubaini kuna vifaa havikuwapo na ndipo taarifa ikatolewa kwa Jeshi la Polisi.

## Chadema Kusini yajiweka sawa

**Na Sabato Kasika**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Kanda ya Kusini, kimewataka wanachama wake wanaotaka kuwania nafasi mbalimbali katika uchaguzi mkuu, wajitokeze kwa wingi ili wapimwe utendaji wao mapema kabla ya uchaguzi huo unaotarajia kufanyika mwishoni mwa mwaka huu.

Wanachama hao ni wale wa ndani na nje ya kanda hiyo, ambao watakuwa na nia ya kuwania udiwani, ubunge ukiwamo wa viti maalum, katika uchaguzi huo utakaoshirikisha vyama mbalimbali vya siasa.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Chadema, Kanda ya Kusini, Suleiman Mathew, alipokuwa akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu na kuelezea mikakati ya chama hicho, kwa ajili ya uchaguzi huo.

"Kanda ya Kusini inajumuisha mikoa ya Lindi, Mtwa na Ruvuma...tumekutana na kuzungumzia jambo hilo, na tumewaomba wanachama wetu wanaotaka kuwania uongozi wajitokeze tuwapime utendaji wao," alisema Mathew.

Alitaja utaratibu wa kugombea kwamba, mwanachama anayetaka udiwani awasilishe kusudio lake la kugombea kwa maandishi kwenye kata husika na nakala ipelekwe katika wilaya kwenye kata anayotaka.

"Anayetaka kugombea ubunge awasilishe kusudio lake la kugombea kwa Katibu Mkuu kupitia kwa Katibu wa Kanda na nakala ya kusudio hilo awasilishe kwa Katibu wa Mkoa, ambao kuna jimbo analotaka kugombea limo na kwa Katibu wa Jimbo husika analotaka kugombea," alisema. Mathew.

Alisema kwa anayetaka kugombea urais anatakiwa kuwasilisha kusudio lake la kugombea kwa Katibu Mkuu wa chama taifa, hivyo wanachama wote wenye sifa wamekaribishwa kutangaza kusudio la kugombea nafasi hizo.

"Tujitokeze mapema ili tujiandae mapema kwa ajili ya uchaguzi mkuu, mwaka 2020 ni uchaguzi mkuu, katika kanda yetu tunazo jumla ya kata 515 na majimbo 27 ya uchaguzi," alisema.

Mwenyekiti huyo aliongeza kusema: "Tunatoa wito kwa wanachama wote walioko ndani na nje ya kanda yetu wenye nia ya kugombea nafasi za udiwani na ubunge ukiwamo wa viti maalum na urais wajitokeze sasa ili waweze kupimwa utendaji wao mapema katika maeneo wanayogombea," alisema.

HABARI KITAIFA

## Uelewa changamoto kwa uandikishaji NEC

**Na Said Hamdani, LINDI**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imesema moja ya changamoto zonazoikabili mara kwa mara ni jamii kushindwa kufahamu au kutofautisha kati ya uchaguzi mkuu na wa serikali za mitaa.

Hayo yalielezwa na Makamu Mwenyekiti wa NEC, Jaji Mbarouk M'barouk, wakati akifungua mkutano wa NEC na wadau wa uchaguzi mkoani Lindi.

Jaji Mbarouk alisema yapo maeneo wananchi wake wamekuwa na mtizamo tofauti, wakifikiri uchaguzi wa Serikali za MItaa na uchaguzi zote zinasimamiwa na tume hiyo, jambo ambalo sio la kweli.

Alisema uchaguzi wa Serikali za Mitaa unasimamiwa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), wakati NEC inawajibika na usimamizi wa uchaguzi mkuu pekee, ambao unahusisha Rais, wabunge na madiwani.

"Wananchi walio wengi katika baadhi ya maeneo wanashindwa kutofautisha uchaguzi upi unasimamiwa na Tamisemi na upi Tume ya Taifa ya Uchaguzi," alisema Jaji Mbarouk.

Alisema kwa kutotambua umuhimu wa jambo hilo, tume imeamua kushirikisha wadau kushiriki katika michakato ya uchaguzi kwa lengo la kuwa karibu nao, ili kujenga imani kwa wananchi na kuweka uwazi wa utekelezaji wa majukumu yake.

Alisema tume inaamini kila kundi la wadau, wakiwamo viongozi wa kisiasa, dini, mila, watu wenye walemavu na wanahabari wana umuhimu wake katika zoezi zima la uchaguzi.

Jaji M'barouk alisema uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura unasimamiwa na kuendeshwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na maelekezo ya tume, huku akisisitiza viongozi wa vyama vya siasa watapatiwa maelekezo kwa mfumo wa vijitabu.

Pia aliviomba vyama vya siasa na wadau wengine kuzingatia sheria za uchaguzi, kanuni za uboreshaji daftari na maelekezo kwa vyama vya siasa, huku akiwataka kutoa taarifa sahihi na kwa wakati ili kila mwananchi mwenye sifa ya kuandikishwa ajiandikishe.

Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura unafanyika kwa kutumia teknolojia ya kielektroniki ya Biometriki (BRV) ambavyo huchukuwa taarifa za kibaiolojia na kuzihifadhi katika kanzi data (Database).

Uboreshaji huo kwa mkoa wa Lindi kwa mujibu wa NEC unatarajia kufanyika kwa siku saba, kuanzia Januari 12 hadi 18, mwaka huu.

# Mazungumzo kati ya DPP, kigogo Takukuru yavunjika

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa utetezi katika kesi ya kutakatisha Sh. bilioni 1.477 inayomkabili Mkurugenzi wa zamani wa Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Kulthum Mansoor, umedai mahakamani mazungumzo ya kukiri makosa na Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) yamevunjika.

Wakili wa utetezi Elia Mwingira, alitoa madai hayo jana kwamba awali walimwandikia DPP barua ya kuomba kukiri makosa yanayomkabili mshtakiwa, lakini mazungumzo yamevunjika.

Alitoa madai hayo mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Godfrey Isaya.

Awali, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa na kwamba upelelezi wake bado haujakamilika.

Wakili wa utetezi Mwingira, alidai kuwa kwa kuwa mazungumzo na DPP yamevunjika upande wa Jamhuri uharakishe upelelezi.

Wakili Wankyo alidai wataelekeza wapelelezi kuhakikisha wanakamilisha upelelezi katika maeneo yaliyobaki.

Hakimu Isaya alisema mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu na kesi hiyo itatajwa Januari 20, mwaka huu.

Mansoor anakabiliwa na mashtaka manane ya kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha Sh. bilioni 1.477.

Inadaiwa katika tarehe tofauti kati ya Januari 2013 na Mei 2018, mshtakiwa alighushi barua ya ofa ya Agosti 13, 2003 kwa madhumuni ya kuonyesha kuwa barua hiyo imetolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo huku akijua kuwa sio kweli.

Katika mashtaka ya pili, inadaiwa kati ya Januari 2012 na Mei 2017, maeneo ya Upanga ndani ya Wilaya ya Ilala, mshtakiwa kwa kudanganya alijipatia Sh. milioni 5.2 kutoka kwa Alex Mavika, mfanyakazi wa Takukuru kama malipo ya kiwanja kilichopo Kijiji cha Ukuni Bagamoyo.

Pia inadaiwa kati ya tarehe hizo, Mansoor alijipatia Sh. milioni tatu kutoka kwa Wakati Katondo kama malipo ya kiwanja kilichopo maeneo ya Kijiji cha Ukuni, wilayani Bagamoyo mkoani Pwani.

Mshtakiwa huyo pia alijipatia Sh. milioni tano kutoka kwa Ofisa wa Takukuru, Gogo Migutah, kama malipo ya kiwanja kilichopo eneo hilo hilo. Katika mashtaka ya tano, inadaiwa Mansoor alijipatia Sh. milioni saba kutoka kwa Ekwabi Majungu, ambaye ni ofisa wa Takukuru kama malipo ya kiwanja hicho.

Mansoor anadaiwa kati ya Januari 2012 na Mei 2017, maeneo ya Upanga jijini Dar es Salaam, akiwa Mkurugenzi wa Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini alijipatia Sh. milioni saba kutoka kwa John Sangwa kama malipo ya kiwanja cha eneo hilo.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa akiwa mwajiriwa wa Takukuru, alijipatia Sh. milioni tano kutoka kwa Rose Shingela kwa ajili ya malipo hayo.

Katika mashtaka ya utakatishaji fedha, inadaiwa kati ya Januari 2013 na Mei 2018 huko maeneo ya Upanga, mshtakiwa alijipatia Sh. 1,477,243,000 wakati akijua kuwa fedha hizo ni haramu na ni zao la kosa tangulizi la kughushi.



Baadhi ya wazazi katika Manispaa ya Shinyanga, wakipeleka watoto wao, kuwaandikisha kwa ajili ya kujiunga na darasa la awali na la kwanza katika Shule ya Msingi Town, iliyopo katika manispaa hiyo, jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mzazi kortini tuhuma kukeketa watoto 3

**Na Hellen Mwango**

MKAZI wa Kivule jijini Dar es Salaam, Cosmas Chacha (45), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, akikabiliwa na mashtaka matatu ikiwamo kuwakeketa watoto wake na kuwasababishia maumivu makali sehemu zao za siri.

Baba huyo wa watoto wa kike watatu wenye umri chini ya miaka (18), alisomewa mashtaka yake mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashid Chaungu.

Wakili wa Serikali, Faraji Nguka, alidai kuwa Desemba 8, 2019, eneo la Kivule jijini Dar es Salaam, Chacha akiwa baba mzazi na mwenye jukumu la kumlea mtoto wake (jina limehifadhiwa), alimpeleka kwenda kukeketwa hali iliyomsababishia maumivu makali sehemu zake za siri.

Katika shtaka la pili, inadaiwa mtuhumiwa huyo katika tarehe hiyo eneo la Kivule, akiwa baba mzazi na mwenye jukumu la kumlea mtoto (jina limehifadhiwa) alimpeleka mwingine kukeketwa na kumsababishia maumivu makali sehemu zake za siri.

Katika shtaka la tatu, Ngukah alidai, Desemba 8, 2019 eneo hilo la Kivule, mshtakiwa huyo akiwa baba mzazi na mwenye jukumu la kumlea mtoto wake (jina limehifadhiwa), alimpeleka mtoto mwingine tena kukeketwa hali iliyomsababishia maumivu na kusababisha kupata majeraha sehemu zake za siri.

Hata hivyo, mshtakiwa alikana mashtaka hayo, upande wa mashtaka ulidai upelelezi wa kesi hiyo bado unaendelea na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu Chaungu akitoa masharti ya dhamana, alimtaka mshtakiwa huyo kuwa na wadhamini wawili mwenye barua na vitambulisho watakaosaini bondi Sh. milioni tano.

Mshtakiwa huyo ameshindwa kutimiza masharti ya dhamana na kupelekwa rumande hadi kesi itakapotajwa tena Januari 20, mwaka huu.

# Ofisa polisi, wenzake kortini tuhuma za utakatishaji fedha

**Na Hellen Mwango**

WATU wanne akiwamo Ofisa wa Jeshi la Polisi wa Chuo cha Polisi Moshi (CCP), Emmanuel Mkulia (44) na wenzake watatu, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, wakikabiliwa na mashtaka matatu ya kusababisha hasara, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha Sh. 798,789,272, mali ya Jeshi la Polisi Tanzania.

Mbali na afande Mkulia, washtakiwa wengine ni, mtaalamu wa kompyuta, Dolnald Mhaiki (39), wafanyabiashara Abdi Ally (48) na Mohyadin Hussein (56).

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Salum Ally.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa kosa la kwanza, washtakiwa hao wanakabiliwa na tuhuma za kulisababishia hasara Jeshi la Polisi Tanzania.

Wankyo alidai kuwa kati ya Machi 19, na Oktoba 18, 2013 jijini Dar es Salaam washtakiwa walilisababishia Jeshi la Polisi hasara ya Sh. 798,789,272.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa siku na tarehe ya tukio la kwanza, washtakiwa walijipatia fedha hizo kwa njia ya udanganyifu kutoka Jeshi la Polisi kwa kudanganya wamewekea mfumo wa taarifa za waliokamatwa na wanaoshikiliwa katika jeshi hilo.

Ilidaiwa kuwa washtakiwa walitoa hati ya uongo wakionyesha mfumo huo umewekwa katika vituo vinane wakati wakijua wameweka katika vituo vinne.

Upande huo wa Jamhuri ulidai kuwa siku na tarehe ya tukio la kwanza na la pili, washtakiwa walitakatisha fedha hizo wakati wakijua na zao la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Washtakiwa hawakutakiwa kukana mashtaka hayo.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika, uliomba tarehe ya kutajwa.

Hakimu Ally alisema kwa kuwa Mahakama yake haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi, washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote.

Alisema washtakiwa wapelekwe mahabusu na kesi hiyo itatajwa Januari 20, mwaka huu.




Ofisa wa Chuo cha Polisi Moshi (CCP), Emmanuel Mkulia (kushoto) na wenzake wakiwa chini ya ulinzi wa askari polisi baada ya kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam jana, na kusomewa mashtaka matatu, ya kusababisha hasara, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha Sh. 798,789,272 mali ya Jeshi la Polisi Tanzania. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kesi kutekwa MO yapigwa kalenda

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imepiga kalenda kesi ya kutekwa kwa mfanyabiashara Mohammed Dewji maarufu kama MO inayomkabili dereva wa taksi Mousa Twaleb na wenzake wanne ambao bado hawajakamatwa na kufikishwa mahakamani hapo imepigwa kalenda mpaka Januari 21, mwaka huu.

Kesi hiyo ilitajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashid Chaungu baada ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, aliyepangiwa kusikiliza kesi hiyo kwenda likizo.

Wakili wa Serikali, Faraji Nguka, alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika, hivyo aliiomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu Chaungu alisema kesi hiyo itatajwa Januari 21, mwaka huu na mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu.

Watuhumiwa wengine ambao upande wa mashtaka inawatafuta ni raia wanne wa Msumbiji na mmoja wa Afrika Kusini, wanaodaiwa kumteka bilionea huyo.

Washtakiwa hao ambao hawajakamatwa ni Phila Tshabalala raia wa Afrika Kusini, Henrique Simbine, Daniel Manchice, Issac Tomo na Zacarious Junior wote raia wa Msumbiji.

Katika kesi hiyo inadaiwa Mei Mosi na Oktoba 10, 2018, katika maeneo ya Jiji la Dar es Salaam na Johannesburg Afrika Kusini, kwa makusudi washtakiwa wote kwa pamoja waliendesha genge la uhalifu.

Pia inadaiwa Oktoba 11, mwaka juzi maeneo Hoteli ya Colloseum wilayani Kinondoni Dar es Salaam, Twaleb pamoja na watu wengine ambao hawapo mahakamani, walimteka nyara MO kwa nia ya kumuhifadhi kwa siri na kumuweka maeneo ambayo ni hatari.

Kadhalika, inadaiwa Julai 10, mwaka juzi maeneo ya Mbezi Beach wilayani Kinondoni, Dar es Salaam, Twaleb alitakatisha fedha ambazo ni Sh. 8,000,000 wakati akijua fedha hizo ni kosa la kushiriki genge la uhalifu na makosa ya kupanga.

MO alitekwa nyara Oktoba 11, mwaka juzi alfajiri maeneo ya Hoteli ya Colloseum wakati akienda kufanya mazoezi na alipatikana Oktoba 20, mwaka huo huo katika eneo la Gymkhana.

# Wanafunzi 270 Musoma wanasoma chini ya mti

**Na Ahmed Makongo,**

**MUSOMA**

ZAIDI ya wanafunzi 270 wa Shule ya Msingi Wanyere B, Kata ya Suguti wilayani Musoma mkoani Mara, wanasoma wakiwa chini ya mti kutokana na upungufu wa vyumba vya madarasa.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Peter James, aliiambia Nipashe kuwa wanafunzi hao wanasoma wakiwa katika hali hiyo kutokana na upungufu wa vyumba vitatu vya madarasa.

James alisema kutokana na hali hiyo, walimu wamekuwa wakikumbana na vikwazo katika ufundishaji na uelewa wa wanafunzi hao unakuwa ni mgumu kutokana na mazingira mabaya ya ujifunzaji na ufundishaji.

"Ni kweli kuna uhaba wa madarasa matatu kwa ajili ya watoto 274 katika shule yetu, wanasomea nje kwenye mti kutokana na upungufu huo," alisema.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Wanyere iliko shule hiyo, Thomas Musiba, alisema kutokana na hali hiyo, wananchi walihamasishwa na kuanza kuchangia fedha ili kutatua tatizo hilo.

Hata hivyo, Musiba alidai fedha zilizochangwa na wananchi kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa, "zilichakachuliwa na viongozi waliokuwa madarakani na kusababisha ujenzi huo kutokufanyika".

Alidai wananchi walichanga fedha hizo kuanzia mwaka 2017 hadi mwaka jana kutokana na agizo la Mkuu wa Wilaya, Dk. Vicent Naano.

"Wananchi walianza kuchanga fedha hizo tangu mwaka 2017 hadi mwaka 2019 na kwa kila kaya kuchangia kiasi cha 15,000, waliochelewa kuchanga, walipigwa faini ya Sh. 10,000 kwa kila kaya," alidai.

**"Ni kweli kuna uhaba wa madarasa matatu kwa ajili ya watoto 274 katika shule yetu, wanasomea nje kwenye mti kutokana na upungufu huo," alisema.**

# Mbinu kudhibiti ujangili zazaa matunda

**Na Christina Haule, MOROGORO**

MBINU za kudhibiti ujangili zinazofanywa na serikali zimeanza kuzaa matunda baada ya pembe za ndovu mbili na vipande 13 kukamatwa Desemba, mwaka jana mkoani hapa.

Mhifadhi Mkuu wa Mamlaka ya Wanyapapori Tanzania (Tawa) Kanda ya Magharibi-Iloga Serous, Noti Mgaya, alisema hayo jana wakati akitoa taarifa ya ushirikiano wa Jeshi la Polisi, Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa) na Tawa kuhusu matukio ya ujangili katika kipindi cha Desemba, mwaka jana, pekee.

Mgaya alisema jitihada kubwa zilizofanywa na serikali katika kudhibiti ujangili hifadhini, zimezaa matunda na nyara nyingi zinaonekana ni za mauaji ya tembo kuanzia Julai, mwaka jana na kurudi nyuma.

Awali, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, alisema kupitia ushirikiano huo, wamekamata watuhumiwa saba wa makosa mbalimbali yakiwamo ya kupatikana silaha zilizotengenezwa kienyeji, pembe za ndovu mbili na vipande 13 vya pembe za ndovu vyenye thamani ya Sh. 137,576,250.

Kamanda Mutafungwa alisema tukio la kwanza lilitokea Desemba 27, mwaka jana saa 1:00 usiku katika kitongoji cha Kimbwala, Kisaki wilayani Morogoro.

Alisema askari polisi kwa kushirikiana na askari wa Hifadhi ya Taifa Mikumi, wakiwa doria, walimwona mtu na kumtilia shaka na kuanza kumfuatilia.

Mutafungwa alisema walipomsogelea alikimbia kisha kujitosa kwenye Mto Kimbwala na kudondosha mfuko wa sandarusi uliokuwa na pembe mbili za ndovu zenye uzito wa kilo 3.10 zikiwa na thamani ya Sh. 34,155,000.

Kamanda Mutafungwa alisema mtuhumiwa huyo anaendelea kutafutwa na Jeshi la Polisi baada ya kukimbia.

Alisema tukio lingine lilitokea Desemba 30, mwaka jana saa 10:00 usiku katika Kijiji cha Isongo wilayani Ulanga. Katika tukio hilo askari wakishirikiana na askari wa wanyamapori pori la akiba la Selous, waliwakamata watuhumiwa watano wakiwa na vipande 13 vya pembe za ndovu vyenye uzito wa kilo 13.9, mkia wa tembo, magobole matatu yaliyotengenezwa kienyeji na risasi 7 za shotgun zilizotengenezwa kienyeji walizokuwa wakizitumia katika ujangili, vyote kwa pamoja vikiwa na thamani ya Sh. 103,412,250.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Abdalah Mputa (36) na Fanuel Mbena (34) wakazi wa kijiji cha Isongo Ulanga, Fikiri Salum (28) mkazi wa kijiji cha Iputi, Salum Ally (22) mkazi wa kijiji cha Chigandugandu wilayani Ulanga na Novatus Kadinda (34) mkazi wa kijiji cha Isongo Ulanga.

Katika tukio la tatu, alisema Juma Kitambi (31) na Charles Godson (40) wakulima na wakazi wa Ruhembe wilayani Kilosa, wamekamatwa na polisi kwa tuhuma za kumiliki bunduki aina ya Break Action shotgun bila kuwa na kibali ikiwa na maganda tisa ya risasi aina ya shotgun ikiwa imehifadhiwa kwenye mfuko wa sandarusi kisha kufichwa kichakani.

Kamanda Mutafungwa alisema watuhumiwa hao pia walikamatwa na nyama ya nyati kilo moja na kwamba baada ya mahojiano walikiri kumiliki silaha kinyume cha sheria na kuitumia katika ujangili.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC), Emmanuel Ndomba, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu sheria za utoaji ushuru na mizigo bandarini. Kushoto ni Mkurugenzi wa Udhibiti Uchumi wa Wakala huo, Nahson Sigalla. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Upungufu wa madaktari bingwa waikwaza Tumbi

**Na Futuna Seleman, KIBAHA**

SHIRIKA la Elimu Kibaha mkoani Pwani limeadhimisha miaka 50, huku likikabiliwa na changamoto kubwa ya uchakavu wa miundombinu na upungufu wa madaktari bingwa katika Hospitali yake ya Rufani ya Tumbi.

Hospitali hiyo inakabiliwa na changamoto hizo licha ya kuhudumia wastani wa wagonjwa 400 kila siku, asilimia 80 wakiwa ni waathirika wa ajali za barabarani.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hilo, Robert Shilingi, aliyasema hayo wakati wa maadhimisho ya miaka 50 ya shirika hilo.

"Asilimia 80 ya waathirika wa ajali za barabarani za mkoa wa Pwani huudumiwa katika Hospitali ya Tumbi na asilimia 8 ya waathirika wa ajali za barabarani kwa nchi nzima hupata huduma katika Hospitali ya Tumbi, " alisema Shilingi.

Changamoto nyingine aliitaja ni upungufu wa wafanyakazi. Hata hivyo alisema katika kupambana na changamoto zilizoainishwa shirika linatekeleza ipasavyo mpango mkakati wa miaka 2016/17-2021, kualika wawekezaji ili kuitumia ardhi ya shirika kama chanzo cha mapato.

Kuhusu malengo ya kitaasisi kwa mujibu wa mpango mkakati wa 2016/2017 2020/2021 ni kuboresha afya na kupunguza maambukizi ya virusi vya ukimwi na ukimwi kutekeleza ipasavyo mpango mkakati na endelevu wa taifa wa kupambana na rushwa.

Aidha, alisema katika kufikia maono ya kuwa kituo bora katika kupambana na maradhi kituo kimeweza kuanzisha mfumo wa kielektroniki unaofahamika GoT-HoMIS yaani mfumo wa habari wa menejimenti.

"Mfumo huu kuanzishwa na kuwekwa katika Hospitali ya Tumbi ili kudhibiti makusanyo ya mapato na kusimamia data (taarifa) za wagonjwa, serikali ilikubali mfumo huo uwekwe katika hospitali zote za umma nchini... hospitali hii imekuwa kitovu cha mafunzo ya mfumo huu, "alisema.

Akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Pwani kufungua rasmi maadhimisho hayo, Ofisa Elimu Mkoa huo, Maulid Bundala, alisema shirika limekuwa na mchango mkubwa kwa wananchi wa Pwani na nje ya mkoa huo katika utoaji wa huduma bora katika sekta ya elimu na afya.

## Waziri Mpango aagiza kuimarisha ulinzi fedha

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, amewaagiza Katibu Mkuu, Doto James, na Mhasibu Mkuu wa Wizara hiyo, Francis Mwakapalila, kuhakikisha wanaimarisha usalama katika mifumo ya fedha, ili kuondoa uwezekano wa kudukuliwa na kusababisha hasara kwa serikali.

Dk. Mpango alitoa agizo hilo jijini Dar es Salaam jana, alipofungua kikao kazi cha wahasibu wa taasisi za umma, ikiwa ni maandalizi ya taarifa za fedha za majumuisho za mwaka 2018/2019.

Waziri huyo pia aliwataka wahasibu kuimarisha taaluma hiyo na kuongeza nguvu ya kupambana na vitendo vyote vinavyokinzana na maadili yao ikiwamo wizi, ubadhirifu wa mali za umma na rushwa.

Dk. Mpango alisema hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya wahasibu wanaokiuka maadili na kujihusisha na vitendo vinavyosababisha hasara kwa serikali.

Alipongeza uanzishwaji wa mifumo mingi ya ukusanyaji wa mapato na maduhuli ya serikali, ikiwamo mifumo ya kihasibu na rasilimali za umma kwa njia ya kielektroniki, inayokidhi viwango vya kimataifa.

Dk. Mpango alisema dhamira ya serikali ni kuboresha utoaji wa huduma kwa jamii kwa kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato na maduhuli pamoja na kusimamia vizuri matumizi ya fedha na rasilimali zote za umma.

"Nimefurahi sana kuona kwamba ndani ya kipindi kifupi cha miaka minne tangu serikali ya awamu ya tano iingie madarakani, mmeanzisha mifumo mingi na madhubuti ya kukusanya mapato na maduhuli ya serikali, pamoja na mifumo ya kuhasibu rasilimali za umma yenye kukidhi viwango vya kimataifa," alisifu na kueleza kuwa:

"Hii ni ushahidi bayana kuwa, mnatafsiri kwa vitendo dhamira na dira ya serikali hii chini ya uongozi wa Rais John Magufuli ya kusimamia rasilimali za nchi kwa manufaa ya wananchi hasa wanyonge.

"Mimi waziri mwenye dhamana ya usimamizi wa fedha na rasilimali za umma, ninaona fahari kuwa na wataalamu wazalendo na wabunifu kama ninyi."

Alisema matarajio ya serikali ni kuona mifumo hiyo inatumika vizuri, kwa weledi na uadilifu katika kutoa huduma bora.

Mhasibu Mkuu, Mwakapalila, alisema hatua ya kutumia mfumo wa kielektroniki unaiweka Tanzania kuwa nchi ya kwanza barani Afrika kutayarisha hesabu za majumuisho kwa kutumia mfumo huo ulioandaliwa na wataalamu wake wa ndani.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Utitiri vyama hewa ushirika uwe fundisho*

**KUNA** taarifa kwamba serikali inakusudia kuvifuta vyama hewa vya ushirika 3,436, kutokana na kubainika kuwa vimekosa sifa ya kuendelea kuwapo.

Serikali imesema kuwa itavifuta kwa mujibu wa sheria ya ushirika baada ya kuvifanyia uchuguzi na kubaini kuwa havipo katika maeneo ambayo vinaonyesha vilisajiliwa wala viongozi wake hawajulikani.

Mpango huo ulitangazwa na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari Jumapili jijini Dodoma.

Hasunga alisema mpaka sasa daftari la mrajisi wa vyama vya ushirika nchini lina jumla ya vyama 11,149, vilivyoandikishwa, na kwamba kati ya hivyo 3,436 havijulikani vilipo na vyama 1,250 vimesinzia na vyama 6,463 vipo hai.

Kwa mujibu wa waziri huyo, kutokana na kuwapo kwa vyama hewa katika daftari la mrajisi wa vyama vya ushirika, aliagiza kutangaza kwenye gazeti serikali kusudio la kuvifuta vyama hivyo kwa mujibu wa sheria ya vyama vya ushirika kifungu 100, ambacho kinaeleza kuwa chama kinaweza kufutwa kwa sababu mbalimbali.

Kufuta vyama vya ushirika ni hatua ya kusikitisha, lakini ni uamuzi wa maana kwa kuwa bila kufanya hivyo, hawatanufaika kwa njia yoyote.

Ikumbukwe kuwa lengo kuu la kuanzishwa kwa vyama vya ushirika, lilikuwa ni kuwawezesha wakulima, hivyo kama inafika mahali baadhi vikatoka katika msingi huo, hakuna sababu ya kuvifumbia macho.

Umuhimu wa vyama vya ushirika ulibainika baada ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, kuvifuta kutokana na kasoro kadhaa, lakini baada ya kuona kuwa uamuzi huo uliwaathiri walengwa, serikali yake iliamua kivirejesha.

Kwa hiyo tunaunga mkono kusudio la serikali la kuvifuta vyama vya ushirika hewa, ambavyo malengo yake hayajulikani, ili kuepusha kutumika vibaya kimyume cha malengo ya ushirika nchini.

Hatutarajii kuwa kutakuwapo na lawama kuhusiana na hatua hiyo kwa kuwa sababu ambazo zinaweza kusababisha chama cha ushirika kufutwa ni kutokuwa na ofisi tangu kuandikishwa, hakijulikani kilipo na viongozi wake hawafahamiki na hawapatikani.

Sababu nyingine ni kushindwa kutekeleza takwa la kisheria la kutayarisha makisio ya mapato na matumizi na kuyapeleka kwa marajis kuyapitia, kutayarisha taarifa ya mwaka, kufunga mahesabu na kuyapeleka COASCO, kwa ukaguzi na kutofanya mikutano ya mwaka ya wanachama wote na bodi zao.


Hata hivyo, tunaona kuna umuhimu kwa mamlaka zenye dhamana ya kusimamia ushirika kuwa na utaratibu wa kuratibu na kufuatilia vyama vya ushirika kila wakati, kwa lengo la kuhakikisha kuwa vinatekeleza matakwa ya kisheria.

Kwa kufanya hivyo, hakutakuwapo na uwezekano wa kuibuka kwa vyama hewa kama ilivyotokea hadi ukafikia utitiri wa vyama 3,436.

Hali hii iliachwa hivi inaweza kusababisha vyama hewa vya mifukoni kama hivi kutumia ujanja kufanya utapeki kwa kutumia mwavuli wa ushirika nchini.

Bila shaka maagizo ya Waziri Hasunga kwa mrajisi wa vyama vya ushirika nchini ya kuzingatia sheria No. 6 ya mwaka 2013 ya vyama vya ushirika kifungu 100 na kanuni ya 26, ambayo inamtaka mrajisi anatakiwa kutoa notisi ya kusudio la kutaka kufuta vyama vya ushirika kwenye gazeti la serikali kwa muda wa siku 90.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Faini hizi ni za kukomoa au kurekebishana?

Na Salome Kitomari

**HAKUNA** ubishi kuwa kwa sasa barabarani, hasa jijini Dar es Salaam, kuna nidhani kubwa kwa madereva kuheshimu alama za barabarani na watembea kwa miguu.

Natamka ni nidhamu, ikilinganishwa na miaka ya nyuma ilikuwa vurugu tupu, kwa kuwa mwenye nguvu ndiye alipita, madereva wa daladala na baadhi ya magari binafsi ambao walitanua na kupita maeneo yasiyotakiwa bila ya kuguswa na yeyote, jambo lililoharibu barabara nyingi.

Ilikuwa kama mashindano ya watu wasio wastaarabu barabarani kiasi cha kuwaweka kwenye hali ngumu watumiaji wengine wa barabara.

Kwa sasa, askari wa usalama barabarani wapo katika maeneo mengi na wengine hujificha, ili kuona utekelezaji wa utii wa sheria bila ya shuruti na inapolazimika sana wanatumia shuruti, kwa kuandika faini kwa madereva.

Kwa sasa, maeneo yenye vibao vya '50' kwa barabara za mikoani, madereva wanaheshimu na hakuna mwendokasi, kwa kuwa wanajua watapigwa picha na kukamatwa mbele kwa kuonyeshwa picha ya gari, mwendo aliozidisha na kibao cha '50' kinavyoelekeza.

Jitihada hizi, operesheni za kila mara mara na ubunifu umesidia kupunguza ajali nyingi za mwisho wa mwaka ambazo zilitokana na mwendo kasi au uzembe wa madereva.

Kwa sasa wako makini, kwa kuwa wanajua nini kitafuata iwapo watavunja sheria hizo.

Pamoja na pongezi ya kazi nzuri inayofanywa na askari hao lakini yapo maeneo yanahitaji marekebisho makubwa kwa kuwa sasa imegeuka kuwa adhabu na maumivu kwa madereva kuliko inavyofikiriwa. Jiji la Dar es Salaam linaoongoza kwa faini ambazo ni za kuumiza au kubambikia madereva na hilo nitalisema nikiwa na mifano halisi ya maeneo ambayo ndiyo la askari kuvizia, jambo linalotoa taswira kwa sasa ni kuviziana zaidi kuliko kuwafanya madereva watii sheria bila shuruti.

Katika barabara ya Bagamoyo nyuma kidogo ya makutano ya barabara ya Goba na Bagamoyo, kwa dereva anayetokea Tegeta upande wa kushoto kuna kituo cha abiria wa daladala na nyuma kidogo kulikuwa na alama ya 'zebra' zilizofutika kwa sasa. Mbele kidogo, ndiko askari hujificha na kujitokeza kwa kasi barabarani wanapoona dereva hajasimama eneo hilo.

Kinachonisukuma kuandika haya ni iwapo askari hao wanajua kwamba alama za pundamilia zinaonyesha kuvuka kwa watembea kwa miguu zimechorwa na kuonekana kwa madereva au wanaamini kuwa barabara hiyo inatumiwa na madereva wenyeji kila siku hivyo wamekariri eneo hilo.

Kinachofanyika kwa askari wanapoona kuna mtu amesimama upande wowote wa barabara na gari likapita bila ya kusimama, wanamkamata na kuambiwa hajaheshimu alama za pundamilia na kuandikiwa faini. Lakini, cha kushangaza alama husika hazipo.

Cha kujiuliza hapo, askari wapo pale kukusanya mapato au kuangalia wakosaji ambao hawapo. Ninasema wakosaji hawapo kwa kuwa eneo hilo hakuna kibao wala alama kwenye lami zinazoonyesha dereva anapaswa kusimama kuruhusu watembea kwa miguu kupita. Eneo lingine ni Majumba Sita, baada ya kutoka Uwanja wa Ndege ukiwa unaelekea Ukonga, jijini Dar es Salaam, katika makutano ya barabara za Kinyerezi na Nyerere ambako kuna taa.

Eneo hilo lina askari wengi na kuna foleni. Kinachoviziwa hapo ni wale wanaoshindwa kukaa kwenye foleni ya mstari mmoja wakati wa kwenda na kurudi kutokana na mabadiliko ya barabara kuwa nyakati za asubuhi ni njia mbili kwenda mjini na njia moja kwenda Ukonga.

Mbaya zaidi hakuna kibao chochote cha kutoa elimu ya jambo hilo bali kinachofanyika ni kuvizia wakosaji wowote ili watozwe faini, jambo linaloonyesha kuwa hakuna nia njema ya kuwafanya madereva watii sheria bila shuruti bali kukusanya fedha kutoka kwao.

Sehemu nyingine ambazo ni maumivu kwa madereva ni kwenye makutano ya barabara ambako kuna taa, lakini hakuna taa za kuelekeza madereva wa pande nyingine bali wanapaswa kukadiria au kutumia akili za kuzaliwa na kwa dereva mgeni anajikutana kwenye wakati mgumu.

Mfano ukiwa umetokea TMDA unakwenda Ubungo hakuna taa ya kukuelekeza sasa unaruhusiwa kukatiza barabara hiyo na badala yake inaruhusu magari yanayokwenda mabibo ukipita ikiwa hivyo ni sawa, lakini iwapo utapita wakati magari yanayotoka Tabata kwenda Mabibo yanakatiza, linahesabiwa ni kosa na faini inamhusu dereva.

Eneo jingine ni Mwenge kwa anayetokea Coca Cola kuelekea Posta, akikatiza wakati magari yaliyotokea uelekeo wa Bagamoyo yanakatiza, inaonekana ni kosa au wakati yalizotokea Ubungo yanakatiza, ni kosa bali anatakiwa kusubiri yanayotoka upande aliyopo kuelekea Ubungo, ndiyo akatize.

Katika eneo hilo hali ni ileile kwa aliyetokea uelekeo wa ITV anakwenda Ubungo, akikatiza wakati magari mengine yanapishana, anakutana na askari waliojificha kwenye vituo wakiwawinda watu wa namna hiyo.

Pia madereva wanaotokea uelekeo wa Tegeta na kwenda Coca Cola nao wanasubiriwa kukamatwa na wale wanaotokea Ubungo wanataka kuingia barabara ya Bagamoyo.

Kwa ujumla, alama za barabarani hususani 'pundamilia' zimefutika kwenye maeneo mengi, kiasi cha kuwafanya madereva kutaabika na kushindwa kufanya maamuzi na kukutwa na mkono wa sheria.

# BARUA/ MJADALA

## *Mashabiki watani wa jadi tujifunze*

***Mhariri pole na majukumu,***

*HATIMAYE mechi ya Yanga na Simba imeshachezwa na timu hizo kutoka sare ya bao 2-2, zote zikiambulia pointi moja moja, huku kelele na majigambo za mashabiki wa timu hizo zikizua tafurani, wengi kufikia hadi kupigana.*

*Ni mechi iliyokuwa na msisimko mkubwa ndani na nje ya uwanja, ikishuhudiwa na maelfu ya mashabiki waliokuwa uwanjani, lakini maelfu ya Watanzania wakiifuatilia mechi hiyo kwa njia mbalimbali kama vile kutazama kwenye runinga, baadhi kusikiliza kupitia vituo vya radio na wengine walikuwa hawasikilizi kabisa mpira zaidi ya kupata taarifa au matokeo ya mechi kwenye simu, au mitandao ya kijamii.*

*Tumeshuhudi wengine wakizimia kutokana na kutoamini kilichotokea, ama kwenda uwanjani na matokeo mfukoni au kutohimili mihemko ya ushangiliaji, wengine hadi kupigana na kutoleana maneno ya karaha. Tunaamini kwamba soka ni mchezo wa furaha, hivyo haina budi wote bila kujali tofauti za tunakoshabiki baada ya mechi kuwa kitu kimoja, ili kusubiri matokeo ya mechi zijazo.*


*Kinachokera zaidi mechi imeshaisha, lakini baadhi ya watu wanaendeleza utani hadi kupigana na kutoleana lugha chafu, ingawa ndani ya Simba na Yanga utani ndio jadi yao. Niseme, isifikie hatua watu wakadhuriana, kushambuliana kwa kila namna.*

*Mwaka mpya sasa tushangilie kistaarabu, utani kawaida, lakini tusifikie hatua mbaya mpaka ya kugeuka kero kwa wengine.*

***Mdau wa Soka,***
***Kijitonyama, Dar es Salaam.***

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**




# Elimu nje ya mfumo rasmi nyeti sana, ichangamkiwe

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI ilianzisha programu ya mpango wa elimu ya msingi kwa watoto walioikosa (Memkwa), kwa ajili ya kuwezesha watoto kupata elimu nje ya mfumo rasmi na hivyo ili asiwepo mtu yeyote atakayekosa elimu nchini.

Hatua hiyo inatokana na ukweli kwamba, elimu ni silaha muhimu na mkombozi wa mtoto kifikra na inamuwezesha kutambua mazingira yanayomzunguka, hata kupiga hatua kimaendeleo kwa siku zake za usoni.

Kimsingi, Memkwa imegawanyika katika makundi rika mawili. Kundi rika la kwanza linajumuisha watoto walio na umri kati ya miaka 10 hadi 13, wanaosoma kwa miaka miwili hadi minne.

Baada ya hapo huruhusiwa kufanya mtihani wa darasa la nne na kundi la rika la pili, linajumuisha vijana walio na umri kati ya miaka 14 hadi 18, wanaofanya vizuri katika masomo yao, kisha wanaruhusiwa kujiunga na elimu ya mfumo rasmi.

Wakishafikia hatua hiyo, hufanya mtihani wa darasa la saba nawakifaulu wanaendelea na elimu ya sekondari. Hivyo ni wazi kwamba, wale ambao hawakupata elimu kwa mfumo rasmi bado wana nafasi ya kusoma.

Uamuzi huo wa serikali umechukuliwa kwa kutambua kuwa elimu ndiyo pekee inayoweza kumkomboa mtoto kifikra, hasa kwa kuzingatia kwamba elimu ni kati ya haki za msingi za kibinadamu.

Mwaka 1999 ndio Memkwa ilianzishwa kwa majaribio kwenye baadhi ya wilaya, zikiwamo Ngara mkoani Kagera, Masasi mkoani Mtwara, Songea Vijijini mkoani Ruvuma na Kisarawe mkoani Pwani.

Baada ya programu hiyo kuonyesha mafanikio, mwaka 2003 serikali ilianzisha madarasa ya Memkwa katika shule za msingi kote nchini lengo likiwa ni kuhakikisha wote waliokosa elimu rasmi wanaipata kupitia mpango huo.

Pamoja na juhudi hizo za serikali kutaka kuhakikisha Watanzania wanapate elimu, bado kumekuwapo tatizo kufuatia baadhi yao kutojua kusoma na kuandika.

Hiyo inatokana na kile kilichowahi kusemwa na bungeni na Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Injinia Stella Manyanya, kwamba asilimia 20 ya Watanzania hawajui kusoma na kuandika.

Waziri Manyanya, alisema hayo Septemba mwaka jana, alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum, Tasca-Restuta Mbogo (CCM) ,kwa niaba ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mbunge huyo alihoji kuwapo mpango wa serikali kurudisha elimu ya watu wazima iliyokuwpo katika miaka ya nyuma.

Kwa hali kama hiyo, ni wajibu wa kila Mtanzania kupambana na adui ujinga kutokana na ukweli kwamba, tayari serikali imeshatoa fursa kumwezesha kila aliyekosa elimu rasmi, kuipata kwa njia ya Memkwa.

Hata wale ambao ni watu wazima, bado wana fursa kwenye mfumo wa elimu ya watu wazima, ambao wanaweza kuutumia wakajua kusoma na kuandika kuliko kubweteka tu na kumkumbatia adui huo.

Ikumbukwe kwamba, kusoma na kuandika ni mwanga wa kumwezesha mtu kuendesha maisha yao kwa na hata kupambana na maradhi na umaskini pia kusaidia kuondokana na ugumu wa maisha. Kwa hiyo, Memkwa ni fursa nzuri kwa vijana wasiojiou kusoma na kuandika, ili waitumie waondokane na adui ujinga ambaye anaweza kusababisha washindwe kuendelea.

Mbali na hiyo, kwa sasa serikali inatoa elimu bure kuanzia msingi hadi kidato cha nne, hivyo sidhani kwa mazingira kama hayo ni rahisi kila mtoto kupata elimu, labda wasiwe makini na kujikuta wakitoka kapa.

Lakini ukweli uliopo, serikali imerahisisha njia ya kumwezesha mtoto wa Kitanzania na hata watu wenye umri mkubwa kuweza kupata elimu, kinachotakiwa ni kila mhusika kuchangamka tu.

Vilevile, siyo vibaya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) kuandaa mkakati wa kusaidia kupunguza idadi ya watu wasiojua kusoma na kuandika kwa kutambua kwamba ujinga ni adui wa maendeleo.

Jamii itambue kuwa iwapo kama watu wengi watakuwa hawajui kusoma na kuandika, itakuwa vigumu nchi hii kufikia Tanzania ya viwanda, ambayo inahimizwa kwa ajili ya maendeleo.

Hivyo, ni muhimu kurudi darasani kwa wale, ambao wameenda shule, lakini wakatoka bila kujua kusoma na kuandika na pia, ambao hawakubahatika kupata elimu, wajiunge na Memkwa au kisomo cha watu wazima.

Inawezekana, wapo baadhi ya watu wanaoona aibu kuhudhuria madarasa ya Memkwa au kisomo cha watu wazima, lakini watambue kuwa elimu haina mwisho na ina mchango mkubwa katika maendeleo.

Sensa ya mwaka 2012 ilionyesha kuwa asilimia 22 ya Watanzania walikuwa hawajui kusoma na kuandika na huenda takwimu hizo zikawa zimeongezeka au kupungua iwapo jamii itakuwa imetambua umuhimu wa elimu.



# Maziwa yatajwa tiba ya uzee, vidonda vya tumbo

**Na Dege Masoli, TANGA**

UNYWAJI maziwa umeelezwa kuwa na faida nyingi ikiwamo kuzuia uzee kabla ya wakati, ngozi kutokukunjamana na kuzuia meno kuuma hadi kufikia hatua ya kung'oa.

Kutokana na faida hizo, Watanzania wametakiwa kutilia mkazo unywaji maziwa ili kupata manufaa hayo pamoja na ulinzi wa mwili dhidi ya maradhi.

Hayo yalisemwa juzi na Meneja wa Vyanzo vya Maziwa kutoka kiwanda cha Tanga (Tanga Fresh), Nadomana Nyanga, baada ya waandishi wa habari kutembelea kiwandani hapo kwa lengo la kujionea mafanikio yaliyofikiwa katika kuboresha ubora wa huduma ya maziwa.

Nyanga alisema utafiti unaonyesha unywaji wa maziwa ni njia pekee inayoweza kusaidia mtu kuepukana na baadhi ya madhara yanayotokana na jamii kukosa utamaduni wa kutumia maziwa.

Alisema unywaji maziwa unasaidia kuondoa uzee, ngozi kukunjama kwa binadamu, kuzuia tatizo la meno kuuma na kusababisha hata hatua ya kung'olewa na kwamba njia kuu ni pamoja na kunywa maziwa bora ambayo hayajachanganywa na maji. Nyanga alisema endapo Watanzania watajiwekea utamaduni wa kunywa maziwa, matatizo yote hayo watayaepuka kutokana na ukweli kuwa yana virutubisho vingi ambavyo huufanya mwili uongeze kinga muda wote.

Aliongeza kuwa wakiwa wataalamu wa maziwa, wanajitahidi kuwahamasisha wananchi watumie maziwa kama kinywaji cha kawaida ili kuongeza kinga ya mwili na hatimaye kuwa na afya njema.

Kwa upande wake, mtaalamu wa mbuzi wa maziwa kutoka kituo cha utafiti wa malisho ya mifugo (Taliri) mkoani Tanga, Ayubu Kambadu,

alisema asilimia kubwa ya watu wamekuwa wakifika kituoni hapo wakisema kuwa unywaji wa maziwa ya mbuzi umekuwa ukiwasaidia kwa kiwango kikubwa kutibu matatizo ya vidonda vya tumbo hali inayosababisha kufanya utafiti kwa kina. Mtaalamu huyo alisema mbuzi wanaopata malisho mazuri na chakula bora wanauwezo wa kutoa maziwa lita mbili kwa siku na maziwa yake yana virutubisho vingi vinavyoweza kumsaidia binadamu aweze kuongeza kinga ya mwili na kuepukana na magonjwa yasiyo ya kuambukizwa.

Aliongeza kuwa wamekuwa wakizalisha mbegu bora za mbuzi wa maziwa na kwamba kwa sasa wamejipanga kuhakikisha wanaongeza mbegu bora ili kuwawezesha wananchi kununua kwa wingi na hatimaye kupata tiba ya tatizo hilo.



Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Atashasta Nditiye (katikati), akifurahia jambo na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), Mhandisi Japhet Maselle (wa pili kushoto), baada ya kumaliza zoezi la kukagua na kukishusha kwenye maji kivuko cha MV. Ilemela katika yadi ya Songoro, jijini Mwanza jana. Kivuko hicho, kina uwezo wa kubeba abiria 200 na magari 10 sawa na tani 100 na kimejengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 2.7. **PICHA: WUUM**

# Kivuko kipya kubeba abiria 200

**Na Mwandishi Wetu, MWANZA**

WAKAZI wa Ilemela mkoani jana walishuhudia kivuko kipya cha Kayenze-Bezi, MV. Ilemela kilichogharimu Sh. bilioni 2.7, kikishushwa kwenye maji baada ya kukamilika kwa ujenzi wake.

Ushushwaji wa kivuko hicho ulifanyika kwenye yadi ya Songoro iliyoko wilayani huko, mgeni rasmi akiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Uchukuzi na Mawasiliano), Atashasta Nditiye.

Nditiye alimshukuru Rais John Magufuli na serikali ya awamu ya tano kwa kuendelea kutimiza ahadi ya miradi mbalimbali ya maendeleo nchini.

"Hadi sasa, Mheshimiwa Rais tayari ameshatoa fedha zote kiasi cha Sh. bilioni 9.954 iliyokuwa imepangwa kwenye bajeti ya miradi ya maendeleo kwa ajili ya vivuko kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema kivuko cha MV. Ilemela kitakapoanza kutoa huduma, kitaondoa tatizo la usafiri kwa wananchi kati ya Kayenze na Kisiwa cha Bezi.

"Kivuko hiki kitakapoanza kutoa huduma ni dhahiri kuwa kitaondoa tatizo la usafiri kwa wananchi kati ya Kayenze na Kisiwa cha Bezi, hivyo kitainua maisha ya wananchi wa maeneo hayo kibiashara, kiuchumi na kijamii. Mara tu mtakapokamilisha majaribio, anzeni kutoa huduma," aliagiza.

Alitoa wito kwa watumishi wa Wakala wa Ufundi na Umeme (Temesa) kufanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kivuko hicho pamoja na vivuko vingine vinatunzwa vizuri na vinadumu kwa muda mrefu na kuhakikisha huduma zinatolewa kwa kuzingatia usalama wa abiria na mali zao.

Mtendaji Mkuu wa Temesa, Japhet Maselle, akisoma taarifa kwa mgeni rasmi, alisema serikali kupitia wakala huo, inaendelea na ujenzi wa vivuko vingine vipya kwa ajili ya Mafia-Nyamisati kwa gharama ya Sh. bilioni 5.3, Bugorola Ukara kwa gharama ya Sh. bilioni 4.2 na Chato-Nkome kwa Sh. bilioni 3.1.

"Vivuko hivi vyote vinagharimu jumla ya Sh. bilioni 15.3 na fedha zote hizi zinatolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," Maselle alisema na kuishukuru serikali ya Rais Magufuli kwa kutoa fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya ununuzi wa vivuko, ukarabati na ujenzi wa maegesho ya vivuko.

Mbunge wa Ilemela ambaye ni Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, aliishukuru serikali kwa kutimiza ahadi iliyoitoa.

"Nimshukuru Mheshimiwa Rais, niwashukuru Temesa kwa kazi kubwa na nzuri ambayo imefanyika, tunao uhakika sasa kwamba shida ya usafiri katika eneo la visiwa vya Kayenze na Bezi itakua ni historia," alisifu.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, alimwomba Nditiye kufikisha salamu za shukrani zao kwa Rais kwa mambo makubwa anayoufanyia Mkoa wa Mwanza, hasa kwenye sekta ya usafiri wa majini, akieleza kuwa wakazi wa mkoa huo wanategemea mwezi ujao kuona vivuko vingine vikiingia ziwani, tayari kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

Kivuko cha MV. Ilemela kina uwezo wa kubeba abiria 200 na magari 10, sawa na tani 100. Hadi sasa, wakala unaendesha na kusimamia vivuko 30 katika vituo 20 Tanzania Bara na hivyo kukamilika kwa kivuko cha MV. Ilemela kutafanya idadi ya vivuko kufikia 31 na vituo kuwa 21.

## Wachimbaji 280 wapewa leseni

**Na Jaliwason Jasson, BABATI**

MKOA wa Manyara umetajwa kuwa na leseni 284 za uchimbaji madini na wachimbaji wadogo 500 ambao ndio wamejiajiri katika sekta ya madini.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na Kaimu Ofisa Madini wa Mkoa wa Manyara, Mhandisi Godfrey Nyanda, wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake.

Mhandisi Nyanda alisema leseni hizo na wachimbaji hao ni kwa wilaya za Babati, Mbulu, Hanan'g na Kiteto ambazo anazisimamia huku akiitaja Wilaya ya Simanjiro kujitegemea kama mkoa wa kimadini.

Alisema toka ofisi ya madini ianzishwe mjini Babati Januari, mwaka jana, wameishatoa leseni za wachimbaji wadogo 60, hivyo kufikia jumla ya leseni 284.

Pia alisema leseni 16 wameshazifuta wilayani Mbulu na kuwapatia wachimbaji wengine ambao wana uwezo wa kufanya uzalishaji.

"Hizo leseni tumezifuta kutokana na kuwa na leseni bila kufanya kazi ni kuiingizia serikali hasara, hivyo ni bora wakapewa watu wenye uwezo wa kufanya kazi," alisema Mhandisi Nyanda.

Mtaalamu huyo wa madini alisema idadi iliyopo ya wachimbaji kwa uwiano wao Hanang' 150, Mbulu 200, Kiteto 100 na Babati 50.

Alifafanua kuwa kwa sasa mkoa umeanza kuamka kwenye sekta ya madini na akasema mwitikio wa wadau ni mkubwa na waombaji wa maeneo ya uchimbaji yameongezeka.

Nyanda aliongeza kuwa wanatoa leseni za uchimbaji kwa wachimbaji wadogo tu na kwamba mtu akihitaji leseni za wachimbaji wakubwa anapaswa kwenda makao makuu ambako ndiko zitatolewa.

Mmoja wa wachimbaji ambaye hakutaka kuandikwa majina, aliishauri serikali kutokuwa na haraka ya kuwafutia leseni wamiliki wa leseni pengine wamepata matatizo na wanajipanga.

Mkazi wa Babati, Domina Pius, alisema watu wengine kufutiwa leseni ni sahihi kwa kuwa ni wadanganyifu kila mara wao ni kulia hasara kumbe wanapata faida.

**"Hizo leseni tumezifuta kutokana na kuwa na leseni bila kufanya kazi ni kuiingizia serikali hasara, hivyo ni bora wakapewa watu wenye uwezo wa kufanya kazi," alisema Mhandisi Nyanda.**

HABARI KITAIFA

# Gulio bidhaa zilizotumika laanza Dar

**Na Elizabeth Zaya**

GULIO la kuuza bidhaa zilizotumika limeanzishwa jijini Dar es Salaam, huku wananchi wakiombwa kuchangamkia fursa hiyo kuuza bidhaa ambazo hawazitumii.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Kampuni ya Masoko ya Gateway Buy and Sell, Rehema Moses, gulio hilo litakuwa linatumika kuuza bidhaa zilizotumika kila baada ya miezi mitatu.

Alitaja baadhi ya bidhaa zitakazokuwa zinauzwa katika gulio hilo ni pamoja na nguo, viatu, mashuka na vitu vya ndani vilivyotumika.

Kwa mujibu wa Moses, gulio hilo limeanza na litafanyika kwa mara nyingine Machi mwaka huu na kuwataka wajasiriamali kujitokeza kuchangamkia fursa hiyo.

Alisema dhumuni la gulio hilo limelenga kuwasaidia wananchi kuuza bidhaa walizozichoka ambazo zimekuwa mzigo katika nyumba zao.

"Wapo watu ambao nyumbani kwao kuna bidhaa ambazo hawazitumii lakini bado zinafaa kutumika na watu wengine, hivyo badala ya kuziacha kuendelea kuwapo ndani ya nyumba tukaamua kuanzisha gulio ambalo litasaidia na wengine kufaidika hata kama wana kipato kidogo," alisema Moses.

"Kwa mfano wapo kinamama ambao wamenunua begi nyingi za mkononi na hawazitumii, gurio hili litafanya kazi hiyo, badala ya kuziacha ziharibike ndani, watauza kwa wengine na bidhaa nyingine zinazofanana na hizo."

"Tumeamua kuanzisha gulio hili baada ya kufanya uchunguzi na kubaini kwamba kuna bidhaa ambazo zinaharibika kutokana na watu kutozitumia, wakati bado zinahitajika kuwasaidia wengine," alisema.

Kwa upande wake, mmoja kati ya waliojitokeza kwenye gulio la kwanza kuuza bidhaa zao, Farssy Kassim, alipongeza kuanzishwa kwake na kwamba amelitumia kuuza bidhaa mbalimbali ambazo alikuwa hazitumii.

"Magulio kama haya yamekuwa yakifanyika zaidi nchi za Ulaya na Amerika na yana faida kubwa kwa maana hakuna bidhaa zinazotupwa, pia inawasaidia wale wasio na kitu kupata kitu kwa gharama ndogo tena zina ubora."

**"Tumeamua kuanzisha gulio hili baada ya kufanya uchunguzi na kubaini kwamba kuna bidhaa ambazo zinaharibika kutokana na watu kutozitumia, wakati bado zinahitajika kuwasaidia wengine," alisema.**

# Ndalichako aahidi utoaji elimu bora

**Na Neema Hussein, KATAVI**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, amezindua tawi la Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) mkoani Katavi, na kusema kuwa serikali itaendelea kuhakikisha inasimamia utoaji elimu bora.

Majengo ya chuo hicho yako Kata ya Kibaoni Halmashauri ya Mpimbwe wilayani Mlele mkoani Katavi.

Amesema utoaji wa elimu bora utasaidia kuboresha kilimo ndani ya mkoa wa Katavi na mikoa jirani.

Ndalichako alizindua chuo hicho juzi baada ya makabidhiano ya majengo kati ya Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda ambaye ni mwanzilishi na msimamizi wa ukamilishwaji wa majengo hayo kwenda kwa Mkuu wa SUA, Jaji Joseph Warioba, kwa ajili ya kuanza mafunzo na kuwa tawi la SUA.

"Nimefurahi sana kuhudhuria tukio hili la kihistoria ambalo limefanyika leo na pia nampongeza sana baba yangu mheshimiwa Pinda kwa kujitoa na kuamua kutoa majengo haya kwa ajili ya kuanzisha chuo kikuu cha kilimo na tutashirikiana kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu bora hapa," alisema Ndalichako.

Jaji Warioba alimpongeza Pinda akisema pamoja na kustaafu, lakini anaendelea kulitumikia taifa, na kwamba kwa heshima wao kama uongozi wa chuo hicho wameridhia kukipa jina la Kampasi ya Mizengo Pinda kutokana na jitihada alizofanya hadi chuo hicho kukamilika.

Hata hivyo, Pinda alisema hakufanikisha kazi hiyo peke yake bali mwanzo wazo lilikuwa ni kuanzisha shule ya msingi, lakini kwa kushauriana na wadau mbalimbali na kuona uhitaji wa watumishi wa masuala ya kilimo pamoja na kuwasaidia wakulima, hivyo wazo hilo lilibadilika na kuamua kuanzisha chuo cha kilimo.

"Ni historia ndefu sana japo mwanzo majengo haya nilijenga kwa ajili ya kuanzisha shule ya msingi, kikubwa tu naushukuru ubalozi wa China pamoja na ubalozi wa Japan, nilipowaeleza suala hili hawakusita kunipa msaada na kuanza kazi hii," alisema na kuongeza:

"Lakini pia tazishukuru taasisi zingine na wananchi kwa ujumla, tumeshirikiana pamoja, naishukuru serikali ya kijiji kunipa eneo hili la hekari 263."

Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, alisema chuo hicho kitakuwa na manufaa kwa Tanzania nzima. Pia alimshauri Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera, kuendelea kuwekeza kwenye kilimo, na kwamba serikali ina matumaini chuo hicho kitazalisha wataalamu wengi wa kilimo.



Barabara ya Kimara Bonyokwa, ikiwa imeharibika kutokana na mvua kubwa zilizonyesha jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Watumishi Mambo ya Ndani wasisitizwa uwajibikaji 2020

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Meja Jenerali Jacob Kingu, amewataka watumishi wa wizara yake kufanya kazi kwa kujituma na kutimiza wajibu wao.

Aidha, amewapa angalizo watumishi hao akisema mwaka 2020 ni wa kufanyakazi na sio ujanja ujanja, huku akihimiza kuwapo ushirikiano.

Meja Jenerali Kingu aliyazungumza hayo katika kikao na watumishi wa wizara hiyo, kilichofanyika jana jijini Dodoma, ambacho kililenga kutoa salamu za mwaka mpya wa 2020 na kuwataka kuendelea kufanya kazi kwa kasi ndani ya mwaka huu.

"Lengo la kikao hiki ni kupeana salamu za mwaka mpya, na pia tunapaswa kumshukuru Mungu kwa kutufikisha mwaka huu salama, wengi hawakufika lakini mimi na wewe tumefika, hivyo tuendelee kufanya kazi kwa upendo," alisema Kingu.

Aliongeza kuwa mwaka 2020 ni mwaka wa kazi na ushirikiano, licha ya kuendelea kufanya majukumu yao, lakini watumishi wawe wazi katika masuala yote ya kazi ili kuleta ufanisi na mafanikio ndani ya wizara hiyo.

"Mwaka huu tunapaswa tubadilike zaidi, tufanye kazi, kila mtu awajibike kutokana na kazi anazozifanya, Mungu atupe uzima na afya, tuwe na umoja, upendo katika kutekeleza wajibu wetu kisawasawa, na atakayefanya kazi atapewa haki yake na siyo kuishi kiujanjaujanja," alisema Kingu.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Emmanuel Kayuni, alimshukuru Katibu Mkuu kwa kikao hicho, na kuwataka watumishi kufuata maagizo yake na pia kuendelea kufanya kazi kwa umoja na kutii sheria za kazi.

# Pwani waelezwa mbinu ya maendeleo

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, ametoa wito kwa watumishi mkoani Pwani, kila mmoja kutimiza wajibu wake kwa nafasi anayoitumikia kwa lengo la kuuletea maendeleo mkoa.

Ndikilo alitoa wito huo Mjini Kibaha alipokuwa akizungumza na wadau wa kamati ya ushauri, pamoja na watumishi mbalimbali wa mkoa huo, wakiwamo wakuu wa wilaya na wakurugenzi.

Ndikilo alisema, watumishi wanatakiwa kushikamana kwenye halmashauri kwa kila mmoja kutimiza wajibu wake, kuondoa changamoto kwa wananchi ambazo zinakuwa kikwazo cha maendeleo.

"Kila mmoja asimame katika nafasi yake, tufanye kazi tuwatumikie wananchi kwa uadilifu tushikamane kuondoa changamoto kwa wananchi, tukifanya hivyo mkoa wetu utakuwa na maendeleo," alisisitiza.

Aliwataka wakurugenzi ambao katika maeneo yao kuna ujenzi wa vituo vya afya na hospitali, kuhakikisha miradi hiyo inakamilika kwa muda uliopangwa ili huduma zianze kutolewa.

Aidha, Ndikilo aliwataka watumishi kusoma alama za nyakati, kufanya kazi zao kwa kufuata maadili kuepuka mambo ambayo yanaweza kuwasababishia matatizo kazini.

Ndikilo alisema mtumishi wa umma anatakiwa kuwa mwadilifu, kufanya kazi zake kwa kufuata taratibu na sheria za kazi na kwa kufanya hivyo mipango ya utekelezaji kazi itafanyika kwa wakati na maendeleo yatapatikana bila kikwazo.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Arusha, Zelothe Stephen (kushoto), akisajili laini yake ya simu kwa alama za vidole katika Banda la TTCL, ndani ya Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

## Ujenzi kituo cha afya wapigwa jeki

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

MBUNGE wa Shinyanga Mjini, Stephen Masele, ameahidi kuendelea kusaidia ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Ndembezi pamoja na Zahanati ya Ngokolo ili kuboresha huduma za afya.

Masele alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na wajumbe wa kamati ya siasa CCM ngazi ya matawi Kata ya Ndembezi na Ngokolo.

Alisema ataendelea kushirikiana na wananchi pamoja na serikali kuchangia shughuli za maendeleo, ambapo kwenye ujenzi wa zahanati hiyo awali alishachangia Sh. milioni tano, na sasa ameahidi kutoa tena kiasi cha shilingi milioni sita.

Aidha, katika ujenzi wa zahanati ya Ngokolo, aliahidi kuchangia shilingi milioni mbili ili kununua mifuko ya saruji 100, hivyo kuanza hatua ya msingi, na baada ya hapo ataendelea kuchangia zaidi hadi pale ujenzi utakapokamilika, huku akiwasihi pia wananchi waendelee kuchangia shughuli za maendeleo.

"Mimi mbunge wenu nitaendelea kushirikiana na wananchi pamoja na serikali, kuchangia shughuli mbalimbali za maendeleo hususan katika sekta ya afya, miundombinu ya barabara, maji, pamoja na umeme ili kuubadilisha mji wetu kimaendeleo," aliongeza Masele.

Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Ndembezi, Manispaa ya Shinyanga, David Nkulila, alisema ujenzi wa kituo hicho cha afya ulianza Machi mwaka jana, na mpaka sasa wameshapandisha boma la ujenzi wa huduma la wagonjwa wa nje (OPD), ambalo hadi kufikia Septemba mwaka huu litakuwa limekamilika.

# Wadau watoa neno vita ya udhalilishaji

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

JAMII imetakiwa kushirikiana na vyombo vya sheria pamoja na wadau katika kuhakikisha wanadhibiti vitendo vya ukatili na udhalilishaji vinavyofanywa dhidi ya wanawake na watoto.

Wakizungumza katika mkutano wa kamati na mtandao wa kupinga vitendo vya udhalilishaji na ukatili wa wanawake na watoto, ulioandaliwa na Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA-Pemba) ambao uliofanyika Gombani Chakechake, washiriki walieleza kuwa bado jamii haijawa tayari kupiga vita vitendo vya udhalilishaji.

Walisema kunakosekana uadilifu kwa jamii na baadhi ya watendaji, jambo ambalo linasababisha vitendo vya udhalilishaji kuongezeka siku hadi siku, hivyo ipo haja ya kushirikiana pamoja katika kuhakikisha wanadhibiti.

Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Chakechake, Adam Abdalla, alisema kuna baadhi ya wazazi hurejesha nyuma juhudi za kupambana na udhalilishaji kwa kuwaoza waume watoto wao ambao tayari wameshafanyiwa vitendo vya ubakaji.

"Hii inarudisha nyuma, kesi zinaletwa mahakamani, lakini mwisho unasikia mtoto ameolewa na mtuhumiwa, hivyo hawawezi tena kutoa ushahidi unaofaa na wengine hawapiti tena mahakamani kabisa," alisema Hakimu huyo.

Alieleza, pia ipo haja ya kuangaliwa upya sheria ya mtoto, kwani inawalinda wanapofanya makosa hasa watoto wenye umri mkubwa kati ya miaka 15 hadi 17 wanapowafanyia udhalilishaji watoto wadogo sana.

Naye Wakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Chakechake, Mohamed Ali Juma, alieleza kuwa wazazi wamekuwa na tabia ya kupeleka barua za maombi ya kufutisha kesi za udhalilishaji katika ofisi yao, jambo ambalo linawahuzunisha kwani baada ya hapo wanavuruga ushahidi, ili mtuhumiwa asiweze kutiwa hatiani.

"Sisi barua hatujibu lakini wakishazileta tu wanakimbia wenyewe na hata ukilazimisha lazima wanaharibu ushahidi, jambo ambalo inasababisha mtuhumiwa kuachiwa huru, maana hakuna hatia bila ya ushahidi," alifahamisha.

Nassor Said Amour kutoka kituo cha Mkono kwa Mkono Wilaya ya Micheweni, alisema filamu wanazoangalia watoto sio rafiki kwao, kwani zina mambo ya mapenzi ndani yake, hivyo huiga.

Salma Khamis Haji kutoka Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto, aliliomba Jeshi la Polisi kuharakisha upelelezi wa kesi hizo, ili haki iweze kupatikana.

Mkuu wa dawati la Jinsia la Wanawake na Watoto Mkoa wa Kaskazini Pemba, Fakih Mohamed Yussuf, alieleza kuwa kufuatia hali iliyopo sasa ya watoto kwenda kuokota karafuu, Jeshi la Polisi litaandaa operesheni maalum, ili kuondosha hali hiyo ambayo inasababisha kwa kiasi kikubwa watoto kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji.

Ofisa Wanawake na Watoto Wilaya ya Micheweni, Bizume Haji Zume, aliwataka kinababa kuwajibika ipasavyo katika malezi na kuacha tabia ya kuwaachia kinamama peke yao.

Naye mshiriki Hadia Sultan kutoka ZAPHA+ Pemba, alisema vyombo vya sheria havitendi haki ipasavyo, hivyo vibadilike, vitende haki na wasiwaachie wahalifu.

Akifungua mkutano huo, Ofisa Mdhamini Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Hakim Vuai Shein, alisema suala la udhalilishaji linamgusa kila mtu, hivyo kila mmoja ana haki na wajibu wa kulipiga vita na kuelimisha ili kuhakikisha linaondoka.

Mratibu wa TAMWA Pemba, Fat-hiya Mussa Said, alitaja baadhi ya changamoto zinazorudisha nyuma juhudi za wananchi kuwa ni pamoja na kuambiwa wakamtafute mhalifu na kisha wampeleke polisi, jambo ambalo sio rahisi kwao.

"Pamoja na kuwa baadhi ya wananchi hawataki kutoa ushahidi, lakini na hao waliopo tayari wanalalamika kuwa wanapokwenda kushtaki wanaambiwa wakamchukue mtuhumiwa, hii inarudisha nyuma," alisema.

# Vijana kunufaika mtandao wa uvuvi

**Na Mwandishi Wetu**

VIJANA kutoka mikoa 13 ya Tanzania Bara na Visiwani watanufaika na mtandao wa vijana unaojihusisha na shughuli za uvuvi na mifugo.

Lengo la kuanzishwa kwa mtandao huo kutawasaidia vijana nchini, kujiajiri moja kwa moja kupitia mtandao huo wa uvuvi na mifugo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mtandao huo, uliofanyika jijini Arusha, Rais wa Mtandao huo, Laban Boaz, alisema vijana chini ya miaka 35, kutoka mikoa hiyo, watanufaika na mtandao huo kwa kufundishwa mbinu bora za kisasa za ufugaji.

Alisema lengo la kuanzishwa kwa mtandao huo, ni kuhamasisha vijana nchini, kujiajiri katika sekta ya mifugo na uvuvi kwa kutumia njia ya kisasa ambazo zitasaidia kuongeza uzalishaji mali na ajira kwa vijana.

Alisema walianzisha mtandao huo, baada ya kuona kuna mwanya wa kimaendeleo kati ya wazee na vijana.

"Mtandao huu utasaidia kuwapa ujuzi na maarifa vijana namna ya kufuga kisasa na vijana waliopo vijijini ambao hawakupata maarifa haya lengo la mtandao huu ni kuwanufaisha vijana wote," alisema Laban. Alisema mtandao huo, ulianzishwa jijini Dar es Salaam mwaka 2017, lengo likiwa ni kupanua wigo kwa vijana nchini.

Mkurugenzi wa Uzalishaji na Masoko Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Felix Nandonde, alisema mtandao huo ni juhudi za muda mrefu zilizofanywa na Umoja wa Afrika kupitia mradi wa kuendeleza rasilimali za wanyama (AU-IBAR).

Alisema mtandao huo, umewashirikisha vijana wanaojihusisha na kazi tofauti katika mnyororo wa thamani ya mifugo, samaki, kuku na nguruwe na vijana hao, kupitia mtandao huo watawekwa pamoja na kufanya kazi ya mnyororo wa thamani.

Nandonde alisema serikali itaendelea kushirikiana na mtandao huo, kuwafikia vijana ili waitumie fursa hiyo ipasavyo.

Makamu wa Rais wa Mtandao huo, Veronica Lyambiko, alisema wamefikia hatua ya kuanzisha mtandao huo, kwa kuwa vijana wengi nchini wanakabiliwa na tatizo la ajira.

Alisema, kupitia mtandao huo, idadi ya vijana wataingia na kuwafikia vijana waliopo vijijini.



Umati wa wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru, mkoani Arusha, wakiwa kwenye foleni kwa ajili ya kuandikisha ili kupata vitambulisho vya Taifa, katika makao makuu ya ofisi za Nida, wilayani humo jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Wazee, wenye mahitaji maalumu wakatiwa bima

**Na Allan Isack, ARUSHA**

WATOTO wenye mahitaji maalumu kutoka katika vituo mbalimbali vya kulelea watoto yatima, jijini Arusha, wamekabidhiwa kadi za afya 20 (Bima), kwa lengo la kuwarahisishia upatikanaji wa huduma za afya bila malipo.

Akizungumza wakati wa kukabidhi kadi hizo, msemaji wa kundi la Friends of Batuli, Batuli Kisaya, alisema wamegawa kadi hizo, kwa ajili wa kuboresha mazingira ya upatikanaji wa huduma za afya kwa watoto wenye mahitaji mbalimbali.

Alisema kadi hizo, wamezitoa kwa watoto yatima, wenye ulemavu na waliotoka katika mazingira magumu kutoka kwenye vituo mbalimbali vya kulelea watoto wenye mahitaji maalumu jijini Arusha.

Alisema kundi hilo walichangisha fedha hadi kufikia kiasi cha Sh. milioni moja ambazo walizitumia kukata kadi za matibabu za watoto hao.

"Kupitia kikundi chetu tulichangishana na kupata fedha kiasi cha Sh. milioni moja na fedha hizo tumezitumika kukata kadi za watoto wenye mahitaji maalumu hivyo, tunaomba jamii kujitolea kusaidia makundi haya bila kukata tamaa," alisema Batuli.

Hata hivyo, alisema licha ya kutoa kadi kwa watoto hao, pia wametoa msaada wa vyakula, mahindi gunia moja, mafuta ndoo ndogo ya kupikia, katoni moja ya sabuni ya kufuli na maji ya kunywa katoni tatu kwa wazee saba kutoka katika kituo cha Herototo kilichopo Kata ya Moshono, jijini hapa.

Mgeni rasmi katika shughuli hiyo, alikuwa mfanyabiashara maarufu jijini Arusha, Filemon Mollel.

Alitoa rai kwa jamii kuwa mstari wa mbele kuwasaidia watu wanapopatwa na matatizo bila kujali hali zao za kimaisha, dini na kabila.

"Siri ya mafanikio katika maisha ni kuwasaidia watu wenye matatizo na mahitaji maalumu katika jamii, pia sijawahi kuona Mungu akiwaacha bure watu ambao ni watoaji wazuri wa sadaka zaidi amekuwa akiwazidishia mara dufu pale watoapo," aliongeza Mollel.

Ofisa Maendeleo ya Jamii katika Jiji la Arusha, Mather George, alisema, Jiji la Arusha kuna wazee 9,307, kati ya hao 3307, wamepewa kadi za afya na huduma za afya wanapata bure katika hospitali, vituo vya afya na zahanati mbalimbali za jijini humo.

Kwa upande wa watoto yatima, wenye ulemavu na wenye mahitaji maalumu alisema wapo 21,000, na wazee wenye ulemavu ni 560, hivyo ameiomba jamii kujitokeza kusaidia makundi hayo kutokana na idadi kubwa ya watoto na wazee wenye mahitaji maalumu.

# Wananchi walalamika kuhamishwa makazi yao

**Na Allan Isack, MANYARA**

BAADHI ya wananchi wanaoishi pembezoni mwa Kituo cha Afya Magugu wilayani Babati mkoani Manyara, wamelalamikia kitendo cha kuamrishwa kuondoka kwenye makazi yao kwa madai kuwa wamevamia eneo la kituo cha afya.

Wakizungumza juzi na Nipashe kwa nyakati tofauti, wakazi hao walisema, kwa sasa wapo katika wakati mgumu baada ya kupewa amri ya kuondoka katika eneo hilo.

Mmoja kati ya wakazi hao, Mariam Hamis, alisema alizaliwa katika eneo hilo miaka 40 iliyopita na hakukuwa na tatizo lolote.

Alisema hivi karibuni waliambiwa kuwa wamevamia katika eneo la kituo cha afya.

Hata hivyo, wameambiwa waondoke bila kulipwa fidia ya makazi yao waliyojenga na wanaishi na familia zao na hawana sehemu nyingine ya kwenda.

"Hatujui hatima yetu itakuwaje kwa kuwa wanataka tuondoke hapa, bila ya kutulipa fidia ili tukaishi sehemu nyingine kwa kuwa hapa tulipo wanadai ni eneo la Kituo cha Afya Magugu," alisema.

Kwa upande wake Richard John, alisema wamesikitishwa na jambo hilo, hawajui mustakabali wa maisha yao, baada ya kuambiwa waondoke kwenye makazi yao.

Alisema wazazi wake walihamia eneo hilo baada ya kutokea ugonjwa wa mifugo na kwa kipindi chote walikuwa wakiishi hapo, hivyo wameshangazwa kuambiwa wamevamia eneo la kituo cha afya.

"Tunaomba serikali itusaidie kwenye jambo hili, watu tumejenga nyumba zetu kuanzia msingi tumezaa watoto wetu miaka mingi iliyopita, tunashangaa leo tunaambiwa tumevamia," alisema John.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, Hamis Malinga, alikiri kuwapo kwa tatizo hilo, kwa baadhi ya wananchi hao kuvamia eneo la kituo cha afya.

Malinga alisema kulipwa fidia au kutokulipwa wananchi hao, bado halijapatiwa ufumbuzi kwa kuwa bado wanafanya tathmini ya namna walivyoingia kwenye eneo hilo la serikali.

**"Tunaomba serikali itusaidie kwenye jambo hili, watu tumejenga nyumba zetu kuanzia msingi tumezaa watoto wetu miaka mingi iliyopita, tunashangaa leo tunaambiwa tumevamia," alisema John.**

## Avunja uongozi kisa soko chafu

**Na Godfrey Mushi, SIHA**

MRUNDIKANO wa uchafu sokoni pamoja na masoko ya walaji ya Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro kukosa uangalizi mzuri 'umemsukuma' Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Ndaki Mhuli, kuamuru kufanyika upya uchaguzi wa viongozi kwa kila soko.

Mhuli alifikia uamuzi huo jana, baada ya kwenda kukagua soko la walaji la Sanya Juu na kuzungumza na baadhi ya wafanyabiashara kuhusu suala la usafi.

"Nyie wafanyabiashara ni lazima mbadilike na kwenda na hali ilivyo. Huwezi kusubiri uchafu ukarundikana kiasi hiki na wala huna mpango wa kuwasisitiza viongozi wako kusimamia usafi ndani ya soko hili, nadhani hapa hamna viongozi wawajibikaji. Nataka leo mnichagulie viongozi wanaoeleweka," aliagiza Mhuli.

Kutokana na hali hiyo, Mhuli aliagiza wahusika wayafanyie usafi masoko yote ya walaji ili kuepuka magonjwa ya mlipuko kujitokeza.

Alisema masoko ya walaji wilayani humo, mengi hayana viongozi hivyo kusababisha kukosa uangalizi wa maana na kusababisha kuwa machafu.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, mwarobaini utakaomaliza matatizo yanayoyakabili masoko ya walaji hivi sasa ni kuchagua viongozi wapya ambao watawajibika kusimamia masoko hayo kwa ukaribu zaidi.

Masoko ya walaji ya Wilaya ya Siha ambayo yana idadi kubwa ya wafanyabiashara ni pamoja na Sanya Juu, Lawate, Karansi na Ngarenairobi.

Baada ya kauli hiyo, wafanyabiashara hao walihamasika na kuamua kuchagua viongozi wapya sita akiwamo Mwenyekiti wa Soko la Sanya Juu, Idrissa Mndeme na Katibu wake, Amedeus Kitali.

Baada ya uchaguzi huo, Mwenyekiti wa soko hilo alitangaza kuwa kila mfanyabiashara atapaswa kuchangia Sh. 300 kwa ajili ya kubeba uchafu huo kwa kila siku ya soko na wafanyabiashara wa maduka wao watachangia Sh. 1,800 kwa mwezi.

# Afukua kaburi na kupanda mgomba

**Na Mwandishi Wetu, MOSHI**

MKAZI wa Kibosho katika Wilaya ya Moshi, anashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Kilimanjaro kwa tuhuma za kufukua kaburi la mtoto mchanga na kuchukua mifupa yake yote na baadaye kupanda mgomba juu ya kaburi.

Taarifa iliyothibitishwa jana na Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Joseph Manyama, inaeleza kuwa mtuhumiwa huyo baada ya kufukua kaburi hilo, anadaiwa kutelekeza sanda iliyokuwa na mwili wa marehemu juu ya kaburi.

Tukio hilo linalohusishwa na imani za kishirikina, limeacha maswali mengi kwa wakazi wa Kibosho, huku taarifa zaidi zikieleza polisi wanasubiri amri ya mahakama kwenda kufukua kaburi hilo ili kujiridhisha.

"Ni kweli tukio hilo lipo na limetokea maeneo ya Kibosho. Kuna kijana anadaiwa kufukua kaburi na kupanda mgomba. Baada ya tukio hilo kutokea, taarifa ilifikishwa Kituo cha Polisi Moshi na polisi walikwenda kukagua eneo la tukio na kumkamata mtuhumiwa.

"Polisi waliokwenda katika eneo la tukio hilo, wamekuta sanda iko juu ya kaburi kwa maana juu ya shimo na sehemu hiyo kulikuwa kumepandwa mgomba. Tayari tumemkamata mtuhumiwa na tunaendelea kumhoji ili kujua kiini cha kufanya ukatili huo," alisema Manyama.

Akizungumzia tukio hilo, Juliana Kullaya ambaye ni mama mzazi wa marehemu, alisema Januari Mosi, mwaka huu, majira ya saa 12:30 jioni, alisikia kishindo kama mtu analima shambani na yeye na nduguze walidhani mtuhumiwa anayetajwa kwa jina la Devenja, labda anaziba njia ili watu wasipite shambani kwenda nyumbani kwa bibi yao mdogo.

"Nimefika kwenye kaburi nimethibitisha sanda niliyomzika nayo mwanangu iko juu ya kaburi, mifupa haionekani na (mtuhumiwa) ameotesha mgomba kwenye kaburi. Kitendo alichokifanya ni kitendo cha uuaji, ni sawa ameua.

"Kwa kweli naweza kulihusisha na imani za kishirikina kwa sababu baada ya kumbana na kumuuliza mifupa iko wapi hakutaka kusema. Kiukweli mimi binafsi imeniumiza sana," alisema Kullaya.

Mkazi mwingine wa Kibosho, Joseph Kullaya, alisema wanaamini huenda tukio hilo likawa na chembechembe za imani za kishirikina kwa sababu hakuna ugomvi wowote katika familia.



Wataalamu na watafiti wa kilimo cha mpunga kutoka Chuo cha Kilimo Kilimanjaro (KATC) na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Ifakara (Tari), wakitoa elimu ya matumizi bora ya pembejeo ya kilimo cha mpunga katika Skimu ya Mpunga ya Kivulini, Wilaya ya Mwanga, mkoani Kilimanjaro, jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Abiria treni Dar-Moshi kukata tiketi siku 3 kabla

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

IDADI kubwa ya abiria wanaohaha kupata usafiri wa treni ya De Lux kati ya Moshi na Dar es Salaam, wamelilazimisha Shirika la Reli Tanzania (TRC) kutoa angalizo kwa abiria wake kukata tiketi siku tatu kabla ili kupata nafasi.

Mji wa Moshi ulioko mkoani Kilimanjaro, unapokea idadi kubwa ya wasafiri wa treni hivi sasa kutoka mikoa ya Arusha na Manyara, huku wengi wao wakiwa wafanyabiashara wadogo wanaokwenda kufungasha mizigo Dar es Salaam.

Jana, Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano wa TRC, Jamila Mbarouk, akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu alisema: "Ushauri kwa abiria wetu kwa sasa wanapofika stesheni huwa tunawaeleza kwamba wanapaswa kukata tiketi siku tatu kabla ili mtu apate uhakika wa kusafiri na sisi kwa sababu abiria wanaotoka mikoa ya kanda ya kaskazini ni wengi."

Moshi imekumbwa na mahitaji hayo makubwa ya usafiri baada ya mabasi yaendayo mikoani kuzidiwa na wingi wa abiria wakiwamo wanafunzi wanaorejea shuleni kukodi mabasi hayo.

Treni hiyo ya abiria iliyokuwa imesitishwa kutoa huduma kati ya Dar es Salaam na Moshi, ilianza tena safari zake Desemba 6, mwaka jana.

Wakati abiria wanaosafiri kutoka Moshi kwenda Dar es Salaam wakitumia saa 10 hadi 11 njiani kufika kwa usafiri wa basi, kwa usafiri wa treni wanatumia saa 16.

Kwa mujibu wa ratiba ya TRC, kutoka Dar es Salaam kwenda Moshi ni siku ya Jumanne na Ijumaa saa 10 jioni na huwasili Moshi saa 2:00 asubuhi wakati kutoka Moshi kwenda Dar es Salaam ni Jumatano na Jumamosi saa 10 jioni na kuwasili Dar es Salaam saa 2:00 asubuhi.

Abiria wanaotumia mabasi, kuanzia juzi idadi kubwa ya abiria katika kituo kikuu cha mabasi cha Moshi Mjini waliokuwa wakienda Dar es Salaam, Tanga, Morogoro, Arusha na mikoa ya Kanda ya Ziwa, walikwama kwa saa kadhaa kusafiri kutokana na mabasi kukodiwa na baadhi ya shule kwa ajili ya kubebea wanafunzi, hivyo kusababisha wengi wao kusota kwa muda mrefu kituoni.

Baadhi ya abiria waliozungumza na Nipashe kuhusu hali ya usafiri, walisema sababu hiyo ndiyo inayochangia kuwapo kwa uhaba wa mabasi yaendayo mikoani.

Nipashe
# TESA
Jumanne Januari 7, 2020
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 15

## Waliofuata shule kilomita 5 sasa kupumua kwa shule mpya kijijini



## Hii ndio haki na gharama zake

Ukurasa 17



Ukurasa 19

## Mhitimu uhandisi 'anayepiga kiwi' sasa ajutia safari ya shule



SHIDA YAANZIA UKUNGA...

# Mtoto mwenye ulemavu alia kusoma na kuandika, juhudi zaishia hewani

Ukurasa 16

ELIMU YA KIPOLISI

# Huu hapa umuhimu wa kumlinda mtoto




Mrakibu wa Polisi, Faidha Suleman, kutoka Dawati la Jinsia na Watoto, alipowasilisha mada katika mafunzo ya kuwajengea uwezo Mkamanda wa Polisi wa Mikoa ya Tanzania kuhusu makosa ya ukatili wa kijinsia. **Chini**, uchangiaji mkutanoni ukiendelea. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

JESHI la Polisi ni chombo kilichopewa mamlaka ya kusimamia mustakabali wa haki, ulinzi na usalama wa watu na raia.

Kuwapo ulinzi una sura pana, lakini sura kuu iko jamii iliko. Ni siku chache tu tulisikia mkoani Rukwa katika kijiji cha Mtakuja, mtu anayedaiwa kuwa ana matatizo ya akili alimuua mtoto mdogo wa mikaa mitatu. Imestua na kugusa nafsi za wengi kwa huzuni.

Lakini hili suala la ulinzi linaanzia umma uliko na Polisi ni wasimamizi waratibu, waelimishaji na wasaidizi wa umma unapobidi. Ndio maana wanasisitiza; 'Tii Sheria, Bila shuruti.'

Kimsingi, watoto wote wana haki ya kulindwa. Kila mtoto ana haki ya kuishi, anahitaji kuwa salama na wazazi au walezi, kusikilizwa, kupata huduma muhimu na kuwa katika mazingira salama.

Familia ndicho chanzo cha ulinzi wa mtoto. Wazazi au walezi wengine wana jukumu la msingi la kutengeneza mazingira ya nyumbani ambayo ni salama na yenye upendo.

Shule na jamii ina jukumu la kutengeneza mazingira ya nje ya nyumbani ambayo ni salama na rafiki kwa mtoto.

Kwa bahati mbaya mamilioni ya watoto hawana ulinzi. Kila siku duniani kuna kilio cha watoto wanaokabiliwa na ukatili, unyanyasaji, utelekezaji, unyonyaji, kutengwaji na ubaguzi.

Aina hizo za ukiukwaji wa haki za watoto hupunguza uwezekano wao wa kuishi, kukua vizuri na kufikia ndoto zao.

Duniani kunatajwa kuwapo zaidi ya watoto milioni 160 wanaotumikishwa badala ya kufurahia utoto na inakadiriwa kwamba zaidi ya watoto milioni 160 wa umri wa miaka mitano na minne wanatumikishwa katika ajira za watoto.

Mamilioni ya watoto, hususan wasichana wanafanya kazi za nyumbani kwa watu binafsi na zaidi ya watoto milioni moja husafirishwa kila mwaka.

Ulinzi ni nini? Inahimizwa wasichana na wavulana wahimizwe na wasaidiwe ili wazungumze kuhusu utetezi wa haki za watoto.

Vijana nao hawana budi kuwa mstari wa mbele katika ulinzi wao wenyewe dhidi ya unyanyasaji, ukatili, unyonyaji na ubaguzi.




JIELIMISHE

# Ilivyo haki ya kijana na ustawi wa familia

KIJAMII inaelezwa, vijana wanapaswa kuwa mstari wa mbele katika ulinzi wao wenyewe dhidi ya unyanyasaji, ukatili, unyonyaji na ubaguzi kwa hatua zifuatazo zinazowaangalia wadogo zao ambao ni watoto.

• Kila mtoto ana haki ya kukulia katika familia. Endapo familia haina uwezo wa kumhudumia mtoto, mamlaka katika jamii husika ichukue hatua ya kujua sababu za hali hiyo na yafanye kila juhudi ili kuiwezesha familia husika iendelee kuwa pamoja.

• Kila mtoto ana haki ya kuwa na jina. Kila mtoto ana haki ya kuwa na utaifa. Kusajili uzazi wa mtoto husaidia kumhakikishia haki yake ya kupata elimu, huduma za afya pamoja na huduma za kisheria na za kijamii.

Duniani kote, uzazi wa takribani watoto milioni 230 wa umri wa chini ya miaka mitano haukusajiliwa mahali popote. Kusajili uzazi wa mtoto ni hatua muhimu katika kumlinda mtoto dhidi ya unyanyasaji na unyonyaji.

• Wasichana na wavulana hawana budi kulindwa dhidi ya aina zote za ukatili na unyanyasaji. Ukatili ni pamoja na unyanyasaji wa kimwili, kingono na kihisia, utelekezwaji na kutendewa matendo hatarishi kama vile ndoa za utotoni na ukeketaji. Familia, jamii na mamlaka ni lazima ziwajibike katika ulinzi dhidi ya ukatili huo.

• Watoto walindwe dhidi ya aina yoyote ya kazi za hatari. Kazi zisiwanyime watoto kwenda shule. Watoto wasitumikishwe kabisa kwenye ajira mbaya kama vila utumwani, kazi za kushurutishwa, uzalishaji na uuzaji wa dawa za kulevya.

• Wasichana na wavulana wanaweza kufanyiwa unyanyasaji na unyonyaji wa kingono katika maeneo ya nyumbani, shuleni, kazini au ndani ya jamii.

Ni lazima hatua zichukuliwe kuzuia unyanyasaji na unyonyaji wa kingono. Watoto waliofanyiwa vitendo vya unyanyasaji na unyonyaji wa kingono wanahitaji msaada wa haraka wa kuwawezesha kuondokana na hali hiyo.

• Watoto wanaweza kuwa katika hatari ya kuingizwa kwenye biashara ya kusafirisha watoto endapo watakosa ulinzi au watakuwa na ulinzi mdogo. Serikali, vyama vya kiraia na familia zina jukumu la kuzuia au kutokemeza biashara ya kusafirisha watoto na zina jukumu la kusaidia watoto waliokumbwa na biashara ya hiyo kurejea kwenye familia na jamii zao, kwa manufaa ya watoto husika.

• Utekelezaji wa masuala ya kisheria kwa watoto uzingatie haki za mtoto. Kifungo au kuwekwa rumande kwa wtoto kufanyike tu kama ni lazima sana. Taratibu zinazozingatia watoto zitumike kwa watoto waliotenda makosa ya kisheria au wanaotoa ushahidi.

• Huduma za msaada wa kipato na za ustawi wa jamii zinaweza kusaidia katika kuleta utangamano kwa kifamilia, watoto shuleni na katika kupatikana kwa huduma za afya.

• Watoto wote wana haki ya kupata habari zinazoendana na umri wao, kusikilizwa na kushirikishwa katika kufikia maamuzi yanayowahusu.

Kutekelezwa kwa haki hii huwezesha watoto kushiriki kikamilifu katika masuala ya ulinzi wao dhidi ya unyanyasaji, ukatili na unyonyaji, pamoja na kuwa raia wenye kujali wajibu.



Watoto wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DCR) wakifurahia siku yao kimataifa. **PICHA: MTANDAO**

ELIMU

NA MARCO MADUHU, MSALALA

# Waliofuata shule km 5 sasa kupumua shule mpya kijijini

• Mabinti wasimulia hatari zao • Uongozi, wanakijiji wanena yao

ELIMU ni mwanga wa jamii katika maisha ya binadamu nchini, ambayo inampatia upeo namna ya kufikiri juu ya kuendesha maisha yake. Hiyo ni mbali na kuajiriwa au kujiari, elimu ikiwa na nafasi kwa asilimia kubwa.

Ni miaka zaidi ya minne, serikali iliyoko madarakani ilitangaza elimu bure kwa wanafunzi kuanzia awali hadi kidato cha nne, ikiwa ni moja ya ahadi zilizotolewa kwenye kampeni za uchaguzi mkuu mwaka 2015.

Utekelezaji wa ahadi hiyo umesababisha idadi kubwa ya wazazi kuitikia wito hasa kwa maeneo ya vijijini, ambako baadhi hawakupeleka shule watoto kwa sababu za kiuchumi na kuamua kuwaingiza kwenye shughuli za kilimo huku watoto wa kike wakiolewa ndoa za utotoni.



Aliyekuwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Igundu, Jalema Cherehani, akielezea walivyoanzisha mradi mpya wa shule. **PICHA: MARCO MADUHU.**

**KILICHOKO MSALALA**

Kijiji cha Igundu chenye vitongoji saba katika Kata ya Mwalugulu, ndani ya Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, kinakabiliwa na shida ya ukosefu wa shule.

Sehemu kubwa ya wanafunzi wake wanafuata elimu ya msingi kwenye kijiji jirani cha Mwankima kuanzia kilomita tano hadi 20.

Lulu Abdallah, ni Msaidizi wa Kisheria kutoka Shirika la Paralegal Aid Center (Paceshi) wilayani Kahama, anayesema alipokuwa kwenye shughuli zake kwenye kijiji hicho cha Igundu kutoa elimu ya msaada wa kisheria, alikumbana na changamoto ya ukosefu wa shule, wanafunzi wanaenda umbali mrefu hata kuchelewa kuanza masomo.

Anasema watoto wenye umri kuanzia miaka sita, walipaswa kuanza masomo ya awali, lakini idadi kubwa wanashindwa kuanza masomo na wengine wanatembea umbali mrefu tofauti na umri wao.

"Kijiji hiki cha Igundu ambacho kina vitongoji saba hakina kabisa huduma yoyote ya shule, ambapo wanafunzi wamekuwa wakilazimika kwenda kusoma kwenye kijiji jirani cha Mwankima kuanzia kilomita tano hadi 20 kutokana na umbali wa kitongoji," anasema.

"Siku moja nilihudhulia kwenye kikao cha kijiji, ikabidi nianze kufanya ushawishi kwa wazazi ili wahamasike kuanza kujenga shule ya msingi kijijini hapa, ambayo itaondoa adha ya watoto wao kusoma umbali mrefu na wengine kukatisha masomo na kuishia kwenye shughuli za kilimo na wanafunzi wa kike kuolewa.

"Baada ya kufanya ushawishi huo, mwaka 2015, nilishirikisha pia uongozi wa kijiji pamoja na Jeshi la Jadi Sungusungu, ili kushawishi wazazi waanze kuchanga fedha pamoja na kujitolea nguvu kazi ya kujenga shule hii, ndipo mwaka 2016 ujenzi ukaanza na sasa 2019 tumekamilisha madarasa mawili, huku mawili tukiendelea na ujenzi," anaeleza.

> Kutokana na umbali huo wa shule kwenda kwenye kijiji jirani, anakiri watoto wao wanateseka sana, nahasa kipindi cha mvua ni hatari zaidi.

**MWENYEKITI KIJIJI**

Jalema Cherehani, aliyekuwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Igundu, anasema baada ya kupewa wazo la kujenga shule ya msingi, ilikaa na kamati ya kijiji na kuamua kutenga eneo la ujenzi wa shule hiyo uanze mara moja, huku wakihamasisha wananchi kutoa nguvukazi na kufanikisha ujenzi kukamilika kwa madarasa mawili.

Anasema, kijiji kina kaya 545 waliohamasisha kila mmoja kuchanga Sh.18,000 na kusomba mchanga na mawe na kupeleka kwenye eneo, huku wakilimwangilia kila siku kwa zamu hadi kufikia kwenye 'rinta' ndio serikali ikatoa msaada wa kulimazia.

**MWALIMU MKUU**

Malugu Mbeleng'anyi, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mwankima, iliyopo katika Kata ya Mwalugulu Halmashauri ya Msalala. Hiyo ni shule mama inayohudumia wanafunzi wa kijiji cha Igundu, anayesema shule hiyo inakabiliwa na msongamano wa wanafunzi ambapo wapo 1,444 wakitumia madarasa 14 na walimu 18.

Anasema, msongamano huo wa wanafunzi umelazimisha mwalimu moja kufundisha wanafunzi zaidi ya 200, wakati wastani ni mwalimu kufundisha wanafunzi 45.

"Changamoto hii ya ukosefu wa shule kwenye kijiji jirani, imekuwa ikisababisha msongamano wa wanafunzi shuleni hapa na hata kutofanya vizuri kwenye matokeo ya darasa la saba. Mwaka jana walifanya mtihani wanafunzi 61, na kufaulu 42," anasema Mbeleng'anyi.

"Kuanzishwa kwa shule hiyo ya msingi kwenye kijiji hicho cha Igundu, kutasaidia kupunguza msongamano hapa shuleni na hata wanafunzi kufanya vizuri pamoja na kupunguza utoro sugu na baadhi yao kutokatisha masomo," anasema.

**OFISA ELIMU**

Ofisa Elimu Kata ya Mwalugulu, katika Halmashauri ya Msalala, Adrophina Maswage, anawapongeza wananchi wanakijiji hao kujitoa kujenga shule ya msingi, kwani inaendana na utaratibu uliopo sasa wa kuhamasiha ujenzi wa madarasa mengi ili yafike saba, kuweza kupata usajili kamili.

Anasema, kwa sasa shule itakuwa 'shikizi' ili wanafunzi wa awali na darasa la kwanza wataanza kusoma hapo, na watakapoingia darasa la tatu watakwenda kusoma kwenye shule mama jirani na kijiji hicho cha Mwankima, wakati ujenzi ukiendelea kukamilika taratibu za kuisajili.

"Shule hiyo ya msingi Igundu ambayo imejengwa kwa nguvu na wananchi hivi sasa ina majengo ya madarasa manne. Mawili tayari yameshakamilika na yanafaa kutumiwa kutoa elimu," anasema Maswage.

**MWANAFUNZI**

Mwanafunzi, Margareti Peter, mkazi wa kijiji cha Igundu anayesoma katika shule ilyoko katika msingi kijiji jirani cha Mwankima darasa la sita, anasema umbali wa safari ya shule, wakati mwingine inawakatisha tamaa kuendelea na masomo, hasa kipindi cha mvua wanalazimika kuacha masomo kwa muda, mito ikijaa maji na hatari kwao.

Anasema, kwao wanafunzi wa kike wamekuwa wakikumbana na changamoto za kufuatiliwa na wanaume njiani, hasa wanapopewa lifti za usafiri.

**MWANAKIJIJI**

Cosmas Masunga, ni mwananchi wa kijiji hicho cha Igundu, anayesema baada ya kuhamasishwa kujenga shule ya msingi kijijini kwao, ikabidi waitikie wito huo, kwa sababu ni faida kwao na watoto wao.

Anasema kutokana na umbali huo wa shule kwenda kwenye kijiji jirani, anakiri watoto wao wanateseka sana, nahasa kipindi cha mvua ni hatari zaidi.

"Madarasa matatu ambayo yamesalia kujengwa tunaahidi kuendelea kuhamasishana kuyajenga ili shule yetu ipate usajili kamili wa kutoa elimu ya msingi na kuwaondolea changamoto watoto wetu kusoma umbali mrefu," anasema Masunga.

ELIMU

NA NEBART MSOKWA, MBEYA

SHIDA YAANZIA UKUNGA...

# Mtoto mwenye ulemavu alia kusoma na kuandika, juhudi zaishia hewani

• Mtoto, mama watapatapata bila mafanikio • Baba: Namhangaikia, watu waniambia... • Kijiji, wanaharakati wajiunga vitani



Mwandishi wa makala hii, akizungumza na Trans Mzumbwe, nyumbani kwao katika kijiji cha Mlowo, wilayani Mbeya. **NA MPIGA PICHA WETU**

TRANS Mzumbwe (17), ni kati ya watoto watatu wa familia ya Mzee Neva Mzumbwe, mkazi wa kijiji cha Mlowo, kilichopo katika Kata ya Isuto, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Kijana huyo ni mlemavu wa miguu yote miwili, hawezi kutembea wala kusimama na badala yake, anakaa na kutambaa, licha ya kuwa na umri mkubwa. Inaelezwa kiafya, miguu yake haina nguvu.

Mbali na ulemavu huo wa miguu, pia ana ulemavu wa mikono pamoja na shingo, kwa maana mikono yake imejikunja kiasi kwamba kiganja chake hakiwezi kushika vitu sawa sawa na kichwa kinatikisika, wakati wote kutokana na matatizo aliyo nayo ya shingo.

Kingine ni kwamba, kijana huyo ana tatizo lingine la kushindwa kutamka neno kwa usahihi baadhi ya maneno, hivyo ili aeleweke vizuri, msikiaji anatakiwa akae naye kwa muda mrefu kumfuatilia.

> Waliniambia kuwa mtoto alikatwa vibaya kitovu wakati anazaliwa na kwamba ndio chanzo cha matatizo.

### MWANZO WAKE

Kwa mujibu wa mama mzazi wa kijana huyo, Mesia Shusa, alijifungua mtoto Juni 9, mwaka 2003 nyumbani kwa mmoja wa wakunga wa jadi waliokuwa maarufu katika kijiji hicho, kabla ya serikali kuanzisha opereshemi ya kuwapiga marufuku wakunga hao.

Anasema mtoto huyo ni wa pili, akitanguliwa na kaka yake, Isaya Mzumbwe na kisha akafuatia mdogo wake, Lista Mzumbwe, ambaye ni wa mwisho na wa kike pekee kwenye familia yake.

Mama Mesia anasema, baada ya kujifungua mtoto Trans, alibaini ana tatizo la shingo, kutokana na kuchezesha kichwa muda wote, lakini matatizo mengine aliyabaini baadaye, baada ya kijana huyo kufikisha umri wa miezi sita.

Anasema baada ya kugundua hayo, alimpeleka kwenye zahanati ya kijiji cha Isuto kwa ajili ya matibabu na alipofika akaambiwa na manesi, kuwa matatizo ya mtoto huyo yalianzia wakati alipokuwa anazaliwa.

"Waliniambia kuwa mtoto alikatwa vibaya kitovu wakati anazaliwa na kwamba ndio chanzo cha matatizo. Walimpimia sindano tano ambazo alichomwa zote, lakini bado hakupona," anasema Shusa.

Anasema kutokana na hali ya mwanawe huyo, hadi sasa hawezi kumuacha nyumbani peke yake na kwenda kufanya kazi shambani, kwa sababu anahitaji kusaidiwa kila anachotaka kukifanya.

Mama huyo wa Trans, anasema kijana wake alipofikia umri wa kwenda shule, hawakuwa na uelewa kuwa watoto wenye ulemavu wanastahili kusoma, hivyo aliamua kubaki naye nyumbani muda wote.

### AKOSA SHULE

Anasema baada ya muda baadhi ya watu waliwashauri yeye na mumewe, Mzee Mwakazizi, wampeleke mtoto huyo shule, lakini walishachelewa, kutokana na umri wake mkubwa, ambao hauwezi kumruhusu kuanza darasa la kwanza.

Hata hivyo, anasema shule za maeneo ya jirani ikiwamo Shule ya Msingi Mlowo, iliyoko umbali wa kilomita moja kutoka nyumbani kwake, ilishindwa kumpokea kwa sababu haina miundombinu rafiki kwa wanafunzi wenye ulemavu kama alivyo kijana huyo.

"Hata wangekubali kumpokea, bado ingekuwa kazi ngumu kwangu, maana ningelazimika kumpeleka kila siku na kwenda kumchukua. Mazingira yetu ni ya milima, asingeweza kufika peke yake," anasema Mesia.

Vilevile, anasema kutokana na hali ya uchumi wa familia yake kuwa ngumu, hakumudu kufanya juhudi za kumpeleka mtoto huyo kwenye shule zinazopokea watoto mchanganyiko na wenye mahitaji maalumu ya kilemavu.

Mama huyo anasema, alipewa taarifa na baadhi ya watu kuwa shule hizo zipo mjini, hivyo akashindwa kumpeleka mtoto huyo na badala yake akabaki naye nyumbani.



Kijana mwenye ulemavu, Trans Mzumbwe (katikati), akiwa na mama yake, Mesia Shusa na kulia ni baba yake, Neva Mwakazizi katika Kijiji cha Mlowo wilayani Mbeya. **PICHA ZOTE: NEBART MSOKWA**

Pia anasimulia pindi mwanawe huyo alianza kumsumbua kuwa anataka kwenda shule, hakuwa na namna yoyote ya kumpeleka, kutokana na mazingira ya eneo hilo na hali yao kiuchumi.

"Muda sio mrefu kuna watu ndio wamemletea msaada wa baiskeli ya magurudumu matatu, ambayo alikuwa anaihitaji na angeipata kwa wakati ule alipokuwa mdogo, ingetupa hata nguvu ya kumtafutia shule mjini," anasema Mama Mesia.

### BABA ALONGA

Mzee Mzumbwe anasema kutokana na maisha kuwa magumu na wakati mwingine, amekuwa akisafiri kwenda kutafuta pesa katika sehemu mbalimbali za nchi na huwa anakaa muda mrefu bila ya kurejea.

Anasema, kutokana na kukaa muda mrefu kwenye vibarua, baadhi ya watu wamekuwa wakimtafsiri kama anakimbia majukumu ya kulea mtoto wake kitu ambacho anasema sio kweli, naye binafsi anampenda mtoto huyo kama ilivyo kwa wenzake.

Mzee Mzumbwe, anasema angekuwa anakimbia jukumu hilo na asingerejea kabisa na yeye huwa anatamani wakati wote angekuwa anakuwa karibu na familia yake, lakini hali ya uchumi ndio inamzungusha safari za mbali.

Anajitetea kwa mfano, kuna kipindi alishawahi kwenda kutafuta kazi mkoani Tanga, alikokaa miezi saba bila ya kurejea na ndipo yalipoibuka maneno kuwa ananuia kuitelekeza familia kutokana na ulemavu wa mwanawe.

"Nilishakubaliana na hali aliyo nayo mwanangu na sijawahi kuwa na wazo la kumnyanyapaa na natamani sana mwanangu angekuwa anapata mahitaji yote muhimu, lakini hali yangu ya uchumi ndio kikwazo kwangu na ndio maana huwa naenda kutafuta hela," anaeleza Mzumbwe.

Baba huyi anasema, kwa sasa mwanawe anasumbua sana, kutokana na kudai kila siku kwenda shuleni, lakini wanashindwa kumtekelezea hitaji hilo, kutokana na mazingira yao pamoja na hali ya uchumi.

Ombi la baba huyo ni kuelekea kwa wadau wenye uwezo, wamsaidie kumpeleka mwanawe huyo shule, ili akatimize ndoto yake ya kibinadamu, aliyoikosa na kwamba hata kama atasoma katika mfumo ambao sio rasmi.

### MLEMAVU AFUNGUKA

Mtoto Trans ambaye hajui vizuri lugja ya Kiswahili, zaidi akitumia lugha ya asili ya kabila la Kimalila, katika tafsiri inayohiyaji umakini kumfuatilia, anasema kwamba kikuu anachokitaka ni kwenda shuleni akajifunze kusoma, kuandika na kuhesabu.

Hisia za hitaji lake analifananisha na alilo nalo mdogo wake, Lista ambaye kwa sasa anasoma kidato cha pili. Anaendelea: "Nataka na mimi nivae nguo za shule, nataka niwe na uwezo wa kusoma chochote nitakachokuwa nakiona, kwa sasa sijui chochote."

### MWANAHABARAKATI JE?

Mmoja wa wanaharakati wa kutetea haki za watu wenye ulemavu, Frank Mwashilindi, anaanza kuitetea elimu kuwa miongoni mwa haki za msingi za watoto, huku akirejea Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009.

Anasema aliwahi kumwombea Trans nafasi kwenye shule mbalimbali za Kata ya Isuto, lakini ilishindikana kutokana na walimu wa shule hizo kueleza kuwa shule hazina miundombinu rafiki kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu.

Mtetezi huyo anasema, kutokana na changamoto hiyo alienda mpaka katika Jiji la Mbeya yalipo makao makuu ya Chama cha Watu wenye Ulemavu, ili kupata utaratibu ambao ungesaidia Trans kusoma shule, lakini ilishindikana kwa anachokitamka 'hakupata ushirikiano wa kutosha.'

"Sasa tunaiomba serikali iweke miundombinu rafiki kwa wanafunzi wenye ulemavu na wasiokuwa na ulemavu katika shule zote. Tulipoomba nafasi katika Shule ya Msingi Mlowo, walisema hawana vyoo ambavyo vingefaa kwa Trans," anasema Mwashilindi.

Ushuari wake anataka ni vyema serikali ikajenga shule za kutosha kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu, ili kuondoa changamoto kama inayomkabili Trans.

Anasema kwa sasa wanaendelea kuwahamasisha wananchi kuwafichua watu wote wanaowaficha watoto wenye ulemavu, ili kila kijiji kiwe na taarifa sahihi juu ya idadi ya watoto wenye ulemavu.

Hata hivyo, anaiomba serikali kuiingiza familia hiyo kwenye Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini nchini (Tasaf), ili kuepusha mizunguko ya mzazi wa kiume kwenda kutafuta fedha na kumwachia mwanamke jukumu la kulea watoto.

### MTENDAJI KIJIJI

Kaimu Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mlowo, anasema baada ya kubaini kuwapo watoto wenye ulemavu wanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo ya elimu, waliamua kufanya sensa katika kijiji kizima ili kujua idadi halisi ya watoto wanaoangukia kundi hilo.

Anasema walipofanya sensa hiyo mwaka 2017, waligundua kuna watoto wenye ulemavu saba na kwamba ilibainika kuwa Trans ndio mwenye changamoto kubwa zaidi kuliko wenzake, kutokana kuwa na ulemavu wa viungo vingi.

> Walimpimia sindano tano ambazo alichomwa zote, lakini bado hakupona.

Ofisa Mtendaji huyo anasema, baadhi ya watoto hao wana ulemavu wa kiungo kimoja kimoja kama miguu, mikono na kwamba mmoja naye ana tatizo kubwa la kutoona macho yote.

"Sisi kama serikali ya kijiji, tumekuwa tukiwaunganisha watoto hawa na taasisi mbalimbali ambazo zinasaidia watu wenye mahitaji, lakini tunamshukuru Mungu mpaka sasa Trans ameshasaidiwa baiskeli," anasema Mwaniwanga.

Anasema kijiji hicho ni miongoni mwa vichache ambavyo havijanufaika na Mpango wa Taifa wa Kunusuru Kaya Maskini (Tasaf) na kwamba endapo mradi ungepita katika familia hiyo, ingekuwa msaada kwao.

Mwaniwanga anawaomba wadau mbalimbali kuendelea kuwasaidia watoto wenye ulemavu wanaoishi katika kijiji hicho, kuwapunguzia changamoto zinazowakabili kutokana na ulemavu walio nao.

HAKI, UWAJIBIKAJI & VITA YA RUSHWA

## Hii ndio haki na gharama zake



Kikao kinachohusu haki za jinsia, kupitia Dawati la Jinsia, Polisi Wilaya ya Kinondoni. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Niko Kasera**

NI ngumu siku kupita bila ya kusikika haki zikidaiwa katika maeneo mbalimbali. Katika mahakama, sehemu kubwa kama si zote katika kesi za madai, zinaagukia madai ya haki.

Hiyo haishii mahakamani pekee, hata katika nyumba za sheria kama vile vituo vya polisi, kwenye serikali za mitaa na nyumba za ibada, hata katika lugha ya masihara.

Mathalan, madai ya haki mrundikano ulipokuwa mkubwa na msukumo wa upatikanaje wake kuwa mpana, ililazimu chombo hicho cha kusimamia sheria, haki na usalama, kuunda Dawati Maalum la Jinsia.

Lengo hilo ni kuingiza mkono wake, kujitahidi kusawazisha hayo nje ya mahakama na mambo yakaenda sawa, kwa misuguano yote yenye mtazamo wa kifamilia. Iko wazi, tangu kuwapo kwake, mchango katika kusawazisha madai ya haki katika eneo hilo uko juu.

Inapozungumziwa haki kwa jumla, ina mustakabali mpana sana. Haki za kinamama, wafanyakazi wa ndani, jamii zenye uchumi duni, wanyonge, wanaobaguliwa na kudhalilishwa, wasomaji na hata anayetuhumiwa au kuthibitika ni fisadi au jinai nyiginezo, bado kuna haki za kuisikilizwa, ambayo kisheria inajulikana kama 'Natural Justice.' Kwa kifupi, dhana haki ina orodha ndefu.

Jambo moja la kufahamu ni kwamba, ina podaiwa haki, ikumbukwe upo upande ambao utalazimika kunyang'anywa haki zake, ili haki ile ya kwanza inayodaiwa ipatikane.

Kwa maneno mengine, mtu anajikuta ili kutetea haki, inabidi anyang'anye haki. Upande unaolazimika kupoteza haki kufidia haki inayodaiwa.

Kwa mfano, mtoto anapodai haki, maana yake inamlazimu mzazi kupoteza haki zake ili kumpatia mwanawe haki, mathalani kumbembeleza. Kwa maneno mengine, haki ya mtoto inakuwa utumwa kwa mzazi.

Mwanafunzi wa kike anapodai haki ya kusoma kwa upendeleo, inabidi mamlaka zinazohusika kubinya haki za wavulana kwa kiasi fulani, ili haki hiyo inayodaiwa itimie na huenda mabinti hao huko nyuma walipoteza haki sana zilizowaendea wavulana.

Sasa hapa ndiko liliko swali langu. Haki maana yake nini?

Na haki hizi ni kwa ajili ya nani? Jamii, kikundi cha watu fulani wanaodai rehema au mtu binafsi?

Inakuwaje kama tukiamua kuzivunja haki hizi, je, haki ni kutii sheria na taratibu zilizopo kwa lengo tu la kuepuka adhabu?

Je, haki ni kile kinachoweza kufanywa na watu wengine, ili kutupa sisi faida, hata kama kufanya hivyo kunawaumiza wao? Je, wao hawana haki?

Je, haki ni kuwa mtu mzuri anayekubalika kwenye jamii?

Je, haki ni kutimiza matakwa ya sheria zilizopo hata kama zinaingilia uhuru wangu?

Je, haki ni kutetea matakwa ya wengine, hata kama kufanya hivyo kunakunyima vitu fulani Fulani?

Je, haki ni matakwa ya kibinafsi yasilazimika kushahibiana na sheria zinazoonekna ni halali katika jamii?

Kumbuka palipo na haki kuna gharama upande fulani, kama ilivyo kwa mzazi anayejinyima na kujitesa, ili mtoto apate haki yake ya asili. Askari anajitoa na kunadi usalama binafsi, ili kuuhakikishia umma anaouteea usalama. Nao wananchi wanadai, sehemu ya matunda ya uchumi wao kuwawezesha askari kutimiza majukumu yao kwa ufanisi.

**Makala hii ni kwa mujibu mijadala ya kitaalamu katika mitandao, ikiwamo bwaya.blogspot.com, ya Februari 4, 2009.**

SAYANSI

NA MWANDISHI WETU

MAAJABU YA ELIMU

# Dunia ilipoketi kusomeshwa mazingira na binti miaka 16



Greta Thunberg, alipokuwa mkutanoni New York, Marekani. **PICHA: MTANDAO**

MAWASILIANO yamepiga hatua katika kuondoa tofauti za kitabaka na rika siyo katika jamii peke yake, ila hata katika diplomasia, eneo ambalo kwa jadi wadogo hawawezi kufika, kwani mchujo wa jina la mtu kusikika huko ni mkali kuliko mazingira ya jamii ya kawaida.

Ila hali hiyo sasa imeanza kuonekana, ambako dunia hivi karibuni ilifunzwa na kusutwa na mtoto wa miaka 16 anayesema 'asingepoteza muda wake kuongea na Trump' baada ya mkutano wa kimataifa kuhusu hatua za kudhibiti mabadiliko ya tabianchi mwezi Septemba mwaka jana.

Inapofikia mahali wakubwa hawajui waseme nini au wafanye nini, watoto wanasimama na kuanza kuonyesha njia, na hata kuonyesha tu aibu kile ambacho kinafanyika.

Hivyo dunia inajiuliza maswali kupamba moto kwa majanga yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi, kuna mabadiliko mengine ambayo hayakutazamiwa ya rika la vijana au tabaka la wanaharakati wa umri mdogo kushika usukani katika kusukuma mabadiliko kote duniani.

Suala la vijana, na hasa wa vyuo vikuu kuhusika na mabadiliko maeneo mengi duniani siyo jipya, lakini uhusika wao katika ngazi ya kimataifa ni jambo geni.

Katika mkutano uliopita wa Umoja wa Mataifa kuhusu hali ya hewa uliofanyika New York, Marekani, sauti iliyosikika kuliko zote ilikuwa ya mtoto kutoka Sweden, Greta Thunberg.

> Ambacho kinastaajabisha katika harakati ya mtoto huyo ni kuwa hakuinuliwa na kikundi chochote ila ana uwezo wa kujieleza yeye mwenyewe.

Kuingia kwa mtoto huyo mwenye umri wa miaka 16 katika malumbano kuhusu changamoto za tabianchi ni tukio la kushangaza, kwani tofauti na wengi walivyokuwa wanadhani, mtoto hajainuliwa tu na shirika fulani lisilo la kiserikali ili sauti yake isikike, badala ya shirika hilo.

Kinachoonekana katika mitandao ni kuwa alianzisha harakati ya migomo shuleni nchini Swaden na baadaye Scandinavia kutaka serikali zianze kuchukua hatua muhimu na za haraka kwa suala hilo, nchini na kimataifa.

Tangu aanze harakati hizo katikati ya 2018 amepata sifa na tuzo lukuki, anafahamika dunia nzima, aliorodheshwa tuzo ya Nobel.

Tayari kuna vitabu viwili ambavyo mtoto huyo ndiye mwandishi au mzungumzaji mkuu, hasa 'No One is Too Small to Make a Difference,' (Hakuna aliye mdogo mno asilete tofauti) kilichochapishwa mwezi Agosti mwaka 2018, ambako kuna hotuba 11 alizozitoa katika harakati hizo.

Zaidi ni kuhusu kuongezeka kwa joto duniani na mabadiliko ya tabia nchi, ambako orodha ya watunzi inaonyesha kuwa familia yake ilihusika kwa karibu, akiwamo baba yake, mama na ndugu zake Svante, Beata.

Ni baada ya mafanikio nyumbani kwa harakati hiyo, ambao alijenga kwa kuandamana na bango nje ya Bunge la nchi hiyo akitaka shule zifanye migomo kwa suala hilo, na punde akaanza kupata wafuasi Ulaya na kwingineko.

Akiwa nyumbani, mtoto huyo alifaulu kuishauri familia yake iachane na safari za ndege pamoja na kula nyama ili kusaidia kupunguza utoaji wa hewa haribifu duniani, na mazingira hayo ya nyumbani yakampa nguvu na ari katika harakati zake shuleni na nje ya jengo la Bunge.

Kwa baadhi ya wachunguzi, alichofanya mtoto huyo ni moja ya miujiza ya siku za karibuni, ambako hisia za kimataifa kuhusu mabadiliko ya tabia, hasa kuchoshwa na mwelekeo wa taasisi za kimataifa na serikali duniani kutofanya lolote muhimu la wazi, ndiye msemaji wake.

Ni ule usemi wa kuzuia watoto, halafu mawe yaseme.

Ambacho kinastaajabisha katika harakati ya mtoto huyo ni kuwa hakuinuliwa na kikundi chochote ila ana uwezo wa kujieleza yeye mwenyewe.

Ni mtoto mwingine aliyeteka hisia za dunia katika miaka ya karibuni baada ya Malala Yousafzai, binti wa Pakistan aliyezaliwa mwaka 1997 ambaye mwaka 2012 akiwa katika basi kutoka shuleni kurudi nyumbani alipigwa risasi kichwani na mpiganaji wa Taliban aliyevaa soksi usoni kujificha, kutokana na michango yake katika vipindi vya radio ya Uingereza kwa lugha ya Urdu, inayozungumza kote nchini Pakistan.

Hakufariki, alipelekwa Uingereza kutibiwa na kusaidia kutoa picha halisi ya ukandamizaji dhidi ya elimu kwa watoto wa kike unaofanywa, kushadidiwa na makundi ya siasa kali na wengi wakapata picha tofauti ya makundi siasa kali na itikadi zao ni zipi hasa.

Harakati zilizofikisha dunia kuwatambua Malala Yousafzai na Greta Thunberg siyo rahisi kutatuliwa na walio madarakani au wenye nafasi katika nchi tofauti, na imefikia mahali ambapo dunia inachoweza kufanya ni kutoa sauti na kusikika.

Ni katika hali hiyo ambako watoto wadogo wanaweza kuleta kitu tofauti, kwani siyo kawaida kwa mtoto mdogo kuwa na neno la kusema linalosikilizwa siyo tu ndani ya nchi hii au ile ila dunia nzima ione umuhimu wa kufuatilia anachosema. Imefika hatua hata wakubwa wa dunia wanaanza kuweka tegemeo lao kwa sauti hizo, kwamba katika kauli ya mwisho ndizo zitasikilizwa.

Umuhimu wa harakati aliyoendesha Thunberg imeonekana bayana katika salamu za mwaka mpya za Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, ambaye alionekana kukwepa lawama kuhusu suala la nini cha kufanya, kiaina.

Katika salamu zake za mwaka mpya kwa wawakilishi wa mataifa mbalimbali na nchi wanachama, Guterres amesikitishwa na athari za mabadiliko ya tabianchi katika mwaka uliopita, akisema kwa mwaka huu unaoanza, tumaini liko katika kizazi kipya.

Ni mwelekeo wa hisia unaotokana na kazi iliyofanywa na mwanaharakati huyo mtoto tu wa Sweden, kuwa inawezekana sauti kama ya kwake, au sauti yake na wengine wa rika hilo kote duniani, wakasikilizwa na watawala.

Unaweza kuelewa kwanini Guterres, aliyekuwa Waziri Mkuu wa Ureno miaka kadhaa iliyopita, anaweka matumaini yake kwa kina Thunberg, kwani Umoja wa Mataifa hauna nyenzo za kuleta maelewano duniani kuhusu suala hilo. Tayari Marekani imejitoa katika mikutano ya kimataifa ya kujadili nini cha kufanya kuhusu tabianchi, kwani utawala wa Rais Donald Trump unaona dunia inataka tu kuilalia Marekani itoe pesa nyingi kwa suala hilo.

Bila Marekani umuhimu wa mikutano hiyo unapungua nguvu zaidi; ni hapo utegemezi unaanza kuwa labda sauti za kina Greta zisikike Ikulu ya Marekani, ibadilike.

ELIMU

# Mhitimu uhandisi 'anayepiga kiwi' ajutia safari ya shule

• Kiwi imemdhamini msingi hadi digrii

CHEKOLE Menberu, mwenye umri wa miaka 27, alikuwa na matumaini makubwa ya kupata ajira baada ya kumaliza masomo shahada yake ya uhandisi wa kemikali miaka miwili iliyopita nchini Ethiopia.

Ulikuwa wakati wa ukombozi, akiangalia miaka aliyoteseka kufikia kiwango hicho cha elimu cha chuo kikuu.

Kwa miaka mingi, amekuwa akisafisha viatu barabarani ili aweze kujikimu kimaisha na tangu akiwa mdogo, Chekole alikuwa anafanya shughuli za mtaani.

Baba yake alifariki katika umri wake mdogo, hivyo akahamia kwa babu na bibi yake waliopo eneo la Amhara, mahali alikoolewa tena mama yake.

Anakumbuka historia yake, kwamba alitaka sana kwenda shule, lakini babu na bibi yake hawakuwa na uwezo wa kumlipia ada na kumhudumia katika matumizi mengine.

Hivyo, anasema aliamua kwenda nyumbani kwa mjomba wake kumsaidia kazi za ufugaji, akiwa na matumaini kuwa babu na bibi yake wataweza kumsaidia.

"Nilikuwa ninawasumbua sana babu na bibi yangu wanipeleke shule," anasimulia na baadaye, walikubali maombi yake na kumtaka aende kujiandikisha katika shule ya serikali iliyoko mjini Woreta.

Juhudi za kijana huyo zilikwama, baada ya msaada wa babu yake kukatika ghafla alipokuwa darasa la pili. Anaendelea: "Ilinibidi niondoke na kwenda mtaani kutafuta namna ya kujisaidia mwenyewe."

Kwa msaada wa rafiki yake ambaye, alimwezesha kuanza kazi ya kusafisha viatu, akiwa darasa la tatu mpaka alipomaliza chuo kikuu, fedha alizozipata, alilipa ada.

"Nilidhani kuwa kusafisha viatu ni kazi ambayo ingeweza kunisaidia. Nusu siku nilitumia kufanya kazi na nusu siku nilitumia kusoma, anasimulia na kuongeza:

"Maisha yalikuwa magumu sana, lakini nilikuwa ninajipa moyo kwa simulizi za watu ambao walikuwa wanafikiri kama mimi na mwisho wa siku wakawa madaktari au wahandisi."

Kila mwaka wa masomo ulipoanza, msongo wa mawazo ndio ulipoanza, kwa sababu ilimbidi kununua sare za shule ambazo alikuwa anapata wakati mgumu sana kumudu kuzinunua na anaeleza: "Elimu ilinigharimu sana.

"Nilikutana na wakati mgumu mara nyingi, lakini siwezi kusahau jinsi nilivyokuwa nakata tamaa, nilipokuwa kidato cha nane mpaka 10 na mwaka



Chekole Menberu, katika mazingira tofauti ya maisha yake, shule na mtaani katika kusafisha viatu. **PICHA: MTANDAO.**

mwingine nilijiunga chuo kikuu."

Pamoja na changamoto nyingi ambazo alikutana nazo, mwaka 2013, alifanikiwa kuingia Chuo Kikuu cha Bahir Dar, katika mji mkuu wa Amhara, alikosomea Uhandisi Kemikali.

"Kulikuwa na uvumi kuwa nchi inahitaji wahandisi wengi katika viwanda ndio maana niliamua kusomea masomo ya uhandisi. Nilikuwa natumaini kuwa nitaajiriwa nikihitimu masomo yangu," anasema.

Maisha yake ya chuo kwa miaka mitano yalikuwa magumu kama ilivyokuwa awali, pamoja na kuwapo barua ya kutaka apewe msaada, wakati huo chuo kilikuwa kinanilipa dola 10 (Sh. 24,000) kwa mwezi.

"Nilikuwa nikipata msaada kutoka kwa marafiki zangu na wanafunzi niliokuwa nakaa nao. Lakini wakati siku ya kuhitimu chuo ilipokaribia, hofu ilizidi nikifikiria kama nitaenda kuajiriwa baada ya kuhitimu chuo kikuu.

"Nilikuwa na hofu kuwa sitapata ajira," alisema.



> Kulikuwa na uvumi kuwa nchi inahitaji wahandisi wengi katika viwanda ndio maana niliamua kusomea masomo ya uhandisi.

**ALIPOHITIMU**

Mwaka 2017, bwana Chekole alihitimu shahada ya uhandisi na jambo la kwanza alilolifanya ni kutafuta ajira, lakini hakufanikiwa, anaongeza: "Nilitumia miezi mitatu kutafuta ajira katika mji mkuu wa Ethiopia, Addis Ababa.

"Nilizunguka katika viwanda vingi kutoka mji mmoja kuelekea mwingine ili kutafuta ajira lakini sikuweza kufanikiwa."

Anasema, alisafiri miji mingi bila mafanikio yoyote, akisimulia: "Niliomba kazi ambazo walikuwa hawataki kiwango cha shahada, lakini maombi yangu yalikataliwa na waajiri wote."

Anasema, baadaye alipata kibarua kiwandani alikolipwa dola moja (Sh. 2,400) kwa siku, lakini aliiacha kwa sababu kiwango kilikuwa kidogo kukimu mahitaji yake.

Kijana huyo anasema, baada ya miezi kadhaa ya kutafuta ajira ya elimu yake, alirudi Bahir Dar - na kufanya kazi ambayo akutegemea kurudi kuifanya tena ya kusafisha viatu.

"Nilipoona kuwa nilikuwa sina namna nyingine ya maisha, niliamua kwenda kufanya kazi ya kusafisha viatu tena," anasema, huku akijilaumu kwenda shule, keamba asingekuwa katika hali ngumu ya kiasi hicho cha sasa.

"Elimu imenigharimu mno na sijapata tuzo katika changamoto zote alizopitia," anasema na kuongeza: "Nisingejitolea kiasi hicho kwa ajili ya kupata elimu."

Chekole analalamikia serikali ya Ethiopia kuangazia zaidi masuala ya siasa na usalama zaidi ya kutengeneza ajira kwa watu ambao hawana ajira.

"Walimu wangu walifahamu kuwa nilikuwa ninajilipia chuo kwa fedha nilizopata kwa kusafisha viatu, walinipa moyo na hata walikuwa wananisaidia na hela... marafiki zangu niliosoma nao chuo walikuwa wanakuja kusafisha viatu vyao na kunipatia fedha," anasimulia.

Licha ya changamoto, anasema bado ana matumaini ya kupata ajira siku za usoni.

Ethiopia imekuwa ikikabiliana na changamoto za kiuchumi hivi karibuni, vijana wenye umri kati ya miaka 15 mpaka 29 katika maeneo ya mjini hawana ajira.

Kwa mwaka jana, vijana wasoajiriwa waliongezeka kwa asilimia 22 kutoka mwaka 2016, kwa mujibu wa takwimu za nchi.

**BBC**



WADAU
**SABATO KASIKA**

# Sauti za wadau

## Baadhi ya wazazi wana kawaida ya kuwachagulia watoto wao masomo shuleni, ili wanapohitimu, wafanye kazi ambayo wao (wazazi) hao wanaitaka. Wadau wana maoni gani?



**JUMA KITIA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

YAPO mambo ya msingi, ambayo mzazi anapaswa kuyafanya kwa mtoto, kwa kutambua kwamba ndiye mwalimu wake wa kwanza, na ndiye kwa kiasi kikubwa mtoto hujifunza na kuiga mambo mbalimbali kutoka kwake.

Kwa hiyo mzazi anatakiwa kuhakikisha anamfundisha mtoto wake mambo muhimu anayopaswa kujifunza, ili akue katika malezi bora na awe na baadaye njema.

Hivyo kwa kutambua umuhimu wa mzazi katika malezi, anatakiwa kumfundisha mtoto wake mambo kadhaa muhimu ikiwamo matumizi mazuri ya muda.

Matumizi ya muda ni suala muhimu kwa kila mtu, tena ni msingi wa mafanikio kwa kila mtu. Hivyo mzazi au mlezi anapaswa kumfundisha mtoto wake matumizi ya muda tangu akiwa mdogo, ili akue akiwa na tabia hiyo.

Mzazi au mlezi amfundishe mtoto wake kama vile kuamka mapema, kulala kwa wakati, kuwahi eneo husika kwa muda stahihi, kujiwekea ratiba na kuifuata. Kuna suala la elimu ya jinsia.

Wazazi wengi hudhani kwamba kuwafundisha watoto wao elimu hiyo ni kinyume na maadili au ni kuwafundisha tabia mbaya.

Hili limetoa mwanya kwa watoto wao kupata elimu potofu kutoka kwa marafiki au watu wasio sahihi. Nikirejea kwenye suala la kumchagulia mtoto mambo ya kusomea, ninadhani siyo sahihi. Kama mzazi daktari, asilazimishe mtoto naye awe daktari. Unaweza kukuta yeye ana ndoto zake nyingine kabisa.

Hivyo watoto waachwe huru kuchagua kile wanachotaka kusomea kulingana na uwezo wao darasani na jinsi ambavyo wamepanga kutimiza ndoto zao.



**JANETH MAWINZA (MKURUGENZI WA TAASISI YA WAJIKI)**

WAJIKI linaweza kuwa jina geni, lakini kirefu chake ni Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo.

Kuhusu swali lako ni kwamba, kutambua kipaji cha mtoto na kukiendeleza ni jambo la msingi sana kuliko kumlazimisha mtoto asomee taaluma ambayo haipendi, na baadhi ya wazazi wamekuwa na tabia hiyo ya kutaka watoto wasomee kile ambacho wao (wazazi) wanataka.

Kwa mtazamo wangu ni kwamba sioni kama uamuzi huo una mantiki, hasa kwa kuzingatia kwamba mtoto naye huwa anakuwa malengo yake ya baadaye. Watoto waachwe wasomee kile wanachokitaka.

Suala la uendeleza vipaji vya watoto, kwa wenzetu Wazungu wanalizingatia sana, lakini huku kwetu utasikia mzazi anasema anataka mtoto wake awe rubani au mhandisi wa majengo ama fani nyingine yoyote bila kuangalia mtoto ana kipaji gani na kumlazimisha achukue masomo fulani, ambayo wakati mwingine ni magumu kwake. Mfumo huo siyo sahihi kabisa ni kuingilia na kumharibia mtoto ndoto zake. Mzazi anaposaidia kuendeleza kipaji cha mtoto wake, faida zake si kwake peke yake bali pia kwa jamii nzima.

Kwa hiyo ni vyema wazazi wanaowachagulia watoto wao masomo wakalielewa hilo. jambo la msingi ni mzazi kufuatilia maendeleo ya mtoto wake na kubaini uelekeo wake uko upande upi na kumuhimiza aongeze kasi ili kufikia kile anachokitafuta kwa baadaye.

Vipaji vya watoto vimekuwa haviendelezwi, kwa sababu tu mzazi anataka mtoto wake awe katika nafasi ambayo haiwezi.



**FATMA MACHONGWE (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

JAMBO hili lina mkanganyiko sana, kwani pia wapo baadhi ya wazazi wanaofanya kazi fulani na hawataki watoto wao waje kuifanya hata kama wanaitamani, badala yake wanawakazania wasomee taaluma nyingine, ambayo wakati mwingine hawaipendi.

Miongoni mwa kazi hizo ni ya ualimu. Bila kufanya utafiti, ni kwamba wazazi ambao ni walimu na hasa wa shule za msingi, hawatamani watoto wao waje kuwa walimu, hata kama watoto hao wanaitaka kazi hiyo na ndiyo wanadhani wanaimudu.

Ikumbukwe kuwa kazi nyingine kama ualimu ni wito, hivyo wito wa mtoto unaweza kuwa huko, lakini mzazi akataka alazimishe asomee kingine. Ninadhani hiyo itakuwa ni kumvuruga mtoto. Aendelezwe kipaji chake hicho cha ualimu, ili baadaye aje kulitumia taifa kupitia taaluma ya ualimu.

Mimi nina amini kwamba kila mtu tangu akiwa tumboni mwa mama yake, Mungu alishatupangia kazi ya kufanya katika jamii zetu.

Kwa hiyo wazazi wanapoamua kuwachaguliwa watoto wao kazi ya kufanya, wajue wanakwenda kinyume kabisa na matakwa ya watoto wao na wanaweza kuwaharibia kabisa matarajio ya baadaye, hata kama mzazi alikuwa ni mwalimu halafu akakutana na changamoto kwenye taaluma hiyo, asidhani kwamba hata kwa mtoto itakuwa hivyo.



**TUNZA MGAYUKO (MKAZI WA MJINI MOROGORO)**

KWANZA kabisa ni vyema jamii ikaelewa kuwa dunia ya leo yenye ushindani mkubwa katika elimu, inahitaji maandalizi ya watoto, ili wawe katika nafasi nzuri kushindana.

Hivyo kuna uhitaji mkubwa wa kipaji cha mtu binafsi ukiachana na elimu anayopewa, na wazazi ndiyo wenye jukumu la awali kuibua na kukuza vipaji ndani ya watoto. Wazazi wanatakiwa kutenga muda ili kuwa karibu na watoto wao na kuwaangalia na kuzungumza nao kwa ajili ya kubaini mambo muhimu anayoyatilia mkazo katika masomo.

Kwa njia hiyo, wazazi wanaweza kujua ni vipaji gani watoto wao walivyo navyo na kuwajengea matarajio  kwa kuwatafutia hata vitabu ili wazidi kujijengea uelewa kwenye maeneo walioegemea, lakini pia siyo vibaya kumsaidia mtoto katika masomo, kutokana na ukweli kwamba wapo baadhi yao wanasoma tu wala hawaonyeshi wanataka kufanya nini au kuwa nani kwenye jamii hapo baadaye. Watoto wa aina hiyo ni wa kusaidia kuchagulia masomo na kuwahimiza wakazanie huko, ambako wazazi wamechagua na inawezekana wakafanya vizuri na hatimaye wakafanikiwa, katika maisha yao ya baadaye.

Hili linawezekana iwapo wazazi wanafuatilia maendeleo ya watoto wao shuleni, kutokana na ukweli kwamba watabaini kama kuna haja ya kuwachagulia, lakini siyo vibaya kumpa nafasi ya kumsikiliza kama ana jambo la kusema, ingawa ameshindwa kuchagua cha kusomea.



**RAMADHAN KIDOGA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

KUWEKEZA kwenye elimu ni hatua muhimu sana, katika maisha ya mtoto, lakini linapokuja suala la kutaka mtoto arithi taaluma ya mzazi wake au shughuli za mzazi wake ni jambo muhimu pia.

Wapo baadhi ya wazazi wanaopenda watoto wao wasomee kile ambacho wao wamesomea au wanachokifanya. Hili ni jambo jema ni mimi ninalitamani. Ukifuatilia utagundua kuwa wapo vijana wengi tu ambao wamefuata nyayo za wazazi wao iwe kwenye biashara shughuli nyingine za kitaaluma.

Unaweza kukuta mtu ni daktari, mwalimu au mfanyabiashara na angependa mtoto wake naye aelekee huko na ambao waliamua kufuata nyayo za wazazi wao wanaendelea na maisha kama kawaida. Hivyo kwa ujumla ni kwamba sioni tatizo mzazi kumchagulia mtoto wake masomo au kumwelekeza afuate nyayo zake.

Mzazi anafanya hivyo kwa lengo zuri na anamfundisha mbinu za kufikia huko aliko, na ndiyo maana siyo ajabu kukuta mzazi anafanya biashara na mtoto naye anaifanya au mtoto anasimamia biashara hiyo ya baba yake.

Matokeo yake biashara inazidi kupanuka na kuwa kubwa. Binafsi ninauona utaratibu huu kuwa ni mzuri kwa ya kurithisha kazi ya baba au mama kwa mtoto.





## Mamlaka yasambaza maji kutumia magari

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA) imeanza kusambaza maji katika baadhi ya maeneo ya Jiji la Mbeya kwa kutumia magari baada ya maeneo hayo kukosa huduma kufuatia vyanzo vya maji kujaa tope na takataka.

Ofisa Uhusiano wa Mbeya-WSSA, Neema Staton, alisema jana kuwa kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha mkoani hapa, baadhi ya vyanzo vya maji vimejaa tope na takataka, hivyo kusababisha maji yasiwafikie wananchi.

Alisema kutokana na hali hiyo wananchi wamekuwa wakipiga simu kulalamika kukosa huduma hiyo, hali iliyoulazimu uongozi kuanza kusambaza huduma hiyo kwa kutumia gari katika maeneo hayo hasa baada ya kujiridhisha.

Staton aliyataja baadhi ya maeneo ambayo wameanza kupeleka maji kuwa ni Kata ya Isyesye na katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi ambako wananchi wamekosa huduma hiyo kwa muda wa zaidi ya wiki moja.

"Ni kweli tunapokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi, sasa tukishayapokea tunaenda kujiridhisha na kisha kuanza kuwapelekea kwa gari japokuwa kuna baadhi ya maeneo yana changamoto ya usafiri," alisema.

Huduma hiyo, alisema inatolewa bure kwenye maeneo hayo na wananchi wanachota bila kuchangia chochote tofauti na ilivyo kwa maji yanayotoka bombani.

Aliwataka wananchi wa mkoa huo kuwa wavumilivu wakati matatizo yaliyopo yanashughulikiwa na kwamba baada ya mvua kupungua watasafisha vyanzo hivyo na huduma kurejea kwa wananchi.

# RC aamuru kung'olewa mabango ya 'masangoma'

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ameliagiza Jeshi la Polisi mkoani hapa kuyaondoa mabango yote ya waganga wa jadi yaliyobandikwa mitaani.

Mabango hayo ni pamoja na yake yanayoeleza kuhusu kuongeza nguvu za kiume kwa madai kuwa yanawaingiza wananchi kwenye majaribu ya kishirikina.

Chalamila ameagiza baada ya operesheni ya kuyaondoa mabango hayo kukamilika, ianze operesheni ya kukamata waganga wa jadi wote wanaokiuka taratibu za nchi na kuwafikisha kwenye vyombo vya dola.

Mkuu huyo wa mkoa alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki baada ya kuwapokea na kuwakabidhi watoto wawili wa familia moja, Faisal Mashaka (5) na Farhana Mashaka (mwaka mmoja na miezi mitano) ambao walikuwa wamepotea na kukutwa mkoani Tabora.

Alisema waganga hao wanawahadaa wananchi hasa vijana wakidai watawasaidia, lakini hakuna wanachowasaidia zaidi ya kuwaharibu na kuanza kuwachonganisha na ndugu zao.

"Tunataka waganga wa tiba mbadala ambao wanawasaidia wananchi ndio wabaki, lakini hawa wanaochonganisha na kufanya udanganyifu ambao unawaharibu watu wetu. Kwa hiyo naagiza mabango yote yaondolewe na hakuna wanachoweza kutufanya," alisema Chalamila.

Alisema kuna baadhi ya vijana wanaamini kuwa nguvu za kiume zinapatikana kwa waganga hao kitu ambacho si cha kweli, hivyo akasisitiza kuwa sheria itachukuliwa dhidi ya waganga hao endapo wataendelea.

Katika hatua nyingine, Chalamila alisema baada ya kupambana na waganga hao, atatangaza kuanza kuhakiki madhehebu yaliyomo ndani ya mkoa ili yanayokiuka taratibu na sheria yafungwe.

Alisema Jiji la Mbeya ni la pili barani Afrika kwa kuwa na madhehebu mengi lakini bado ni miongoni mwa majiji yenye matukio mengi ya ajabu ajabu.

Kwa mujibu wa Chalamila, baadhi ya madhehebu hayo yanakiuka taratibu na tayari ofisi yake imeanza kupokea malalamiko kutoka katika baadhi ya madhehebu yameanza kuhatarisha amani na utulivu unaoendelea ndani ya mkoa huo.

"Tutahakiki waumini wao, fedha zao na hata matumizi yao. Kuna kanisa wameanza kupigana na wanaweza wakahatarisha amani ya mkoa wetu. Tukishafanya uhakiki tutayafuta yanayokiuka taratibu na yale yanayofuata taratibu tutayaweka kwenye usalama," alisema Chalamila.

Kwa upande wake kiongozi wa machifu wa Mkoa wa Mbeya, Rocket Mwashinga, alisema kwa sasa mkoa huo umegubikwa na matukio mengi ya ajabu ambayo mengi yanaambatana na ushirikina.

Mwashinga alisema mbali na mkoa huo kuwa na neema ya makanisa mengi lakini badala ya matukio hayo kupungua, sasa ndio yanaongezeka na kuanza kutishia amani.

"Kila kukicha utasikia watoto wamepotea, watoto wamebakwa na mengine ya ajabu, sasa tunajiuliza kwa idadi hii ya makanisa, haya matukio yanatoka wapi?" Alihoji Mwashinga.

Kuhusu waganga wa jadi, Chifu Mwashinga aliiomba serikali kuchukua hatua haraka ili wale wote wanaokiuka taratibu washughulikiwe.

Kwa muda mrefu, mkoa wa Mbeya umekuwa ukigubikwa na matukio mengi ya ajabu, huku waganga wa jadi wanaopiga ramli, maarufu kwa jina la 'lamba lamba' wakiwahadaa wananchi kwa kuwachangisha fedha wakidai wanataka kuondoa vitu vya ajabu.



Mmoja wa walimu (kulia), wa vituo vya makuzi na malezi ya watoto wenye umri katika ya miaka mitatu na mitano, jijini Mbeya, vilivyoanzishwa na Shirika la Brack, akiwaonyesha wazazi zana za kufundishia kwa vitendo, wakati wa sherehe za watoto waliohitimu mafunzo hayo, mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Walamba mikopo ya mil. 120/-

**Na Nebart Msokwa, TUKUYU**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, imetoa mikopo yenye thamani ya Sh. milioni 120 kwa vikundi 21 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika robo ya pili ya mwaka wa fedha 2019/20 ili kuendeleza shughuli za ujasiriamali.

Mikopo hiyo ilikabidhiwa kwa vikundi hivyo mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Ezekiel Mwankota, ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye shughuli hiyo.

Akitoa taarifa ya utoaji wa mikopo hiyo, Kaimu Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya hiyo, Deodatus Nenze, alisema katika robo ya kwanza walitoa mikopo yenye thamani ya Sh. milioni 90 ambayo imeanza kurejeshwa taratibu.

Kwa sasa, alisema wakijumlisha mkopo wa robo ya kwanza na ya pili ni kwamba wameshatoa mikopo yenye thamani ya Sh. milioni 210 ambazo ni sehemu ya utekelezaji wa sheria inayowataka kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya vikundi hivyo.

Nenze alisema baadhi ya vikundi vilivyokopeshwa ni vya waendesha pikipiki (bodaboda), wasindikaji wa mafuta na vyakula, vikundi vya mafundi cherehani na hata wanaopika vyakula (mama lishe).

"Hii mikopo inatokana na makusanyo yetu ya ndani na baadhi ya mapato hayo ni marejesho ya baadhi ya vikundi vilivyokwisha kunufaika na mikopo na mengine ni makusanyo ya kawaida ikiwamo ushuru wa mazao," alisema Nenze.

Alisisitiza kuwa wataendelea kutoa mikopo hiyo kama sheria inavyowataka pamoja na kufuatilia ili kuhakikisha wote waliokopa wanarejesha kwa wakati kwa ajili ya vikundi vingine kukopeshwa. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Loema Peter, aliwataka wanufaika wa mikopo hiyo kuirejesha ili na wengine wanufaike ama na wao wenyewe wanufaike kwa awamu zinazofuata.

Alisema lengo la serikali kuweka utaratibu huo ni kuhakikisha inawainua wajasiriamali wadogo kwa kurejesha mapato yanayokusanywa kwao ili waendeleze shughuli zao.

Loema alisema utaratibu huo umeelezwa vizuri kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi CCM ya Mwaka 2015 na malengo yake yameelezwa humo na kwamba mikopo hiyo haina riba kabisa.

"Lengo la halmashauri yetu ni kukopesha mikopo yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 400 ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha wa 2019/20 ambao unaishia Juni. Sasa ili tufikie huko, ni vizuri ninyi mnaokopeshwa mjitahidi kurejesha mikopo yenu," alisema Loema.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Mwankota alimpongeza mkurugenzi huyo kwa kusimamia vizuri mikopo hiyo, hivyo kuifanya wilaya kuwa miongoni mwa zile zinazotekeleza agizo hilo.

Aliwataka wananchi kuhamasika katika kulipa ushuru wa bidhaa wanazouza ili kuifanya halmashauri hiyo iongeze makusanyo na kiwango cha ukopeshaji kwa vikundi.





# Aonya anasa kwa wavuvi

**Na Peter Mkwavila, CHAMWINO**

DIWANI wa Viti Maalum Kata ya Loje wilayani Chamwino, Hilda Kadunda (CCM), amewataka wavuvi wa Bwawa la Mtera kuitumia fursa hiyo kujiongezea kipato badala ya kuendekeza anasa.

Kadunda alitoa rai hiyo alipozungumza na waandishi wa habari kijijini hapo na kuwataka wavuvi hao kutumia fursa hiyo kwa malengo ya kuongeza mitaji waliyokuwa nayo badala ya kujiingiza kwenye starehe na anasa.

Alisema wakijiepusha na matumizi mabaya ya fedha wanazopata kupitia shughuli za uvuvi, wataongeza nyenzo mbalimbali zinazotumika katika uvuvi.

"Tatizo la wavuvi walio wengi wamekuwa na matumizi makubwa ya fedha kwenye anasa na matokea yake baadhi yao hujikuta wakiwa duni kimaisha," alilalamika.

Diwani huyo pia aliwakumbusha wazazi na walezi kuhakikisha watoto wote wanaostahili kupata elimu ya msingi hadi sekondari, wanapelekwa shule, badala ya kufanyishwa kazi za nyumbani, uvuvi na kuchunga mifugo.

Alisema serikali imewaondolea wazazi na walezi mzigo mkubwa uliokuwa ukiwakwamisha watoto wengi kupata elimu kwa kufuta ada na michango shuleni.

"Baadhi ya wazazi na walezi wamekuwa hawana mwamko wa kujua kuwa elimu ndiyo mtaji pekee uliobaki kwa karne hii, kutokana walio wengi wapo tayari kuwaacha watoto hao majumbani ili kuchunga na kufanya kazi za bwawani kuvua samaki bila kujali kuwa wanawatengenezea umaskini kwenye maisha yao ya baadaye," alionya.

# Usafiri treni reli ya kati warejeshwa

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

USAFIRI wa treni kutoka Dar es salaam kwenda Kigoma, umerejeshwa baada ya kukamilika kwa matengenezo katika maeneo yaliyokuwa yamezingirwa na maji na kujaa mchanga mkoani Dodoma.

Maeneo ya reli yaliyokuwa yamejaa maji ni Kigwe wilayani Bahi na Godegode-Gulwe wilayani Mpwapwa na kusababisha kusitishwa kwa usafiri huo.

Mkuu wa Kituo cha Dodoma wa Shirika la Reli (TRC), Rose Ngauga, alisema jana kuwa mazingira ya usafiri wa treni kwa sasa yako vizuri baada ya matengenezo kukamilika.

"Kwa sasa, mambo ni mazuri kwa maana treni zinapita, tulikamilisha matengenezo jana (juzi) na tulianza kuuza tiketi baada ya matengenezo kukamilika, abiria hao wataondoka leo (jana) saa saba nchana na treni ya B17 itafika Dodoma ikitokea Dar es Salaam," alisema.

Alisema mwanzoni mwa wiki hii, TRC ilitumia zaidi ya Sh. milioni 10 kusafirisha kwa mabasi abiria na wafanyakazi 648 waliokuwa wamekwama stesheni ya Dodoma na treni ya Delux kutokana na mvua inayoendelea nchini.

Abiria hao waliokuwa wakitokea mkoani Kigoma kwenda jijini Dar es Salaam, walikwama kutokana na mvua na kusababisha reli kujaa maji na mchanga maeneo mbalimbali.

Kutokana na hali hiyo, TRC walisimamisha usafiri huo ili kupisha matengenezo katika maeneo korofi.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani, Meja Jenerali Jacob Kingu (kushoto), akizungumza na watumishi wa wizara yake, jijini Dodoma, jana. Kingu aliwataka kufanya kazi kwa ushirikiano na kujituma zaidi kwa mwaka mpya wa 2020. **PICHA: WMNN**

# Waziri ataka serikali iombewe

**Peter Mkwavila, DODOMA**

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira na Vijana), Athony Mavunde, amewaomba viongozi wa dini na waumini kuiombea serikali ya awamu ya tano ili iendelee kuongoza baada ya uchaguzi mkuu Oktoba mwaka huu.

Mavunde alitoa rai hiyo alipozungumza na viongozi mbalimbali wa umoja wa madhehebu ya dini kwenye ibada maalum ya kufunga mwaka 2019 na kukaribisha mwaka 2020, iliyoandaliwa na Umoja wa Wachungaji Hombolo kwa kushirikiana na The Global Revival Network Tanzania jijini Dodoma.

Alisema kutokana na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika uongozi wa serikali hiyo, kuna kila sababu kwa viongozi wa dini na waumini kuiombea irudi madarakani baada ya uchaguzi ili taifa liendelea zaidi kiuchumi.

"Niwaombe viongozi wangu wa dini pamoja na waumini wezangu, tuendelee kumwomba Mungu ili serikali yetu iliyopo madarakani ilirudi na kuwatumikia wananchi wake kimaendeleo zaidi, maendeleo ambayo hayatajali itikadi yoyote ya kisiasa, kidini, kirangi wala kabila na ukizingatia kuwa maendeleo hayo sasa tunayaona tena kwa vitendo," alisema. Mavunde pia aliwataka Watanzania kuendelea kuiombea amani, mshikamano, upendo na umoja wa taifa uliopo udumishwe, na kuwaombea Rais, makamu wake, waziri mkuu na viongozi wanaowasaidia katika wizara na idara mbalimbali za serikali.


"Wana Dodoma pamoja na Watanzania, kwa pamoja hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa taifa letu hili jinsi Mungu alivyotutendea kwa serikali hii ya awamu ya tano chini ya Rais wetu Dk. John Magufuli na viongozi walio chini yake.

"Yamepatikana mafanikio makubwa kwenye miradi mikubwa kama vile umeme, reli ya kisasa, kuhamishia makao makuu ya serikali Dodoma na mingine mingi," alisema.

Kiongozi wa Mtandao wa Uamsho na Maombi, Dk. Eliya Mauza, alisema viongozi wa madhehebu ya dini wanawajibika kuombea serikali na viongozi wake wanaofanikisha kuleta mabadiliko ya kimaendeleo kwa watu.

Dk. Mauza ambaye ni Askofu wa Kanisa la Endtime Harvest Dodoma, alisema viongozi wamepewa kazi ya kuiombea serikali na watendaji wake kwa mujibu wa Biblia ili kuelewa vyema jinsi wanavyotakiwa kuwajibika katika shughuli zao za kuiletea maendeleo nchi.

HABARI ZANZIBAR



# Shein ajivunia mfumo bora utoaji wa elimu

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema Zanzibar inasifika kwa kuwa na mfumo bora wa utoaji wa elimu katika ukanda wa Mashariki ya Afrika na bara lote kwa ujumla.

Akifungua Shule ya Sekondari ya Mwembeshauri Mjini Unguja, alisema Zanzibar imepata mafanikio makubwa katika sekta ya elimu, kutokana na misingi bora iliyowekwa na muasisi wa Taifa hilo, Hayati Abeid Amani Karume.

Alisema kabla ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964, elimu ilitolewa kwa malipo, hivyo watoto wa wazalendo hususan wanyonge walishindwa kupata fursa hiyo na elimu kutolewa kwa misingi ya ubaguzi kutegemea na kabila na mtu alikotoka.

Alisema kupitia Ilani ya Uchaguzi ya ASP, Karume alitangaza elimu kutolewa bure nchini kote, kama chama hicho kingeshinda na kukamata hatamu, jambo ambalo limeendelea kutekelezwa hadi leo.

Dk. Shein alisema katika awamu tofauti za uongozi, serikali imekuwa ikifanya juhudi kubwa kuendeleza sekta ya elimu kwa kuimarisha miundombinu ya elimu, ikiwamo ujenzi wa shule hadi kufikia 381 hivi sasa kati yake shule 284 zikiwa za sekondari.

Alisema ujenzi wa shule tisa mpya utaondoa kabisa tatizo la mrundikano la wanafunzi katika shule mbalimbali, akitolea mfano kwa baadhi ya shule, ambapo walimu watatu hufundisha darasa moja kwa wakati mmoja kutokana na wingi wa wanafunzi.

Aidha, alisema serikali inaendelea kufanya juhudi kubwa kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazokwaza maendeleo ya elimu nchini, ikiwamo upatikanaji wa vitabu na madawati.

Dk. Shein alisema changamoto ya upungufu wa walimu wa sayansi imeanza kupatiwa ufumbuzi kwa msaada wadau.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Riziki Pembe Juma, alisema ujenzi wa shule hiyo ya ghorofa mbili una lengo la kuondokana na ufinyu wa nafasi.

Alisema majengo hayo yatawasaidia sana walimu kufundisha katika mazingira mazuri, na wanafunzi kupokea vyema wanachofundishwa, hivyo kuwa katika nafasi nzuri zaidi katika masomo.

Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Dk. Idriss Muslih Hijja, alisema shule mpya ya Mwembeshauri ni miongoni mwa shule tisa zilizokamilika ujenzi wake Unguja na Pemba.

Alisema ujenzi huo umetekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wahisani Opec Fund for International Development (OFID) kupitia mradi wa Zanzibar Third Education Project (ZATEP).

Alieleza kuwa ujenzi wa shule hizo unaendana na utekelezaji wa Ilani ya CCM, ukiwa umegharimu Sh. bilioni 26.3, kati ya hizo Sh. bilioni 23.4 ni mkopo kutoka Opec Fund na Sh. bilioni 2.9 ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.



Waziri wa Afya Zanzibar, Hamad Rashid Mohamed, akikata utepe kuashiria ufunguzi wa jengo jipya la wazazi la hospitali binafsi ya Mayda Health Charitable Foundation, iliyopo Fuoni Ijitimai, Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mvuvi aokotwa baharini amekufa

**Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MVUVI aliyekuwa amepotea baharini kwa siku saba, amekutwa amefariki dunia, huku mwili ukielea baharini Micheweni, Pemba.

Mvuvi huyo aliyetambulika kwa jina la Ali Hassan Simba (27), alipotea baharini tokea Desemba 30, mwaka jana akiwa katika shughuli zake za uvuvi.

Akizungumza na wananchi na wavuvi wa Wilaya ya Micheweni, Mkuu wa Wilaya hiyo, Salama Mbaruku Khatibu, aliwataka wavuvi kuwa na utaratibu wa kufuatana wakiwa bahari katika shughuli zao za uvuvi ili kusaidiana yanapotokea maafa.

Alisema watakapokuwa na utaratibu huo wanaweza kuondokana na matukio ya kila siku kusikia kuna mvuvi amekufa baharini.

"Kitendo cha kuwa peke yako baharini ni hatari, maana unapokutwa na tatizo hukosa msaada wa haraka," alisema.

Naye Daktari Dhamana wa Hospitali ya Micheweni, Rashid Daud Mkasaha, alisema kifo cha mvuvi huyo kimetokana na kunywa maji mengi, na kushindwa kupata msaada baada ya kuzidiwa na maji baharini.

Wanafamilia wa mvuvi huyo waliishukuru serikali kutokana na ushirikiano na kuhakikisha mwili wa ndugu yao unapatikana.

**"Kitendo cha kuwa peke yako baharini ni hatari, maana unapokutwa na tatizo hukosa msaada wa haraka," alisema.**

# Wauguzi, wakunga wafundwa huduma bora

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Afya wa Zanzibar, Hamad Rashid Mohamed, amewataka wauguzi na wakunga kutoa huduma zenye kiwango ili zinazotolewa zisilalamikiwe na wananchi.

Aliyasema hayo wakati akizindua kituo kipya cha afya ya wazazi, (Mayda Health Charitable Foundation) huko Fuoni Ijitimai Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja.

Alisema kufunguliwa jengo la wazazi kutasaidia matunzo mazuri kinamama kwa kupima maendeleo ya ujauzito pamoja na kujifungua katika kituo hicho.

Waziri huyo aliwataka wauguzi na wakunga watoe huduma nzuri na kuwa na kauli laini ambayo itawaridhisha wagonjwa ili yasijitokeze malalamiko.

Hamad aliwapongeza wafanyakazi wa kituo hicho kuwa na ujuzi wa kazi kwa kuvitumia vifaa vya mashine za kisasa kwani bila ya taaluma vifaa hivyo vitakosa kufanyiwa kazi.

Aidha, alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina lengo la kuhakikisha wananchi wote wanapata huduma bora za afya, hivyo alizitaka sekta binafsi kushirikiana na serikali wanapokuwa na changamoto yoyote katika vituo vyao.

Alisema ushirikiano huo utawezesha kufikiwa na mkurugenzi wa kinga kusaidia kuzitatua changamoto hizo na kuwezesha utoaji huduma bora hasa kwa wajawazito na watoto.

Alieleza kuwa vifo vya wajawazito na watoto vinatokana na ukosefu wa mahudhurio ya kliniki ipasavyo kwa kutopatiwa chanjo za kujikinga na maradhi.

Alisema asilimia 60 tu ya wajawazito ndio hujifungulia katika vituo vya afya, baadhi yao hujifungulia nyumbani, jambo ambalo linachangia kupata matatizo ambayo wakifikishwa hospitali uwezekeno wa kuokoa maisha ya mama na mtoto ni mdogo.

"Kinamama wanaojifungulia majumbani wakipata matatizo hukaa nayo muda mrefu wakifikishwa hospitali uwezekana wa kuokoa mama na mtoto huwa ni mdogo," alisema Waziri wa Afya.

Aliwataka wanafamilia kukubaliana kupanga mpangilio wa uzazi ambao utasaidia kumlea mtoto katika hali nzuri yenye furaha na upendo, na kwamba uzazi usio na mpango hudhoofisha afya ya mama na mtoto.

Naye daktari mwenye dhamana, Maulid Abdalla Khamis, alisema lengo la kuanzishwa kwa jengo la wazazi ni kuisaidia serikali kutokana na wingi wa wajawazito na watoto katika Hospitali Kuu ya Mnazimmoja, hivyo kuchangia wagonjwa kutohudumiwa vizuri.

Alieleza kuwa utaratibu wa utoaji wa huduma katika jengo hilo ni kwa saa 24, jambo ambalo litasaidia kuwahudumia kinamama wanaohitaji kujifungua kwa muda wote .

Daktari wa hospitali hiyo, Kheir Abdallah, alisema kuwa licha ya sekta binafsi kuiunga mkono serikali kuna changamoto zinazojitokeza kwa kukosa vyandarua kwa wajawazito na watoto pamoja na kadi za mfumo wa uzazi wa mpango.

Alieleza hospitali hiyo imekusudia kuongeza huduma bora kwa wananchi katika vitengo vya magonjwa mbalimbali ili kuondoa msongamano katika vituo vingine.

# Wapewa siri ya kudumisha ndoa

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

WANAFUNZI 41 waliohitimu mafunzo ya elimu ya ndoa ya awamu ya tatu kisiwani Pemba, wametakiwa kuyatumia kwa vitendo mafunzo hayo, ili kudumisha na kuleta utulivu katika ndoa zao.

Akikabidhi vyeti kwa wahitimu hao huko Gombani Chakechake, Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kaaby, alisema elimu ya ndoa ni muhimu kwa wanandoa na wanaotarajia kufunga ndoa, kwani mambo yasiofaa yatapungua na kusaidia kuishi namna bora katika ndoa.

Alisema katika ndoa zao wazingatie mafunzo waliyopatiwa, ili kudumisha ndoa na kuweka utulivu, jambo ambalo litasaidia kuishi maisha mema.

"Hali ni ngumu kimaisha, kila siku zinapokwenda mbele talaka hutolewa kiholela, hivyo mafunzo hayo yatasaidia wanandoa na wanaotarajia kufunga ndoa, kuzidumisha ndoa zao," alisema Mufti.

Alifahamisha lengo la kutoa mafunzo hao ni kutengeneza nyumba nzuri ili kupata matunda bora yatakayoinufaisha jamii na Taifa kwa ujumla.

"Katika ndoa zenu mzingatie haya mliyofundishwa kwenye mafunzo asije akawapitia shetani na kuwaharibia kwa hadaa za watu wa nje," alisema.

Aidha, Mufti aliwataka wazazi na walezi kuwaoza watoto wao wa kike, waume wenye kufuata maadili ya dini ya kiislamu, sambamba na kuwapa waume wanaowapenda ili kuepusha talaka za kiholela.

"Kama ilivyo kwa mwanamme kuchagua mke bora, na wanawake nao vile vile muwachagulie mume bora, sio kukurupuka tu na kumuoza mwanaume asiyefaa, hiyo itasababisha migogoro katika ndoa na hatimae talaka," alieleza.

Akitoa neno la shukrani muhitimu wa mafunzo hayo, Sauda Hamad Salum aliishukuru ofisi ya Mufti kwa kuwapatia mafunzo hayo ya wiki kumi na kusema kuwa yatawasaidia kudumisha ndoa zao.

"Mafunzo haya tuliyoyapata ni muhimu kwa wanandoa na wanaotarajia kufunga ndoa, kwani yanaweza kuwaepusha vijana kujiingiza katika maovu kama ulevi, wizi, ubakaji na ulawiti," alisema.

Aidha, aliiomba ofisi ya Mufti kutoa mafunzo hayo kwa kila wilaya ili kupata wanafunzi wengi na kupata vijana bora ambao watafuta maadili mema.

"Watu wengi wanayahitaji haya mafunzo, ingawa wanashindwa kutokana na masafa yaliyopo hasa vijijini, kutokana na hali ya maisha ilivyo katika kisiwa cha Pemba wananchi hushindwa kujiunga na hata sisi tuliojiunga wakati mwengine mtu anakosa darasa kwa kushindwa nauli," alifafanua.

Naibu Mufti Zanzibar, Mahmoud Mussa, alieleza pamoja na matatizo ya ufinyu wa bajeti, watatumia nguvu nyingi kuwafuata wananchi kuwapatia elimu hiyo, ili kufanikiwa.

"Tunafanya kila juhudi kuona tunapunguza masafa ili na wengine wanufaike na awamu hii ya nne tunatarajia kutoa elimu hii Mkanyageni Wilaya ya Mkoani kutokana na maombi ya watu wasiopungua 70 kuhitaji wapewe mafunzo hayo," alieleza.

Naye Msaidizi Katibu Mufti Pemba, Abrahman Abdalla Naaman, alisema kila siku zinapokwenda mbele maombi yanaongezeka ingawa huomba wasogezewe angalau katika Wilaya, ili kupunguza gharama za usafiri.

Wahitimu hao walishukuru kupatiwa mafunzo hayo na kusema watajitahidi katika kuhakikisha wanawafundisha wenza wao pamoja na jamii kwa ujumla.

"Haya mafunzo raha yake hasa aje mke na mume, lakini na hivi pia sio mbaya tutawafundisha na wanajamii kwa ujumla, ili tudumishe ndoa zetu katika jamii," alieleza.

# Mtuhumiwa wa 'Tereza' kortini kesi ya kujeruhi

**Na Joctan Ngelly, KIGOMA**

MKAZI wa Gungu Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Joseph Richard (25), anayedaiwa kuwa mmoja wa kikundi cha kihalifu cha 'Tereza', amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya Mkoa wa Kigoma kwa kosa la kumshambulia Mwamini Hussein kwa kumkata na panga sehemu ya kichwani na kwenye mguu wa kushoto na kumsababishia majeraha.

Mshtakiwa huyo alifikishwa mahakamani na kupandishwa kizimbani mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Eva Mushi.

Hata hivyo, baada ya kusomesha shtaka, alikana na yuko mahabusu katika Gereza la Bangwe kwa kukosa mdhamini.

Hakimu Mushi aliyataja masharti ya dhamana kwa mshtakiwa huyo kuwa na mdhamini mmoja mwenye barua ya utambulisho kutoka kwa ofisa mtendaji wa kata na mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni 2.

Aidha, Hakimu Mushi alisema kutokana na mshtakiwa huyo kukosa mdhamini, atakuwa mahabusu katika Gereza la Bangwe wakati kesi yake ikiendelea.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Raymond Kimbe, alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa huyo maelezo ya awali.

Hakimu Mushi alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi leo kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa huyo maelezo ya awali.

Akisoma hati ya mashtaka, Kimbe alidai kuwa Agosti 8, mwaka 2019, majira ya usiku eneo la Muongwe Mkoa wa Kigoma, mshtakiwa alimshambulia Mwamini Hussein kwa kumkata na panga sehemu za kichwani na kwenye mguu wa kushoto karibu na goti na kumsababishia majeraha mwilini mwake.



Mafundi wakifanya maandalizi ya kupaua choo cha Shule ya Sekondari Busamaba, iliyopo katika Kata ya Busambara, Musoma Vijijini, mkoani Mara juzi, ili kitumiwe na wanafunzi wanaojiandaa kuanza kidato cha kwanza mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wapanda Mlima Balili kutangaza utalii wa ndani

**Na Ahmed Makongo, BUNDA**

KATIKA kuhamasisha utalii wa ndani nchini, watu wa rika mbalimbali zaidi ya 100 wakiwamo skauti kutoka Halmashauri ya Mji wa Bunda mkoani Mara, wamepanda hadi kwenye kilele cha Mlima Balili.

Enzi za uhai wake Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, alipanda mti wa mfano kwa ajili ya kuhamasisha uhifadhi wa mazingira katika mlima huo na nchi kwa ujumla.

Wakipanda mlima huo jana, wakiwamo watoto wadogo wenye umri wa kati ya miaka sita hadi 13, wakiongozwa na mgeni rasmi katika utalii wa ndani, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Bunda, Abraham Mayaya, walisema wanahamasisha utalii wa ndani, ili wananchi wengi zaidi waweze kujenga tabia hiyo.

Wananchi hao walitembea zaidi ya kilomita saba na kutumia muda wa zaidi ya saa mbili kufika kileleni.

Akizungumzia umuhimu wa utalii wa ndani Mayaya alisema kwa kutambua manufaa yanayotokana na utalii, halmashauri hiyo iliamua kutoa eneo bure kwa ajili ya kujenga ofisi za Shirika la Utalii Tanzania (Tanapa) makao makuu kanda ya magharibi, ambayo yatakuwa Wilaya ya Bunda mkoani Mara.

"Sisi Halmashauri ya Wilaya ya Bunda kwa kutambua umuhimu wa uhifadhi na manufaa yanotokana na utalii tuliamua kutoa eneo bure kwa ajili ya kujenga ofisi za Tanapa makao makuu Kanda ya Magharibi zitakazo kuwa eneo la Balili," alisema.

Mayaya aliwaasa wananchi katika halmashauri hiyo kujenga tabia ya kufanya utalii wa ndani katika maeneo mbalimbali ya uhifadhi pamoja na kufanyabiashara ya kiutalii, hali ambayo itawafanya wajiongezee kipato na kujiinua kiuchumi kama walivyo wananchi wa mikoa ya kaskazini wanaotumia fursa ya utalii ipasavyo.

Mwenyekiti wa kamati ya asasi moja isiyokuwa ya kiserikali ya NCT Twende Kutalii, Albert Chenza, ambayo ndiyo inayohamasisha utalii huo wa ndani kwa kushirikiana na redio moja ya kijamii ya Mazingira FM iliyoko wilayani Bunda, alisema kuwa lengo la kupanda Mlima Balili ni kuhamasisha jamii iweze kufanya utalii wa ndani.

"Lengo la kupanda mlima huo ni kwa ajili ya kuhamasisha wananchi kujenga tabia ya kufanya utalii wa ndani, lakini ni kwa ajili ya kuutangaza kwa sababu mlima huu unazo fursa nyingi za kiutalii," alisema.

Chenza alisema kuwa Mlima Balili unazo fursa nyingi za kiutalii, hivyo wananchi wanapaswa kuutembelea badala ya kuachia wageni kutoka nje ya nchi tu, huku akishauri pia halmashauri ya mji wa Bunda kujenga kituo cha utalii ambacho kitakuwa na bidhaa mbalimbali za kuwauzia watalii.

Meneja wa hoteli moja ya kitalii ijulikanayo kwa jina la Balili Mountain Resort & Campsite, iliyobeba jukumu la kuhifadhi na kuulinda mlima huo, Isdory Rupia, alisema wamekuwa waakipata wageni kutoka nchi mbalimbali wakiwamo wazungu na Wahindi, ambao wamekuwa wakipanda hadi kwenye kilele cha mlima huo.

Roza Sulusi (62), Joseph Alstabus (13) na Guin Muro (30), wa wakazi wa wilayani hapa, ambao ni baadhi ya waliofanya utalii huo wa ndani, walitoa wito kwa Watanzania wengine kuiga mfano huo badala ya kusubiri watu kutoka nje ya nchi tu.

Mlima Balili ulioko katika Halmashauri ya Mji wa Bunda, una vivutio vingi wakiwamo wanyama na ndege, lakini ukifika kileleni utapata fursa ya kutazama maadhari nzuri ya mlima huo, Ziwa Victoria, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na eneo lote la mji wa Bunda.

## Shambulizi Al-Shabab laua Wamarekani 3

**NAIROBI,** Kenya

IDADI ya vifo kutokana na shambulio la Al Shabab dhidi ya kambi ya jeshi Mashariki mwa Kenya imeongezeka.

Marekani kupitia makao yake ya kijeshi barani Afrika (Africom) ilieleza kuwa shambulio dhidi ya kambi ya Simba liligharimu maisha ya raia watatu kutoka Marekani.

Ilieleza kuwa askari mmoja na wafanyakazi wawili wa Wizara ya Ulinzi walifariki huku wengine wawili wakijeruhiwa lakini wanaendelea vizuri.

Juzi, mamlaka nchini Kenya ilisema kuwa magaidi wanne waliuawa na washukiwa watano walikamatwa wakihusishwa na tukio hilo.

Wakati wa shambulio hilo, wanamgambo wa Al Shabab walidai kuwa walitekeleza shambulio kubwa kwa upande wa askari wa Marekani na Kenya walioko kwenye kambi hiyo. **RFI**

# Mchungaji na mke wake wauana wakigombea kanisa

**NAIROBI,** Kenya

MCHUNGAJI wa kanisa moja mjini Mombasa pwani ya Kenya amejiua kwa kujikata koo muda mfupi baada ya kumchoma kisu mke wake wakati wa ibada ya Jumapili.

Mchungaji Elisha Misiko (55), alikuwa mhubiri wa kanisa hilo katika mtaa wa Bamburi akishirikiana na mkewe Ann Mghoi.

Jamaa, marafiki na waumini wa kanisa hilo walilieleza gazeti la Nation la Kenya kuwa kisa hicho kilitokana na mzozo wa muda mrefu wa kifamilia kuhusu umiliki wa kanisa hilo.

"Watu hawa wamekuwa wakiendesha kanisa hili kwa zaidi ya miaka nane lakini walitofautiana miezi michache iliyopita, alisema Mtengo Amuri ambaye ni mzee wa mtaa lililopo kanisa hilo.

Inaelezwa kuwa mchungaji huyo alimlaumu mkewe, Ann Mghoi kwa kupanga njama ya kumfukuza kutoka katika kanisa hilo ambalo anadai kulianzisha.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari nchini Kenya, waumini walidai kuwa Mchungaji Misiko aliingia kanisani majira ya saa tatu asubuhi na kukaa viti vya mbele karibu na mke wake.

**Kamanda wa Polisi Wilaya, Julius Kiragu, alithibitisha kutokea kwa kisa hicho na kuongeza kuwa mwanamke huyo alichomwa kisu mgongoni, mikononi na tumboni.**

Walisema wakati ibada ikiendelea, Mchungaji Misiko aliamka ghafla kwenye kiti chake na kumshambulia mke wake kwa visu viwili ambavyo alikuwa ameficha ndani ya koti lake.

Walieleza kuwa Mchungaji Misiko alimchoma kisu mara kadhaa mkewe kabla ya waumini waliokumbwa na mshangao kuingilia kati kumwokoa na kumkimbiza katika hospitali kuu pwani, ambako alifariki wakati akipata matibabu.

Walieleza kuwa wakati wa purukushani ya kumuokoa Mghoi ilipokuwa ikiendelea na kwamba Mchungaji Misiko naye alijiua.

Rafiki wa karibu wa familia hiyo, Janet Tole alisema kuwa wanandoa hao walizozana kwa muda mrefu na kutengana kwa miezi michache iliyopita.

Alisema kuwa Mchungaji Misiko, aliwahi kumtishia maisha mkewe mara kadhaa, madai ambayo yalithibitishwa na kipande cha karatasi ambacho kiliandikwa na mchungaji huyo kabla ya kutekeleza mauaji hayo.

Mmoja wa mashuhuda wa tukio hilo, Tole alieleza kuwa mkewe alimzuia kuona watoto wao walipotengana.

Muumini mwingine alieleza kuwa Mchungaji Misiko na mke wake walipigana ndani ya nyumba yao kabla ya kuanza kwa ibada.

Kamanda wa Polisi Wilaya, Julius Kiragu, alithibitisha kutokea kwa kisa hicho na kuongeza kuwa mwanamke huyo alichomwa kisu mgongoni, mikononi na tumboni.

Kiragu alisema kuwa, Mchungaji Misiko alipanga tukio hilo kwa muda mrefu, kama ilivyobainika katika kipande cha karatasi alichoandika kabla ya kujiua ambapo alimlaumu mkewe kwa kumdhalilisha.

Kamanda huyo wa polisi aliripoti kuwa mchungaji huyo alifariki ndani ya kanisa hilo na kwamba mwili wake umepelekwa katika chumba cha kuhifadhi maiti cha Hospitali Kuu ya Mkoa wa Pwani. **BBC**



Maelfu ya wananchi wa Iran waliojitokeza katika mji mkuu wa nchi hiyo, Baghdad, kuuaga mwili wa aliyekuwa Kamanda wa Jeshi la nchi hiyo, Qasem Soleimani. **PICHA: REUTERS**

# Polisi wafyatua risasi, wamkamata Bobi Wine

**KAMPALA,** Uganda

JESHI la Polisi jijini Kampala, Uganda, limelazimika kufyatua risasi na mabomu ya machozi kuwasambaratisha wafuasi wanaomuunga mkono Mbunge wa Jimbo la Kyandondo, Robert Kyagulanyi maarufu Bobi Wine.

Mbunge huyo alikamatwa na polisi muda mfupi kabla ya kufanyika kwa mkutano wake wa kwanza wa kutafuta kuungwa mkono katika Wilaya ya Wakiso.

Bobi Wine alikamatwa pamoja na wabunge wengine wakiwamo Asuman Basalirwa, Latif Ssebagala, Waiswa Mufumbira na mwenyekiti wa baraza la Kasangati, kwa sasa wanashikiliwa katika kituo cha polisi cha Kasangati.

Gazeti la The Observer lilimnukuu Basalirwa akisema kuwa walikuwa wakiendesha gari la Kyagulanyi kabla ya polisi kuwazuia katika eneo la Kasangati na kuwapeleka katika kituo cha polisi.

Kyagulanyi alikuwa akitarajiwa kuzindua mikutano ya mashauriano kuhusu malengo ya urais kwa uchaguzi mkuu ujao.

Taarifa iliyotolewa na Jeshi la Polisi ilieleza kuwa walilazimika kuuzuia mkutano huo kwa sababu ulipangwa kufanyika kwenye eneo la wazi, wakati mikutano ya namna hiyo hufanyika ndani ili kutoingilia shughuli za watu wengine.

Aidha, wameeleza kuwa hakukuwa na vyoo vya kutosha kwa ajili ya wageni waliokuwa wakitarajiwa.

Mbunge huyo aliiandikia tume ya uchaguzi kabla ya sikukuu ya Krismasi akieleza nia yake ya kufanya mkutano kitaifa kuhusu nia ya kuwania urais.

Licha ya kuruhusiwa kufanya mkutano, lakini tume hiyo ilieleza kuwa hakutimiza vigezo vingine kama vinavyoelezwa kwenye sheria.

Bobi Wine ameeleza nia yake ya kuwania urais dhidi ya Rais Yoweri Museveni ambaye amekuwa madarakani tangu mwaka 1986.

Gazeti la Daily Monitor lilimnukuu Wine siku ya Ijumaa akisema kuwa sheria ya uchaguzi inampa fursa ya kuzungumza na watu kuhusu kama watamuunga mkono katika mipango yake ya kuwa mgombea kwenye uchaguzi ujao wa urais mwaka 2021. **BBC**

# HABARI PICHA



Kaimu Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Kimadini wa Simanjiro, Castro Maduwa, akizungumza juu ya kutenguliwa wajumbe wawili wa kamati ya usuluhishi Kitalu B Opec madini ya Tanzanite, Mji mdogo wa Mirerani jana. **PICHA: GIFT THADEY**



Mbunge wa Jimbo la Ilala, Mussa Zungu (katikati), akikagua Soko la Samaki Feri, Kata ya Kivukoni, jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mwenyekiti wa CCM wa kata hiyo, Sharik Choughule. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mchuuzi wa biashara ya vitunguu akimshawishi mteja wake, kununua bidhaa hiyo, katika eneo la Uhindini, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Watalii wa ndani kutoka Wilaya ya Bunda, mkoani Mara, wakiwa wamekaa juu ya jiwe katika Mlima wa Balili, wakiangalia mandhari ya Mji wa Bunda jana. **PICHA: AHMED MAKONGO**



Watoto wanaoanza darasa la kwanza msimu huu katika Shule ya Msingi Kitunda Kivule, jijini Dar es Salaam, wakiwa na wazazi wao shuleni hapo, jana, wakisubiri kusajiliwa. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro (kushoto), akimhoji mhudumu wa ofisi ya Nida, Wilson Laiser (kulia), katika eneo la Halmashauri ya Arusha jana, kuhusiana na tukio la kuibiwa kwa kompyuta na kamera za Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). **PICHA: WOINDE SHIZZA**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA /MASHAMBA

**Viwanja vinauzwa** Kibaha Misugusugu. Ukubwa ni mita 20 kwa 20 (400m2). Bei ni 2,000,000/- Milioni mbili tuu. (5,000/=1m2). Unaweza kulipa kwa awamu ndani ya miezi mine. Huduma zote zipo. Kwa mawasiliano: 0714 090009 / 0767 090008. Vimepimwa.

### MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MKOPO WA HARAKA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITD (EFL).** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumalizia tenda etc. Kwa maelezo zaidi piga 0758 112 332. Karibu EFL.


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0782253676


### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

BEATRICE BONIFACE SENNI, ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI NO.T 970 AST ILIYOSAJILIWA KWA JINA LA INNOCENT B. MAKOMBA.

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU NAYE. AU APIGE SIMU 0769 496541.

TAARIFA YA POLISI: NZ/RB/5242/2019.

115574702

### CHETI KIMEPOTEA



**KUNDAEL ANDASON** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0125-0097 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa Mwaka 1994 katika shule ya Sekondari LYAMUNGO.
Cheti kilipotelea Bagamoyo. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kwenye kituo cha polisi kilicho karibu.
Taarifa ya polisi: PWA/BAG/RB/575381/2019.

115574602


Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la

Nipashe kila siku

NJOO

UTANGAZE BIDHAA

YAKO

KWA BEI NAFUU


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

### TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMATANO tarehe 8/01/2020** kampuni ya **FAMARI INVESTMENT** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM kuelekea TUNDUMA,** gari hilo lenye namba za usajili:
   T 248 DPS/ T 379 AQB

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 16 |
| Upana | - | mita | 3.00 |
| Kimo | - | mita | 5.2 |

3. Njia itakayotumika: **DAR ES SALAAM hadi TUNDUMA kupitia VIGWAZA, MAKAMBAKO**

Gari zitasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa **12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)**

215574302

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

### TANGAZO

1. Ndugu wananchi mn4. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMATANO tarehe 08/01/2020** kampuni ya **FAMARI INVESTMENT** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM kuelekea TUNDUMA,** gari hilo lenye namba za usajili:
   **T 247 DPS/ T 992 ATV**

5. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 16 |
| Upana | - | mita | 3.00 |
| Kimo | - | mita | 5.2 |

6. Njia itakayotumika: **DAR ES SALAAM hadi TUNDUMA** kupitia **VIGWAZA, MAKAMBAKO**
   Gari zitasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

215574302

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.


*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila

Nipash



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# KIWANGO CHA HUDSON-ODOI CHAMFURAHISHA LAMPARD




**LONDON,** England

CALLUM Hudson-Odoi alicheza kwa kiwango bora na kuisaidia Chelsea kupata ushindi dhidi ya Nottingham Forest kwenye mchezo wa Kombe la FA, na Frank Lampard hana shaka kwamba mengi yanakuja kutoka kwa mchezaji huyo.

Chelsea iliifunga Forest mabao 2-0 kwenye dimba la Stamford Bridge Jumapili, huku Hudson-Odoi akifunga bao la kwanza kabla ya Ross Barkley naye pia kufunga.

Lampard alisema kwamba, anatarajia mengi zaidi kutoka kwa winga huyo mwenye umri wa miaka 19, ambaye amerudi baada ya kuwa nje ya dimba kwa miezi mitano kutokana na majeruhi.

Na Lampard alionyesha kufurahishwa na kiwango cha Hudson-Odoi na kusema kwamba anaamini mengi zaidi yanakuja kutoka kwake.

"Alinionyesha kiwango kizuri. Nilifurahia kumuona akiwa vizuri uwajani, na kwa uhakika alicheza kwa kiwango cha kuvutia zaidi. Alifunga bao zuri," alisema Lampard.

"Imekuwa ni miezi mizuri 12 kwa upande wake na kwa kuwa bado kijana, naamini atafanya makubwa zaidi kwa siku za usoni. "Mwaka jana kila mmoja alikuwa akimzungumzia yeye kwa sababu tofauti. Alipata majeruhi, amerudi mapema na alionekana kuwa ana njaa kali na mafanikio."

# Mourinho: Hakuna wa kuziba pengo la Harry Kane

**LONDON,** England

JOSE Mourinho amesema si Lucas Moura au Son Heung-Min mwenye uwezo wa kuziba pengo la mshambuliaji, Harry Kane baada ya kushuhudia kikosi chake cha Tottenham kikitoka sare ya 1-1 dhidi ya Middlesbrough katika mchezo wa Kombe la FA.

Lucas alifunga kwa kichwa kipindi cha pili kusawazisha kwenye mchezo huo uliopigwa kwenye dimba la Riverside, baada ya Ashley Fletcher kuiweka mbele Middlesbrough kwenye mchezo ambao ulimuacha Mourinho akiwa "amechanganyikiwa".

Tottenham haijapata ushindi kwenye mechi zake tatu zilizopita kwenye mashindano yote na Mourinho alisema kumia kwa Kane, Tanguy NDombele, Hugo Lloris na Danny Rose kumeipa majanga klabu hiyo.

Baada ya kuanza mchezo na Son akiwa mshambuliaji pekee na baadaye kumpandisha Lucas mbele, Mourinho aliwaambia waandishi wa habari: "Hawa ndio tulio nao. Vijana walifanya kile wanachoweza.

"Huwezi kuwategemea Lucas au Son kuziba pengo la Harry Kane."

"Tulibadilisha vitu na tulijihatarisha. Timu yetu kwa dakika 30 zilizopita hatukuwa hata na mchezaji wa kiungo," alisema Mourinho, akielezea uamuzi wake wa kuwapanga Harry Winks na Ryan Sessegnon pamoja na Giovani Lo Celso na Erik Lamela.





# Bayern yatarajia Boateng kubaki

**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA wa muda wa Bayern Munich, Hansi Flick, anatarajia Jerome Boateng kubakia klabuni hapo licha ya kuhusishwa na kutakiwa kule Arsenal.

Boateng mwenye umri wa miaka 31, amekuwa na klabu hiyo tangu alipojiunga nayo akitokea Manchester City mwaka 2011 na alikuwa chaguo la kwanza kwa kipindi kirefu.

Lakini matatizo ya kutokuwa fiti yalimwandama msimu wa 2015-16 na hajacheza mechi zaidi ya 20 za Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, kwa msimu mmoja.

Msimu huu Boateng amecheza mechi tisa tu kati ya 17, huku Bayern ikiwatumia zaidi wachezaji vijana na Arsenal wameripotiwa kuhitaji huduma yake wakati huu wakitaka kuimarisha safu yao ya ulinzi.

Hata hivyo, Flick amebainisha kwamba anatarajia beki huyo atabaki.

"Jerome ni mchezaji wa Bayern Munich na sijihusishi na uvumi, na hivyo ndio nimekuwa nikifanya kwa miaka kadhaa," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Jerome amerudi kwenye mazoezi na anajiandaa baada ya likizo. Hivyo, sifikiri sana kuhusu uvumi uliopo."



# KIWANGO CHA HUDSON-ODOI CHAMFURAHISHA LAMPARD

**LONDON,** England

CALLUM Hudson-Odoi alicheza kwa kiwango bora na kuisaidia Chelsea kupata ushindi dhidi ya Nottingham Forest kwenye mchezo wa Kombe la FA, na Frank Lampard hana shaka kwamba mengi yanakuja kutoka kwa mchezaji huyo.

Chelsea iliifunga Forest mabao 2-0 kwenye dimba la Stamford Bridge Jumapili, huku Hudson-Odoi akifunga bao la kwanza kabla ya Ross Barkley naye pia kufunga.

Lampard alisema kwamba, anatarajia mengi zaidi kutoka kwa winga huyo mwenye umri wa miaka 19, ambaye amerudi baada ya kuwa nje ya dimba kwa miezi mitano kutokana na majeruhi.

Na Lampard alionyesha kufurahishwa na kiwango cha Hudson-Odoi na kusema kwamba anaamini mengi zaidi yanakuja kutoka kwake.

"Alinionyesha kiwango kizuri. Nilifurahia kumuona akiwa vizuri uwajani, na kwa uhakika alicheza kwa kiwango cha kuvutia zaidi. Alifunga bao zuri," alisema Lampard.

"Imekuwa ni miezi mizuri 12 kwa upande wake na kwa kuwa bado kijana, naamini atafanya makubwa zaidi kwa siku za usoni. "Mwaka jana kila mmoja alikuwa akimzungumzia yeye kwa sababu tofauti. Alipata majeruhi, amerudi mapema na alionekana kuwa ana njaa kali na mafanikio."

# Mourinho: Hakuna wa kuziba pengo la Harry Kane

**LONDON,** England

JOSE Mourinho amesema si Lucas Moura au Son Heung-Min mwenye uwezo wa kuziba pengo la mshambuliaji, Harry Kane baada ya kushuhudia kikosi chake cha Tottenham kikitoka sare ya 1-1 dhidi ya Middlesbrough katika mchezo wa Kombe la FA.

Lucas alifunga kwa kichwa kipindi cha pili kusawazisha kwenye mchezo huo uliopigwa kwenye dimba la Riverside, baada ya Ashley Fletcher kuiweka mbele Middlesbrough kwenye mchezo ambao ulimuacha Mourinho akiwa "amechanganyikiwa".


Tottenham haijapata ushindi kwenye mechi zake tatu zilizopita kwenye mashindano yote na Mourinho alisema kuumia kwa Kane, Tanguy NDombele, Hugo Lloris na Danny Rose kumeipa majanga klabu hiyo.

Baada ya kuanza mchezo na Son akiwa mshambuliaji pekee na baadaye kumpandisha Lucas mbele, Mourinho aliwaambia waandishi wa habari: "Hawa ndio tulio nao. Vijana walifanya kile wanachoweza.

"Huwezi kuwategemea Lucas au Son kuziba pengo la Harry Kane."

"Tulibadilisha vitu na tulijihatarisha. Timu yetu kwa dakika 30 zilizopita hatukuwa hata na mchezaji wa kiungo," alisema Mourinho, akielezea uamuzi wake wa kuwapanga Harry Winks na Ryan Sessegnon pamoja na Giovani Lo Celso na Erik Lamela.





# Bayern yatarajia Boateng kubaki

**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA wa muda wa Bayern Munich, Hansi Flick, anatarajia Jerome Boateng kubakia klabuni hapo licha ya kuhusishwa na kutakiwa kule Arsenal.

Boateng mwenye umri wa miaka 31, amekuwa na klabu hiyo tangu alipojiunga nayo akitokea Manchester City mwaka 2011 na alikuwa chaguo la kwanza kwa kipindi kirefu.

Lakini matatizo ya kutokuwa fiti yalimwandama msimu wa 2015-16 na hajacheza mechi zaidi ya 20 za Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, kwa msimu mmoja.

Msimu huu Boateng amecheza mechi tisa tu kati ya 17, huku Bayern ikiwatumia zaidi wachezaji vijana na Arsenal wameripotiwa kuhitaji huduma yake wakati huu wakitaka kuimarisha safu yao ya ulinzi.

Hata hivyo, Flick amebainisha kwamba anatarajia beki huyo atabaki.

"Jerome ni mchezaji wa Bayern Munich na sijihusishi na uvumi, na hivyo ndio nimekuwa nikifanya kwa miaka kadhaa," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Jerome amerudi kwenye mazoezi na anajiandaa baada ya likizo. Hivyo, sifikiri sana kuhusu uvumi uliopo."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MADRID YAJIANDAA KUMNASA WERNER

●●● Ni mmoja wa washambuliaji nyota katika Bundesliga ambaye anawaniwa na ...

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid imeanza maandalizi ya kuimarisha kikosi chake kwa kumsajili mshambuliaji wa RB Leipzig, Timo Werner, katika kipindi cha majira ya joto, taarifa mbalimbali zinaeleza.

**Vigogo hao wa Ligi Kuu Hispania, wanatajwa kujiandaa kutoa dau la pauni milioni 68 ili kumnasa nyota huyo, kiasi ambacho ni cha kushtusha.**

Wakati klabu nyingi zikiwa zinatoa 'macho' kuimarisha vikosi vyake kwa kusajili wachezaji wapya katika kipindi cha majira ya baridi ambacho ni mzunguko wa pili wa msimu, lakini kwa upande wa Madrid iliyoko chini ya Mfaransa, Zinedine Zidane, yenyewe inaangalia mipango ya mbele zaidi.

Gazeti la El Desmarque la Hispania limeandika kuwa, Real Madrid inajiandaa kufanya usajili wa nguvu kwa kumnasa mchezaji huyo ambaye ni mmoja wa mastaa wa Ligi Kuu Ujerumani maarufu Bundesliga na wa klabu ya Leipzig, Werner.

Mshambuliaji huyo pia alikuwa anahusishwa na mipango ya kutakiwa na Liverpool pamoja na Chelsea, lakini sasa inaonekana kuwa Real Madrid ndio iko mbele kwenye mbio za kuwania saini ya mchezaji huyo.

Na katika kuonyesha kwamba inahitaji huduma ya Werner, Madrid imetangaza na ofa ambayo itaitoa kwa Leipzig, ili kukamilisha mchakato wa usajili huo katika kipindi cha majira ya joto.

Tayari Werner alikuwa ameshasaini mkataba mpya wa kuendelea kubakia katika klabu hiyo ya Ujerumani, lakini taarifa zinasema kuwa kwenye mkataba wake kuna vipengele ambavyo vinaitaka Leipzig kumuuza endapo makubaliano yatafanyika.

Gazeti hilo la Hispania limeandika pia Zidane anaonekana 'kuvurugwa' na hali ya majeruhi inayomsumbua, Luka Jovic, ambaye alisajiliwa na timu hiyo katika majira ya joto mwaka jana.

Mserbia huyo pia anatajwa hajawa fiti tangu alipotua Madrid na hivyo amekosa namba katika kikosi hicho cha Zidane.

## ZISIKUPITE

### UNITED YAMGANDA FERNANDES

MANCHESTER United inajiandaa tena kufanya mchakato wa kuwania saini ya kiungo mchezeshaji wa Sporting Lisbon na Timu ya Taifa ya Ureno, Bruno Fernandes, ambaye ana umri wa miaka 25. ***(Goal.com)***

### BOATENG ANUKIA ARSENAL

ARSENAL imewasiliana rasmi na mabingwa wa Bundesliga, Bayern Munich kwa kuwaeleza nia yao ya kumsajili beki wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Jerome Boateng (31). ***(Footmercato - in French)***

### ALABA ANUKIA CHELSEA

CHELSEA inajiandaa kumsajili beki wa kushoto wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Austria, David Alaba, ambaye amebakiza miezi 18 katika mkataba wake. ***(Mirror)***

### OLMO AGOMBEWA ULAYA

BARCELONA imetajwa kuongoza katika mchakato wa kuwania saini ya nyota wa Dinamo Zagreb, Dani Olmo, licha ya Chelsea na Manchester United wakiwa pia kwenye mazungumzo ya kumsajili mshambuliaji huyo Mhispania mwenye umri wa miaka 21. ***(Goal.com)***

### LINGARD ATUA KWA RAIOLA

KIUNGO wa Manchester United na Timu ya Taifa ya England, Jesse Lingard (27), amejumuishwa kwenye nyota wanaotafutiwa timu na wakala Mino Raiola, kufuatia tetesi zilizopo za nyota huyo kutaka kuondoka Old Trafford. ***(Mail)***

### JUVENTUS YAJIPA ICARDI

JUVENTUS ina matumaini itafanikiwa kupata saini ya straika wa Timu ya Taifa ya Argentina, Mauro Icardi, kutoka Inter Milan, licha ya Paris St-Germain kuwa na makubaliano ya kumsajili nyota huyo mwenye umri wa miaka 26 ambaye thamani yake ni pauni milioni 59.7 mwishoni mwa msimu baada ya kumalizika kwa mkataba wake wa mkopo. ***(Mail)***

### GAYLE KUTUA PRESTON

MSHAMBULIAJI wa Newcastle United, raia wa England, Dwight Gayle (29), anahusishwa na mpango wa kujiunga na klabu ya Preston ambayo imepanda daraja kutoka katika Ligi ya Championship. ***(Lancashire Evening Post)***

### ZIYECH KUONDOKA AJAX

KIUNGO wa Ajax na Timu ya Taifa ya Morocco, Hakim Ziyech (26), ameelezwa anaweza kuondoka katika klabu hiyo mwezi huu, baada ya nyota huyo kuhusishwa na mpango wa kujiunga na Arsenal pamoja na Tottenham Hotspur katika dirisha dogo la usajili la Januari. ***(Football. London)***

### BARBOSA AKARIBIA CHELSEA

CHELSEA imemtaja straika wa Inter Milan na Timu ya Taifa ya Brazil, Gabriel Barbosa (23), kuwa ni mchezaji namba moja katika orodha ya nyota wapya inaowahitaji kwenye usajili wa Januari, huku Kocha Frank Lampard akisisitiza anahitaji mshambuliaji mpya. ***(Express)***

### GIROUD SAFARI IMEIVA

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard, amefungua milango kwa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Olivier Giroud (33), kuondoka katika klabu hiyo mwezi huu, huku kukiwa na tetesi kwamba anatakiwa na Aston Villa. ***(Birmingham Mail)***




Bondia Mfaume Mfaume (katikati), akitaka kupigana 'kavu kavu' na mpinzani wake, Ramadhani Jonsina (kulia), wakati wa utambulisho wa pambano lao litakalofanyika Februari 28, mwaka huu jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

## Mlandege yatarajia makubwa Mapinduzi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BENCHI la Ufundi la Mlandege limesema kuwa wamefurahi kupata nafasi ya kushiriki katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi mwaka huu kwa sababu yatawasaidia kuimarisha kikosi chao.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Jaala Abdallah, alisema michuano hiyo inasaidia kuwaongezea uzoefu wachezaji wao na mara watakaporejea kwenye Ligi Kuu Zanzibar, wanakuwa wako tayari kusaka matokeo mazuri.

Abdallah alisema huu ni mwaka wa pili kwa kikosi chake kupata nafasi ya kushiriki michuano hiyo na wanaamini msimu huu watapeperusha vema bendera ya Zanzibar katika mashindano hayo.

"Michuano hii ni muhimu kwetu, inawapa wachezajii uzoefu kwa sababu wanakutana na wenzao wanaoshiriki ligi za nje ya Zanzibar, kiufundi ni sehemu nzuri ya kuimarisha vikosi vyetu," alisema Abdallah.

Mlandege ilitarajia kuanza kampeni ya kuwania kombe hilo jana kwa kuwakaribisha mabingwa watetezi Azam FC kwenye Uwanja wa Amaan jana saa 2:15 usiku.

# JAMHURI FC YAPANIA KUFUTA SITA ZA YANGA

**Na Isaac Kijoti,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa Jamhuri, Mustafa Hassan maarufu 'Mu', amesema licha ya ubora wa Yanga huku ikiwa na wachezaji wengi wazoefu, mpira ni dakika 90 na lolote linaweza kutokea watakapokutana leo.

Timu hizo leo zitashuka katika Uwanja wa Amaan visiwani hapa katika kinyang'anyiro cha Kombe la Mapinduzi kilichoanza kutimua vumbi jana kwa Azam FC kuvaana na Mlandege huku Mtibwa Sugar ikimenyana na Chipukizi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mu alisema hawataraji kufanya makosa kama ilivyokuwa mwaka jana na wamejiandaa kushinda mechi hiyo.

**Alisema wamekuja kushindana na anamheshimu Boniface Mkwasa, Kaimu Kocha Mkuu wa Yanga, lakini hilo haliwezi kuwa kikwazo cha ushindi kwao.**

"Yanga ni timu kubwa lakini mpira ni dakika 90 na tumejiandaa kushindana na kufanya vizuri mwaka huu," alisema.

Naye nahodha wa Jamhuri, Mohamed Juma Mohamed, alisema lolote linaweza kutokea na wamejiandaa vizuri kupambana na kutofanya makosa kwa kuruhusu mabao sita kama mwaka jana.

"Tupo vizuri na hatutarajii kukutana tena na bao sita kama mwaka jana tulivyocheza dhidi ya Yanga," alisema.

Kwa upande wake nahodha wa Yanga, Said Makapu, alisema wanaiheshimu Jamhuri kwa kuwa ni timu nzuri lakini lengo lao ni kushinda na kufika hatua ya fainali.

Azam FC ndio mabingwa watetezi wa mashindano hayo ambayo mwaka huu yanashirikisha timu nane za hapa nchini na yanachezwa kwa mtindo wa mtoano.

## Simba SC yatakiwa kuisahau Yanga

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba umewataka mashabiki na wanachama wa klabu hiyo kusahau matokeo ya mchezo uliopita dhidi ya watani zao, Yanga na kuweka mawazo yao kwenye mashindano ya Kombe la Mapinduzi.

Simba inatarajia kuanza kampeni ya kuwania ubingwa wa michuano hiyo kwa kuwavaa Zimamoto katika mchezo wa Kundi B utakaochezwa kwenye Uwanja wa Gombani, Kisiwani Pemba.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema kwa sasa wanaelekeza nguvu zao katika michuano hiyo ambayo itamalizika Januari 13, mwaka huu na bingwa kupata zawadi ya Sh. milioni 15.

"Naomba mashabiki wetu wasahau yaliyotokea Jumamosi katika mechi ya watani, hayo yamepita, sasa tugange yajayo," alisema Rweyemamu.

Meneja huyo alisema makosa yaliyojitokeza katika mechi hiyo iliyochezeshwa na refa Jonesia Rukyaa, yameshafanyiwa kazi na sasa wataanza mashindano ya Kombe la Mapinduzi wakiwa imara.

"Mwalimu ameufanyia kazi upungufu wote uliyojitokeza tulipokutana na Yanga, lengo ni kufanya vizuri katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi," alisema meneja huyo.

Alisema pia mbali na michuano hiyo, wanajipanga kuendeleza kasi ya ushindi mara watakaporejea kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara hapo wiki ijayo.

# Michezo

Jumanne Januari 7, 2020

Nipashe




## Madrid yajiandaa kumnasa Werner

HABARI UK.30



Kiungo mshambuliaji mpya wa Liverpool, Takumi Minamino (kushoto), akipambana kuwania mpira dhidi ya beki wa Everton katika mechi ya Kombe la FA iliyochezwa juzi mchana. Liverpool ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

## Straika mpya Yanga usipime

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha inarejesha ufalme wake kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano mbalimbali, uongozi wa Yanga umesema kuwa bado unaendelea kusajili wachezaji wenye kiwango cha juu kwa lengo la kukiimarisha kikosi chao, imefahamika.

Kauli hiyo ya Yanga imetolewa jana baada ya kumpokea mshambuliaji mpya kutoka TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Owe Bonyanga.

Straika huyo alikuwa mmoja wa wachezaji muhimu wa Kocha wa TP Mazembe, Pamphile Mihayo, kwenye mechi za mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika mwaka jana.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mjumbe wa Kamati ya Mashindano ya Yanga, Hersi Said, alisema kuwa Bonyanga, amekuja katika mazungumzo na endapo wataafikiana, atasaidia mkataba mpya wa kuanza kuitumikia timu yao.

Said alisema kuwa lengo la Yanga ni kuimarisha kikosi chao ili waweze kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano yote watakayoshiriki mwaka huu.

Alisema nyota huyo alitarajiwa kusafiri jana jioni kuelekea Zanzibar ili kuungana na wachezaji wengine wa timu hiyo ambayo leo usiku watashuka dimbani kuikabili Chipukizi kwenye mchezo wa kwanza wa Kombe la Mapinduzi.

# Simba, Yanga vitani Mapinduzi

**Na Isaac Kijoti,** ZANZIBAR

## ●●● Zapania kuipoka Kombe Azam, zapeleka vikosi kamili zikishuka dimbani Pemba na Unguja, huku....

BAADA ya kutoshana nguvu kwa sare ya mabao 2-2 kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara, miamba ya soka nchini, Simba na Yanga zimehamishia vita mpya kwenye mashindano ya Kombe la Mapinduzi visiwani Zanzibar.

**Katika michuano hiyo iliyoanza kutimua vumbi visiwani hapa jana, licha ya timu hizo kupangwa makundi tofauti, kila moja imejigamba kulibeba taji hilo linalowaniwa na timu nane mwaka huu.**

Yanga ambayo ipo Kundi A sambamba na Azam FC, Mlandege na Jamhuri itashuka dimbani leo usiku kuvaana na Jamhuri kwenye Uwanja wa Amaan mjini Unguja.

Na kwa upande wa Simba ambayo ipo Kundi B sambamba na Mtibwa Sugar na Chipukizi itavaana na Zimamoto katika Uwanja wa Gombani kisiwani Pemba.

Hata hivyo, miamba hiyo ya Tanzania Bara msimu huu imeeleza kupania kutwaa ubingwa huo, ambao unashikiliwa na mabingwa watetezi, Azam FC ambayo jana usiku ilivaana na Mlandege katika Uwanja wa Amaan.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jana kutoka visiwani hapa, mameneja wa timu hizo kongwe nchini, walijinasibu kutofanya makosa mwaka huu katika kinyang'anyiro hicho.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, akizungumza na waandishi wa habari alisema lengo lao ni kubeba Kombe la Mapinduzi na kwa kuonyesha dhamira hiyo wamekuja visiwani hapa na kikosi kamili.

"Leo (juzi) tumetangulia na wachezaji 17 wote hawa ni wa timu ya wakubwa isipokuwa mmoja tu ndiye anatoka timu B, wachezaji wangine watakuja baadaye.

"Wachezaji waliobaki Dar es Salaam ni wale tu walionza katika kikosi cha kwanza dhidi ya Yanga Jumamosi, ambao nao watawasili na kocha anaweza kuwatumia katika mechi ijayo (kama itasonga mbele)," alisema Rweyemamu.

Kwa upande wake Meneja wa Yanga, Abeid Mziba, alisema mwaka jana walileta Kikosi B, lakini mwaka huu wamekuja visiwani hapa wakiwa na kikosi kamili cha wakubwa.

"Lengo letu ni kutwaa ubingwa na tofauti na mwaka jana, mwaka huu tumekuja na kikosi kamili kuna wachezaji wachache tu tunatarajia wataungana na wenzao leo (jana) akiwamo Yondani (Kelvin).

"Mashabiki wetu wajitokeze kwa wingi kuja kuishangilia timu na tunaamini kwa mechi ya kesho (leo) dhidi ya Jamhuri, uzoefu na ukongwe utatubeba," alisema nyota huyo wa zamani wa Yanga na Taifa Stars.

Michuano hiyo iliyoanza jana kwa Mtibwa Sugar kuvaana na Chipukizi katika Uwanja wa Gombani huku Dimba la Amaan Azam FC ikipepetana na Mlandege, mwaka huu inachezwa kwa mfumo wa mtoano.

Fainali ya michuano hiyo itapigwa katika Uwanja wa Amaan Januari 13, mwaka huu kwa kumkutanisha mshindi wa Kundi A na wa Kundi B kutoka Pemba.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >